Nipashe
Alhamisi Aprili 9, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580201
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Anyonga mkewe hadi kufa, naye ajinyonga, waacha watoto watatu

UKURASA 3




UKURASA 13

# Kina Mbowe wakata rufani Mahakama Kuu

• **Ni** kesi ya uchochezi waliyokamuliwa mamilioni Korti ya Kisutu...*Endelea ukurasa 2*




### BAA LA CORONA

**HALI ya wasiwasi imelikumba Bunge la Kenya baada ya ripoti kuonyesha kuwa wabunge na wahudumu 17 wameambukizwa virusi vya corona. DW**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Mafanikio miaka 4 ya JPM Tamisemi Yaanikwa

UKURASA 8




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipokea lita 50,000 za mafuta kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya mafuta ya Puma Energy Tanzania, Dominic Dhanah (wa pili kushoto) na Meneja Uzalishaji wa kampuni hiyo, Lameck Hiliyai (kulia), ukiwa mchango wa kuunga mkono mapambano dhidi ya ugonjwa wa (COVID -19) nchini, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

# China, wadau waipiga jeki Tanzania janga la corona

UK.2

**MICHEZO** SIMBA YAFUNGUKA MABILIONI YA MO UK.32
**MAONI, KATUNI** UK.6

# ...Wadau wasaidia bil. 6/- za corona

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amepokea kutoka kwa wadau, msaada wa fedha pamoja na vifaa mbalimbali kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19) wenye thamani ya Sh. bilioni 6.226.

Baada ya kupokea msaada huo, Waziri Mkuu aliwashukuru wadau hao kwa kuunga mkono juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya virusi vya corona, ambapo hadi sasa kesi 24 zimeripotiwa tangu kuanza kwa ugonjwa huo nchini, na wagonjwa watano wamepona.

Waziri Mkuu alipokea msaada huo jana katika Ofisi Waziri Mkuu Mlimwa, jijini Dodoma na kuwataka Watanzania waendelee kushirikiana na Serikali katika kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema hadi sasa jumla ya watu 396 wapo kwenye karatini katika maeneo mbalimbali yaliyotengwa wakiwamo wageni wanaoingia nchini, ambao wanafuatiliwa afya zao na baada ya siku 14 kama watakuwa hawana maambukizi wataruhusiwa kuungana na familia zao.

Waziri Mkuu alisema Serikali imeendelea kuchukua tahadhari katika kupambana na ugonjwa wa COVID-19, na kwa sasa imejiimarisha kwenye utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kujikinga na virusi vya corona.

Kadhalika, aliwataka wakazi wa mkoa wa Dar es Salaam waendelee kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo ili kuzuia usisambae kwa sababu hadi sasa mkoa huo unaongoza kwa kuwa na wagonjwa zaidi wa corona nchini.

Pia, Waziri Mkuu alivishukuru vyombo vya habari nchini kwa ushirikiano wanaoutoa katika kuelimisha umma namna ya kujikinga na virusi vya corona pamoja na wasanii waliotunga nyimbo za kuelimisha umma namna ya kujikinga na ugonjwa huo.

Miongoni mwa wadau waliotoa msaada huo ni kampuni ya Madini ya Twiga iliyotoa Sh. bilioni nne, mfanyabiashara maarufu nchini Rostam Aziz ametoa sh. bilioni moja, kampuni ya Taifa Gesi imetoa sh. miloni 100 na kampuni ya mafuta ya Puma imetoa msaada wa mafuta lita 50,000 zitakazotumika katika magari yanayotoa huduma za kupambana na corona nchini yakiwamo magari ya kubebea wagonjwa.

Wengine ni kampuni ya TEHAMA ya Huawei imetoa vifaa kuendeshea mikutano kwa njia ya video ambavyo ni cloudlink camera tatu, Cloudlink Mic tatu, Cloudlink TV terminal tatu, Cloudlink Platform pamoja na Thermal Imaging Temperature Measuring System moja vyote vikiwa na thamani ya sh. milioni 940, Asasi za Kiraia (AZAKI) zimetoa Sh. milioni 79.

Waziri Mkuu kwa niaba ya Rais John Magufuli, aliwashukuru wadau hao kwa vitu mbalimbali walivyovitoa kwa ajili ya kupambana na COVID-19, akisema vifaa na fedha walizozitoa zitaisadia Serikali katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Kuhusu wadau wengine wanaohitaji kutoa misaada, Waziri Mkuu alisema ofisi yake iko wazi, pia wanaweza kupeleka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, na kwa walio nje ya nchi au sehemu yoyote wanaweza kutuma fedha kupitia akaunti Na: 9921159801 yenye jina la National Relief Fund Electronic.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu akijaribu kifaa cha kupimia joto la mwili, baada ya kukabidhiwa msaada wa vifaa kinga kwa ajili ya kuendelea kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19, kutoka kwa Balozi wa China nchini, Wang Ke (kushoto), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kina Mbowe wakata rufani Mahakama Kuu

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO wanane wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, wamekata rufani Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, kupinga hukumu ya kulipa faini ya jumla ya Sh.milioni 320 au kwenda jela miaka mitano kwa Kila kosa.

Vigogo hao wa Chadema walikutwa na hatia Machi 8, mwaka huu na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, hivyo kutakiwa kwenda jela au kulipa jumla ya kiasi hicho cha fedha.

Rufani hiyo iliyosajiliwa kwa namba 76 mwaka huu, iliwasilishwa na wakili wa walalamikaji, Peter Kibatala, ikiwa na sababu 14, bado inasubiri kupangiwa jaji wa kuisikiliza.

Kwa mujibu wa hati ya rufani, walalamikaji wanadai kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, ilikosea kuwatia hatiani Mbowe na wenzake kwa sababu haikuchambua ushahidi wa Jamhuri wakati wa kuandika hukumu hiyo. Hoja nyingine, Mahakama ya Kisutu katika hukumu yake haikuonyesha sababu zilizopelekea washtakiwa kutiwa hatiani.

"Upande wa Jamhuri ni jukumu lao kuthibitisha makosa bila kuacha shaka na kwamba si kazi ya mshtakiwa kujitetea," inaeleza sehemu ya hoja za walalamikaji. Hoja nyingine, Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, hakutilia maanani utetezi wa washtakiwa akiwamo Esther Matiko na John Mnyika katika ushahidi wa Jamhuri hakuna ulipoeleza kama washtakiwa walikuwapo kwenye tukio.

Pia, mahakama ilikosea kuwatia hatiani washtakiwa katika shtaka lililokuwa na mashtaka manne ndani yake ikiwamo kufanya maandamano, kusababisha kifo cha Akwilina Akwilin, kusababisha askari polisi wawili kujeruhiwa.

Hoja nyingine kwamba mahakama ilipokea CD iliyoonyesha maandamano ya washtakiwa kinyume cha sheria na kwamba utaratibu wa kisheria haukufuata kielelezo hicho kilipokelewa kiholela.

Mbali na Mbowe, Matiko, Mnyika, washtakiwa wengine ni Mchungaji Peter Msigwa, Halima Mdee, John Heche, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, na Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya. Pia alikuwapo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vincent Mashinji, ambaye hata hivyo, alishahamia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika kesi ha msingi, Mbowe na viongozi wenzake walishtakiwa kwa mashtaka 12 ya uchochezi na moja la kula njama.

Mashtaka 12 yaliyokuwa yakiwakabili katika shtaka la kula njama, wanadaiwa kufanyika kati ya Februari Mosi na 16, mwaka 2018 wakiwa Kinondoni Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani kwa kutenda kosa la jinai na kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Bulaya anakabiliwa na shtaka la kushawishi kutenda kosa la jinai ambapo anadaiwa Februari 16, mwaka huo, katika viwanja vya Buibui Kinondoni Dar es Salaam, alishawishi wakazi wa Kinondoni kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Nchimbi alidai washtakiwa wote Februari 16, mwaka huo, wakiwa katika barabara ya Kawawa, Kinondoni Mkwajuni, Dar es Salaam, kwa pamoja wakiwa walikusanyika kutekeleza lengo kinyume cha sheria, kwa kuendelea na mkusanyiko hali iliyowafanya watu waliokuwa kwenye eneo hilo waogope uwezekano wa kuwapo uvunjifu wa amani.

# China yaipiga jeki Tanzania corona

**Na Mary Geofrey**

UBALOZI wa China nchini Tanzania, umeipatia serikali msaada wa vifaa kinga kwa ajili ya kuendelea kupambana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid 19 (Corona).

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akipokea msaada huo jana jijini Dar es Salaam, alisema utaenda kwa watumishi wa afya kote nchini ambao serikali imewapa kipaumbele cha kwanza ili kuwakinga na maambukizi ya Covid-19.

"Kwa niaba ya serikali tunaishukuru sana Serikali ya China kwa mchango huu na niendelee kuwathibitishia wale wote mnaoisaidia Serikali ya Tanzania, msaada huu tutaupeleka kwa watumishi wa afya, kipaumbele ni kuwakinga watumishi wa afya wasipate maambukizi,"alisema Ummy.

Ummy alisema msaada huo uliotolewa na ubalozi wa China nchini Tanzania ni pamoja na mavazi (PPE) 1,000 ya kujikinga wakati wa kuhudumia watu waliothibitika kuwa na ugonjwa wa corona, barakoa (mask) 100,000 pamoja na vipima joto vya mkono (thermal scanner) 150.

Kwa upande wake Balozi wa China nchini Tanzania, Wang Ke, alisema nchi yake na Tanzania ni marafiki kwa muda mrefu na ugonjwa huo ulipoikumba nchi yao kwa mara ya kwanza, Tanzania ilikuwa mstari wa mbele kuwaunga mkono dhidi ya mapambano hivyo na wenyewe wamejitoa kuisaidia kukabiliana nao.

Wang Ke alisema Serikali ya China kwa sasa imechukua hatua na kujitoa rasmi kuwa nchi itakayoisaidia Tanzania katika misaada ya dharura ya vifaa kinga kukabiliana na ugonjwa wa corona.

Katika mwendelezo wa kuisadia vifaa kinga Serikali, kwa mara nyingine tena inatarajia kupokea msaada wa vifaa tiba vya kusaidia wagonjwa kupumua (Ventilator) 500 kutoka kwa mfanyabiashara raia wa China Jack Ma.

Hadi sasa jumla ya wagonjwa waliogundulika kuwa na virusi vya corona nchini ni 24, akiwamo mmoja aliyepoteza maisha, watano wamepona na wengine 18 wanaendelea kupatiwa matibabu katika vituo maalumu vilivyopo maeneo mbalimbali nchini.

HABARI KITAIFA

# NSSF yanunua shamba la mil. 400/- kwa bilioni 3.3/-

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KATIKA hali inayoashiria kuwapo kwa harufu ya ufisadi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umenunua shamba lenye thamani ya Sh. milioni 416.4 kwa Sh. bilioni 3.32.

Hayo yamebainishwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka fedha 2018/19 iliyokabidhiwa kwa Rais John Magufuli Machi 26 mwaka huu na kuwasilishwa bungeni jijini hapa Jumatatu.

Katika ripoti yake kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Januari 3 mwaka jana, iliiomba Ofisi ya CAG kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi juu ya ununuzi wa shamba lenye Namba za Umiliki 870 maeneo ya Kiluvya uliofanywa na NSSF.

Anasema ukaguzi wa ofisi yake ulijikita kwenye kuthibitisha kama kulikuwa na upotevu wa mali na hasara kutokana na ununuzi huo na ukabaini mfuko kwa ujumla ulipata hasara kubwa.

CAG Kichere alisema Septemba 16, 2010 baada ya idhini ya bodi ya ununuzi, mfuko uliingia mkataba wa ununuzi wa shamba la hekari 277 lililoko Kiluvya kwa bei ya Sh. bilioni 3.32.

Anabainisha kuwa kulingana na waraka Na. 1 wa Mei 14, 1969, uliotolewa na Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Ardhi, Mipango-Miji na Maji, ulielekeza kuwa, ili kudhibiti gharama za ununuzi wa ardhi na mauzo ya ardhi au majengo, mashirika ya umma yatahitajika kuomba ushauri (kuhusu bei ya fidia) kutoka Idara ya Uthamini katika Wizara ya Ardhi.

"Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii haukuomba ushauri wakati wa ununuzi wa shamba la Kiluvya. Ripoti ya uthamini wa ardhi kutoka Manispaa ya Temeke ambayo ilithibitishwa na Mthamini Mali wa Serikali Oktoba 28, 2010, inaonyesha kuwa thamani ya ardhi iliyonunuliwa kwa wakati huo ilikuwa ni Sh. milioni 416.4.

"Bei ya mauziano ya Sh. bilioni 3.32 ilikuwa ni kubwa kupita bei halali ya Sh. milioni 416.40. Hivyo, mfuko ulilipishwa bei ya juu kwa tofauti ya Sh. bilioni 2.90.

"Vilevile, kulingana na ajenda namba 6.11 ya mkutano wa bodi ya ununuzi, bodi ilishauri kuwa malipo ya ununuzi yafanyike kwa awamu tatu ambapo asilimia 30 italipwa wakati wa kusaini mkataba, asilimia 40 wakati wa kuhamisha miliki ya shamba, na asilimia 30 wakati umiliki utakapohama.

"Hata hivyo, kinyume cha maagizo ya bodi, Menejimenti ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ilifanya malipo kwa miamala miwili Septemba 27, 2010 na Desemba 22, 2010.

"Ninapendekeza kuwa Menejimenti ya Mfuko ichukue hatua stahiki kuhakikisha inarudisha kiasi cha fedha cha ziada kilicholipwa wakati wa ununuzi wa shamba na ichukue hatua stahiki za kisheria kwa watumishi wa mfuko na muuzaji wa shamba waliosababisha hasara kwa mfuko," anashauri.



Mfanyabiashara wa samaki soko kuu la Manispaa ya Iringa, Ngwei Msungu, akipanga samaki kwa ajili ya kuwauza jana, samaki wamekuwa wa shida katika soko hilo kutokana na bwawa la Mtera linalotegemewa kujaa maji kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mume amnyonga kwa mikono mkewe hadi kufa, naye ajinyonga

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WANANDOA wawili wakazi wa Kitongoji cha Logoto, wilayani Kiteto, mkoani Manyara, wamefariki dunia baada ya mume kumuua mkewe kwa kumnyonga naye kujinyonga kwa sababu ya wivu wa kimapenzi.

Shedrack Sekeyani (40) alimnyonga mke wake Magdalena Sirai (30), kwa mikono hadi kumuua kisha naye kujinyonga kwenye mti kwa kutumia kanga.

Mmoja kati ya mashuhuda wa tukio hilo, Hassan Juma, akizungumza jana alisema tukio hilo lilitokea Aprili 6, majira ya usiku wakati wakigombana kwa kile kinachodaiwa ni wivu wa kimapenzi.

Alisema marehemu wameacha watoto wanne ambao ni Ziki Sekeyani (3), Babu Sekeyani (5), Faraja Sekeyani (7) na Rejina Sekeyani (12).

Mmoja kati ya watoto wa marehemu hao Rejina alisema usiku wa tukio kulikuwa na ugomvi baina ya baba na mama yao na chanzo chake hawakukifahamu.

Regina alisema katika ugomvi uliotokea usiku huo baba yao alianza kumpiga mama yao na wao waliwaomba waache ugomvi, lakini baba yao hakuwasikiliza na kuendelea kumpiga mama yao.

"Tulianza kupiga kelele baba akatukataza tukanyamaza kwa hofu ndipo akamnyonga mama kwa mikono tukiwa tunashuhudia tukio hilo tukadhani amelala akatuambia tulale ndipo akatoka nje," alisema.

Alisema walipoamka asubuhi saa 12 walikuta baba yao amefariki dunia kwa kujinyonga kwenye mti nje ya nyumba yao.

Mmoja kati ya majirani wa marehemu hao, Mariam Hussein, alisema matukio ya kujinyonga yanazidi kujitokeza kwa kuwa hivi karibuni mwanamke wa eneo alijinyonga.

Alisema hivi sasa maisha ya watoto hao yapo kwenye wakati mgumu kwa kuwa wazazi wote wawili wamefariki mustakabali wa maisha yao haujulikani.

Mjomba wa watoto wao, Samson Tuma alisema, hivi sasa ndiye anaishi na watoto hao wakisubiri uamuzi wa ndugu wengine utakavyoamua namna watakavyoishi, baada ya mazishi ya wazazi wao.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Paul Kasabago, alikiri kutokea kwa tukio hilo.

"Nawaasa wananchi wa mkoa huu wa Manyara waachane na mtindo wa kuchukua sheria mkononi kwa kuwa wangeweza kukaa na kusuluhisha ugomvi wao ku-

# CAG afichua wanyamapori maelfu wanavyouawa ajali za barabarani

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini ufuatiliaji duni wa mauaji ya wanyamapori kupitia ajali za barabarani nchini.

Katika ripoti yake kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, CAG Kichere anasema Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) linakabiliwa na tatizo la mauaji ya wanyamapori kutokana na ajali hizo, akibainisha kuwa jumla ya wanyamapori 2,266 waliuawa katika mwaka mmoja tu ulioishia Juni 30, 2019.

Anasema pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa mauaji ya wanyamapori unaofanywa na Tanapa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwenye barabara kuu, bado kuna matatizo mbalimbali yanayosababishwa na kuwa na teknolojia duni kama vile kukosa kamera za barabarani, jambo linalosababisha kushindwa kutambua wahusika wanaosababisha ajali hizo.

"Mapitio yangu ya ripoti ya kitengo cha ulinzi wa wanyamapori, yaligundua kuwa katika Hifadhi ya Taifa Mikumi (Minapa), jumla ya wanyamapori 124 wa aina tofauti waliuawa katika kipindi cha robo tatu ya mwaka.

"Kutokana na idadi hiyo ya vifo vya wanyamapori mbalimbali, Hifadhi ya Taifa Mikumi ilitakiwa kupokea kiasi cha fedha Sh. milioni 56.64 za tozo na adhabu za kusababisha ajali. Hata hivyo, hifadhi hiyo ilipokea Sh. milioni 12.45 tu, sawa na tofauti ya Sh. milioni 44.18.

"Menejimeti ilieleza kwamba, ajali nyingi za barabarani zinatokea wakati wa usiku, hivyo kushindwa kuwaona wanaofanya makosa kutokana na kukosekana kwa kamera za ulinzi.

"Vilevile, katika hali nyingine, malipo yalikuwa yanajadiliwa kutokana na ukweli kwamba Tanapa haina sheria ndogo za kutoza faini na adhabu, ambapo tozo au faini hutolewa kulingana na Kanuni za Taifa za Uhifadhi wa Wanyamapori, ambazo hazimfungi mtu katika mahakama za sheria.

"Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania na Mamlaka ya Uhifadhi Ngorongoro zitunge sheria ndogo na kuzisimamia ipasavyo. Vilevile, zibuni na kusimamia njia mbalimbali za usalama kama vile kuweka kamera za barabarani ili kudhibiti ajali za barabarani na hivyo kulinda wanyamapori," anashauri.

# Walio karantini wadaiwa kutafuta chakula mitaani

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu, Emmanuel Maganga, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama mkoani humo kuimarisha ulinzi katika maeneo yaliyotengwa kama karantini kufuatia uwapo wa taarifa za baadhi ya watu walio kwenye karantini kuonekana wakitafuta chakula mtaani.

Maganga aliyabainisha hayo wakati wa ziara yake Bandari ya Kibirizi ya usafirishaji mizigo kwa boti katika Ziwa Tanganyika kwenda maeneo mbalimbali ikiwamo nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasi Kongo na Burundi.

Alisema inapaswa mabaharia kuzingatia utaratibu wa karantini katika maeneo yaliyochaguliwa pamoja na kuzingatia usalama wao na wananchi wengine.

"Tunataarifa kule wanakimbia kwenda kutafuta chakula, tunazo taarifa tena sio za kintelejesia za kawaida, watu wanatoka kwenda kutafuta chakula," alisema.

Vile vile, Maganga alikataa ombi la wasafirishaji wa maboti la kuwekwa karantini katika vyombo vyao vya usafirishaji kutokana na vyombo hivyo kutokuwa na huduma muhimu kama choo na kuwapo uwezekano wa mabaharia kutoroka.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Simon Chacha, alibainisha kuwa hadi sasa katika mkoa huo jumla ya watu 61 wamewekwa karantini wakiwamo mabaharia wa usafirishaji wa vyombo majini wanaoenda katika nchi jirani.

Mwenyekiti wa umoja wa wasafirishaji wa maboti Kigoma, alibainisha kupata hasara kutokana na gharama za kuwahudumia wafanyakazi wao wanaokuwa katika karantini na kuomba kupunguza gharama.

Watu waliwekwa karantini katika mkoa huo ni Watanzania 53, kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (6) na Burundi (2).



Wasamaria wema wakisaidia kulisukuma lori baada kuharibika katikati ya barabara ya Uhuru, eneo la Buguruni Rozana, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uboreshaji daftari mikoa 12 wiki ijayo

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili na uwekaji wazi wa lile la awali unatarajia kuanza Aprili 17, kwa mikoa 12.

Mwenyekiti wa Tume, Jaji mstaafu, Semistocles Kaijage, alisema hayo jana na kueleza kuwa, utekelezaji wa uboreshaji wa daftari hilo utafanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe hiyo.

Jaji Kaijage alisema hayo wakati alitoa mrejesho wa kikao kilichofanyika Machi 23, mwaka huu ambacho kilihudhuria na viongozi wa vyama vya siasa ambao pamoja na mambo mengine walijadili masuala hayo mawili.

Alisema michakato hiyo itafanyika kwa siku tatu kwenye kila mkoa na katika awamu (route) mbili badala ya tatu zilizopangwa awali.

Alisema ya kwanza itafanyika kwa siku tatu kuanzia Aprili 17, na kuhusisha mikoa 12 na vituo vya uandikishaji 2005.

Aliitaja mikoa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Mara, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Kigoma na Tabora.

Alisema awamu ya pili nayo itafanyika kwa siku tatu kuanzia Mei 2 na itahusisha mikoa 14 ya Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar.

"Tanzania Bara kutakuwa na vituo vya kuandikisha wapiga kura vipatavyo 2001 na mikoa ni Katavi, Rukwa, Singida, Dodoma, Iringa, Songwe, Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam," alisema.

Alisema jumla ya vituo ambavyo vitatumika kwa uandikishaji ni 4006 badala ya vile 8031 walivyoeleza awali.

"Kati ya vituo hivyo, 3,956 ni kutoka Tanzania Bara na 50 Zanzibar, leo tutawakabidhi orodha mpya ya vituo hivi vipya, ile mliokabidhiwa awali haitatumika," alisema.

Alisema hayo yamefanyika baada ya kushauriana na wadau na kukubaliana waendelee na machakato huo kwa kuzingatia athari za virusi vya corona.

"Tumeshanunua vifaa vya kujikinga na ugonjwa huu na kutoa maelekezo kwa watendaji kuzingatia miongozo ya afya. Uwekaji wazi daftari la awali utakwenda sambamba na uboreshaji wa Daftari awamu ya pili ambao utaanza rasmi Aprili 17, mwaka huu na kukamilika Mei 4 nchi nzima."

Alisisitiza kuwa uboreshaji huo utafanyika kila kata ambapo kutakuwa na Mwandishi Msaidizi na waandikishaji BVR Kit watakaokuwa na orodha ya vituo vyote katika kata.

"Watakuwa na uwezo wa kuboresha taarifa za wapigakura kwa yoyote atakayefika kituoni,"alisema.

Pia alisema uwekaji wazi wa daftari la awali, orodha yake itabandikwa katika kila kituo kilichotumika kuandikisha wapiga kura wa kwanza.

Alisema utaratibu wa kuweka pingamizi kwa aliyeandikishwa utafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 24 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na kifungu cha (3d1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

# CAG asema mapato ya T-Pesa yamepotoshwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini upungufu katika ukokotoaji wa ada ya mauzo ya muda wa maongezi iliyopatikana katika mkataba wa Shirika la Mawasiliano ya Simu (TTCL) na Kampuni ya TTCL Pesa (T-Pesa).

Katika ripoti yake kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, CAG Kichere anasema Kifungu cha 9.2 cha mkataba wa mauzo ya vocha za kieletroniki kati ya TTCL na T-Pesa, kinataka ada ya mauzo ya muda wa maongezi kujumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na ikokotolewe kwa kuangalia mauzo yaliyofanywa na T-Pesa.

"Hata hivyo, uhakiki wangu wa ada ya mauzo ya muda wa maongezi iliyopatikana, ulibaini kuwa ada inakokotolewa kwa kuzingatia muda wa maongezi wa kieletroniki uliotoka TTCL na si mauzo halisi yaliyofanywa na T-Pesa kama ilivyoainishwa katika Mkataba.

"Menejimenti ya T-Pesa imeeleza kuwa mpangilio wa sasa unatokana na makubaliano ya mdomo kati ya pande mbili ambayo bado hayajaingizwa kwenye mkataba.

"Kutokana na mkataba uliopo, ni maoni yangu kuwa mapato ya T-Pesa yanaweza kuwa yamepotoshwa," anasema.

CAG anapendekeza Menejimenti ya T-Pesa ifanye mabadiliko kwenye mkataba uliopo ili kuingiza makubaliano mapya au ikokotoe ada kwa kuzingatia vigezo vya mkataba uliopo.

Pia, anasema amebaini kukosekana kwa ukokotoaji huru kwa riba inayopatikana katika akaunti za udhamini, akifafanua kuwa sehemu ya 2.6 ya mkataba kati ya T-Pesa na Taasisi ya Udhamini ya TTCL Pesa (T-Pesa Trust) na benki (NMB, CRDB, TPB na TIB), inataka riba ikokotolewe kila siku kwa kuzingatia bakaa iliyopo kwenye akaunti na iwekwe kwenye akaunti ya udhamini kila mwisho wa mwezi.

Hata hivyo, CAG anasema hakukuwa na ushahidi kutoka kwa menejimenti ya Taasisi ya Udhamini ya T-Pesa Trust unaoonyesha kuwa kuna utaratibu wa kuhakikisha kuwa riba inayopatikana ni sahihi badala ya kutegemea kile kinachowekwa na benki katika akaunti ya udhamini.

"Nilibaini matukio matatu ambapo riba iliyopatikana ililazimika kuongezwa kwenye akaunti baada ya kubainika kuwa moja ya benki husika iliweka riba pungufu.

"Kushindwa kwa menejimenti ya Tasisi ya Udhamini (T-Pesa Trust) kufanya ukokotoaji huru, kunaweza kusababisha hasara kwa taasisi kama itatokea upunguzaji wa mapato hautabainika.

"Ninapendekeza Menejimenti ya Taasisi ihakikishe kuna ukokotoaji wa riba kila siku ili kuwe na usahihi na ukamilifu wa riba inayowekwa katika akaunti ya udhamini," anasema.

BancABC part of atlasmara

# TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Mwaka uliopita 31-Dec-18 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 3 572 | 2 895 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12 790 | 18 426 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 33 052 | 40 609 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 97 838 | 77 894 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 127 755 | 142 159 |
| | - | - |
| 12 Mali Nyingine | 26 548 | 21 343 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 1 000 | 1 000 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6 639 | 16 278 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **309 194** | **320 603** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 92 642 | 92 378 |
| 18 Amana za Wateja | 99 021 | 107 641 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 Dhima Nyingine | 4 356 | 5 302 |
| 28 Madeni | 69 553 | 64 675 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **265 571** | **269 996** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **43 623** | **50 607** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 105 114 | 98 174 |
| 32 Hisa za Upendeleo | 17 840 | 17 840 |
| 33 Akiba ya Mtaji | - | 1 284 |
| 34 Hifadhi ya hatari ya benki kuu | 130 | 1 284 |
| 35 Mapato Yaliyobakizwa | (80 526) | (67 756) |
| 36 Akaunti Nyingine za Mtaji | 1 065 | 1 065 |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **43 623** | **50 607** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 3 137 | 2 225 |
| 39 Mikopo Chechefu | 17 957 | 20 069 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15 351 | 17 083 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14.1% | 15.8% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 12.5% | 12.6% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 74.7% | 79.6% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 41.3% | 44.3% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.7% | 81.3% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -4.2% | -38.1% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -3.6% | -19.6% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Mwaka uliopita 31-Dec-18 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 40 926 | 48 538 |
| 2 Gharama za Riba | (19 013) | (22 785) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **21 912** | **25 752** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | (1 037) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (4 052) | (3 633) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **7 907** | **5 926** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1 901 | 1 938 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 6 006 | 3 989 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(34 392)** | **(34 209)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (10 842) | (9 940) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (1 829) | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | (21 721) | (24 268) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(8 624)** | **(7 200)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (145) | (154) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(8 769)** | **(7 355)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | (320) |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(8 769)** | **(7 675)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 154 | 157 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (883) | (780.80) |
| 15 | - | - |
| 16 Idadi ya Matawi | 7 | 7 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.74% | -2.00% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -18.30% | -11.91% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -115.33% | -107.99% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 8.47% | 9.88% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-19 | Mwaka uliopita 31-Dec-18 |
|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (8 624) | (7 200) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 9 515 | 7 771 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 10 351 | 33 468 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (8 357) | (123 001) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 7 558 | 14 378 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (17 053) | 1 555 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1 551) | (203) |
| - Kodi Iliyolipwa | (198) | (135) |
| - Mengineyo (bainisha) | 927 | 4 341 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(7 431)** | **(69 026)** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (3 540) | (5 746) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(3 540)** | **(5 746)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | 62 150.00 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 6 940.00 | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **6 940** | **62 150** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (4 031) | (12 622) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 72 780 | 85 402 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **68 749** | **72 780** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116 014** | **-** | **(67 756)** | **0** | **1 284** | **1 065** | **50 607** |
| Marekebisho yatokanayo na IFRS 9 | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la kodi litokanalo na IFRS 9 | - | - | (5 154) | - | - | - | **(5 154)** |
| **Salio la mwanzo wa mwaka lilorekebishwa** | **116 014** | **-** | **(72 910)** | **0** | **1 284** | **1 065** | **45 453** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (8 769) | - | - | - | **(8 769)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 6 940 | - | - | - | - | - | **6 940** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (130) | 130 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1 284 | - | (1 284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122 954** | **-** | **(80 525)** | **130** | **0** | **1 065** | **43 624** |
| **Mwaka Uliopita 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **98 174** | **-** | **(57 322)** | **9 119** | **1 114** | **1 384** | **52 456** |
| Marekebisho yatokanayo na IFRS 9 | | | (17 181) | | | | |
| Tengo la kodi litokanalo na IFRS 9 | | | 5 154 | | | | |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (7 355) | - | - | - | **(1 026)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 17 840 | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 9 118 | (9 118) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (170) | - | 170 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (320) | **18 878** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **116 014** | **-** | **(67 756)** | **0** | **1 284** | **1 065** | **50 607** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na KPMG, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

Taarifa hizi za fedha ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi siku ya tarehe 26 Machi 2020

I. John
(Mkurugenzi mtendaji) Imesainiwa tarehe 08 April 2020

Mr. R. Dave Imesainiwa tarehe 08 April 2020

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Fedha za msaada janga la corona zitumike vizuri

**JANA** Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alipokea fedha na vifaa kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kuisaidia serikali kupambana na homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19), vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.226.

Machi 16, mwaka huu, Tanzania ilitangaza kuwapo kwa mgonjwa mmoja wa corona jijini Arusha, na sasa watu 24 wameugua, na Aprili mosi, mwaka huu mmoja alifariki, na hadi juzi watatu kati yake wamepona na kuruhusiwa kutoka hospitalini. Hata hivyo, jana idadi iliongezeka na kufikia wagonjwa 25.

Tangu kujulikana kwa ugonjwa huo hatua za tahadhari zimechukuliwa na Serikali ikiwamo kufunga shule za awali, msingi, sekondari na vyuo na vyuo vikuu vyote nchini kwa muda wa mwezi mmoja.

Nyingine ni kuzuia semina, mikutano, warsha, makongamano na mikusanyiko yote, huku kwenye vyombo vya usafiri mijini wakikatazwa kusimamisha abiria.

Nyingine ni kuwapo kwa maji ya kunawa kwenye maduka na maofisi pamoja na watu kutembea na majitiba kwa ajili ya kujitakasa mikono.

Aidha, kampeni za kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari zimeendeshwa kila wakati, na vipeperushi vya namna ya kujikinga vikitolewa kwenye maeneo mbalimbali, yote ni kuikinga jamii dhidi ya maambukizi.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya taasisi za dini zilifanya mabadiliko ya ibada huku kukiwa na maelekezo maaluma ya kuendesha ibada hizo, lengo ni kukabiliana na corona.

Machi 29, mwaka huu, Waziri Mkuu alipokea fedha na vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.18 na kufanya jumla ya Sh. 7.406 ya zote zilizopokelewa tangu kuibuka kwa ugonjwa huo.

Akipokea msaada jana, Waziri Mkuu aliwashukuru wadau hao na kueleza kuna jumla ya watu 396 wapo kwenye maeneo ya kujitenga nchini, huku wengine waliokutana na wanaohisiwa huenda wameabukizwa wakifuatiliwa.

Aidha, alieleza kuwa ofisi yake iko wazi pia wanaweza kupeleka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, huku walio nje ya nchi wanaweza kutuma kupitia akaunti namba 9921159801 yenye jina la National Relief Fund Electronic

Pia, Ubalozi wa China nchini, ulitangaza jana kutoa msaada kwa Tanzania wa vifaa vya kujikinga na corona yakiwamo mavazi maalum, barakoa na vipima joto.

Wengi wa waliotoa misaada hiyo ni kwa ajili ya ununuzi wa vitakasa mikono, barakoa kwa ajili ya maeneo ya umma na vyombo vya usafiri.

Tunaipongeza Serikali kwa hatua iliyozichukua, pia wadau wote waliojitoa kuunga mkono mapambano dhidi ya corona ambayo inatikisa dunia kwa sasa.

Tunasisitiza ni vyema fedha zilizotolewa na zitakazoendelea kutolewa zitumike vizuri kwa jambo husika, ili kuendelea kuwatia moyo wote waliotoa kwamba zilikwenda eneo husika kwa jambo sahihi.

Haitarajiwi kukawa na ufujaji wa fedha hizo kwa wale watakaopewa dhamana ya kuzisimamia , kwa kuwa miongoni mwake kuna fedha taslimu kwa ajili ya kununua vifaa hivyo.

Pia, ni vyema ukawekwa utaratibu mzuri wa kugawa vifaa hivyo bila upendeleo kwa kuanza na wana jamii wa chini kabisa na maeneo ya mipakani pamoja na kwenye usafiri wa umma. Tunashauri vigawanywe kutumika vizuri.

Haitarajiwi kuvikosa kwenye maeneo ya vituo vya mabasi ya mikoani na maeneo husika la miji na vijijini, kwa kuwa lengo ni kuhakikisha huduma inawafikia na kujikinga dhidi ya maambukizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Mfumo dume waathiri wanawake kujieleza

Na Salome Kitomari

**USHIRIKI** wa wanawake katika nyanja mbalimbali za maendeleo siyo wa kuridhisha, kutokana na mfumo uliowakuza wa kutokupewa nafasi stahiki, licha ya kuwa na sifa wakati mwingine zilizozidi kundi jingine.

Bado jamii ya Kiafrika, Tanzania ikiwamo, inakabiliwa na mfumo dume kuanzia ngazi ya familia hadi taifa, kwa kuwa imani ni finyu kwa mwanamke kuwa anaweza kufanya jambo flani.

Hali hiyo iko hadi kwenye vyombo vya habari kwa kuangalia idadi ya vyanzo vya habari, wanawake wanaopata nafasi ya kutoa sauti zao dhidi ya jambo fulani ni wachache.

Pia, ndani ya vyombo vya habari idadi ya wanawake waliopo kwenye ngazi ya kufanya uamuzi ni ndogo na bado mfumo dume unawataka kuwa ndani ya vyumba vya habari, hujulikana kama 'dunia ya wanaume.'

Mtu anapotembelea katika shule zinazotoa mafunzo ya uandishi wa habari, kuna idadi kubwa ya waandishi watarajiwa wanawake, lakini wanapomaliza masomo hawaonekani kwenye vyumba vya habari.

Ni kwanini hilo? Hiyo inatokana na wengi kukata tamaa, kukosa wa kuwafanya wasonge mbele na kukatishwa tamaa.

Wakati mwingine ni pale wanapokosa utayari na wengi kuona kuwa kazi hiyo ni rahisi na wanakuwa na matarajio ya kuonekana kwenye luninga akisoma taarifa ya habari, licha ya kwamba hana sauti au mwonekano mzuri kwa ajili ya kazi hiyo.

Aidha, kuna changamoto kubwa ya kupata vyanzo vya habari ambao ni wanawake, wakazungumzia masuala mbalimbali kuanzia michezo, uchumi, siasa, elimu na mambo mengine mtambuka.

Mara kadhaa kuna waandishi wa habari wanapoenda kwenye tukio lolote au kutafuta habari hata kama mwanamke alishuhudia bado inakuwa vigumu kuzungumza.

Yote hayo yanatokana na mifumo iliyomkuza na kuishi kwenye akili yake kuwa, hastahili kuzungumza bila ya ruhusa ya mumewe au kusimama kishujaa kuongea mbele ya wanaume.

Hali hiyo ndiyo imelisukuma Shirika lilisilo la kiserikali la Tha Finnish Foundation for Media Development) ambalo kwa lugha ya kwao linaitwa 'Vikes' likaanzisha mradi wa kuongeza nafasi ya wanawake kwenye vyombo vya habari, unaotekelezwa kwa ushirikiano baina ya Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (Misa-Tan), Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa).

Miongoni mwa yanayofanywa na Vikes, ni kuongeza nafasi ya wanawake wanaofanya uamuzi kwenye chombo cha habari na kuongeza idadi ya vyanzo vya habari kwenye vyombo hivyo, lengo ni kuongeza sauti na uhuru wa kujieleza.

Kwanini tunaona ni muhimu sauti za wanawake zikasikika? Ni kwa sababu kundi husika, ndilo linaweza kujizungumzia na kutoa hisia zao, kuhusiana na jambo flani linalowakabili badala ya kuegejea wasemewe.

Madhara ya kutokusema ni kwamba, wataendelea kukandamizwa au kupitia changamoto ambazo kundi jingine haliwezi kuliwakilisha vyema, jambo litakaloendelea kuwa changamoto katika ustawi wao.

Ni lazima mabadiliko yaanzie kwenye vyombo vya habari kwa kuhakikisha wanawaamini wanawake waliopo na kugawa majukumu ya kazi pasipo kuangalia kwanza kigezo cha jinsia, bali uwezo wa kutenda kazi husika kama inavyotakiwa.

Iwapo jambo hilo litafanikiwa, maana yake ni kwamba itakuwa rahisi kuifikia jamii kwa kuwa sasa kupitia vyombo vya habari wataona mabadiliko, ni rahisi kujifunza kwa kuona zaidi na pale watakapokuwa wanahojiwa wataweza kujizungumzia.

Hiyo pekee haitoshi, bali vyombo vya habari vinapaswa kuendelea kuchapisha na kutangaza maudhui inayowafanya wanawake na wanaume kubadili mtazamo dhidi ya jinsia nyingine na kuona kuna usawa na kila mmoja ana haki ya kutoa hisia zake.

Mabadiliko huanza na mtu, lakini wakati mwingine kuna mabadiliko ya kitaasisi ambayo ndani yake hufanywa na watu. Hivyo basi, inapaswa kuwaamini wanawake kulingana na sifa zao za kitaaluma, pia uzoefu na siyo kulingana na 'uanamke' wao ambao ndani yake una vitu vingi.

Hali ikiwa hivyo, itapunguza au kumaliza mfumo dume unaochangia mambo mbalimbali, ikiwamo ukatili wa kijinsia dhidi ya kundi hilo na watoto.

Pia, sauti zao zitasikika na wao kuchangia katika maendeleo ya nchi.

# Bosi JamiiForums alipa faini ya mil. 3/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imemhukumu Mkurugenzi wa JamiiForums, Maxence Melo (pichani), kulipa faini ya Sh. milioni tatu au kwenda jela mwaka mmoja.

Aidha, Mahakama hiyo imemwachia huru mwanahisa mwenzake, Micke William, baada ya ushahidi wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha tuhuma za mshtakiwa huyo.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi wanne wa Jamhuri na utetezi wa washtakiwa.

Alisema mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa Jamhuri iliwaona washtakiwa wana kesi ya kujibu.

Katika utetezi wao, Mello alikiri kuwa Mkurugenzi wa JamiiForums.

Alikana tuhuma za kulinyima ushirikiano Jeshi la Polisi wakati likifanya uchunguzi kuhusu taarifa iliyotumwa katika ukurasa wa mtandao wake.

Mshtakiwa William alikana kuhusika na tuhuma hizo. Hakimu alisema kwa mujibu wa mashahidi watatu, askari polisi wa Jamhuri kwa nyakati tofauti walidai kuwaandikia barua watuhumiwa na walijibu kupitia kampuni ya uwakili ya Victori Artony. "Ni wazi kuwa kampuni hiyo ya uwakili ililijibu Jeshi la Polisi kwamba watuhumiwa wako tayari kutoa ushirikiano, lakini walipaswa kuelezwa watafanya hivyo kwa mujibu wa kifungu gani cha sheria, na kwamba hawawajibiki kutoa siri za wateja," alisema na kuongeza:

"Melo hajakataa kuwa na uhusiano na mtandao huo, majibu ya barua ya uwakili, ni wazi kuwa walipewa maelekezo ya kujibu wasingeweza kukurupuka kufanya hivyo, Mahakama hii inamtia hatiani na kumwachia huru William," alisema Hakimu Simba.

Alisema washtakiwa walipaswa kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za mtuma taarifa.

Kabla ya hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Silvia Mitanto, aliomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa. Wakili wa utetezi, Peter Kibatala, alidai kuwa mshtakiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na kwamba ana familia inayomtegemea.

Hakimu Simba alisema Melo atalipa faini na akishindwa atakwenda jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja.

Hata hivyo, Melo alilipa faini hiyo, ingawa alisema anakusudia kukata rufani kupinga hukumu hiyo.

Katika kesi ya msingi, Melo na William wanadaiwa kuzuia uchunguzi wa Polisi kwa kushindwa kutoa taarifa muhimu za Mwandishi (Mwanachama wa JamiiForums aliyejulikana kwa jina la Fahrer) aliyeandika kuhusu kampuni ya OilCom (T) Ltd ikidaiwa kukwepa kodi na kuchakachua mafuta katika bandari ya Dar es Salaam.

Polisi walikuwa wakihitaji mambo manne kuhusu Fahrer ambayo walidai yatawasaidia katika uchunguzi. Walihitaji Barua pepe ya mwanachama huyo, namba za simu, IP Address pamoja na mada nyingine zote alizowahi kuanzisha mwanachama huyo.






Mkuu wa kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic Tanzania, Thereza Majinge (kulia), akimkabidhi Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Elisha Osati (kushoto), mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 30, ukiwa ni mchango wa benki hiyo kusaidia mapambano ya ugonjwa wa homa ya virusi vya corona (Covid 19). Makabidhiano hayo yalifanyika katika makao makuu ya Benki ya Stanbic Dar es Salaam wiki hii. Katikati ni Katibu Mkuu wa MAT, Dk. Lilian Mnabwiru. **MPIGAPICHA WETU**

# Wagonjwa wa corona nchini wafikia 25

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amethibitisha kuwapo kwa mgonjwa mpya mwenye maambukizi ya virusi vya corona (Covid-19) jijini Dar es Salaam ambaye ni mwanaume (51) raia wa Tanzania.

Alisema mgonjwa huyo yupo chini ya uangalizi wa watoa huduma za afya katika kituo maalum cha tiba Dar es Salaam na wizara inaendelea kuwafuatilia watu wa karibu waliowahi kukutana mgonjwa huyo.

Alisema hadi sasa jumla ya watu 25 wamethibitika kuwa na maambukizi ya COVID-19 tangu kuingia kwa ugonjwa huo nchini. "Wagonjwa hawa ni pamoja na wale waliotolewa taarifa kutoka Zanzibar na kati yao wagonjwa wa tano wamepona na mgonjwa mmoja alifariki dunia," alisema Ummy. Alisema tangu kuanza kuripotiwa mgonjwa wa kwanza wa COVID-19 nchini, hadi kufikia jana jumla ya watu 789 waliokutana na wagonjwa wanafuatiliwa kwa karibu.

Alisema kuanzia Machi 24, mwaka huu hadi sasa jumla ya wasafiri 2,181 wamewekwa karantini nchini na kati ya hao wasafiri 324 wamemaliza siku 14 za uangalizi.

# Magereza yazungumzia mahabusi kuachiwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini, limesema haliwezi kuwaachia mahabusi bila msamaha wa Rais au hati kutoka mahakamani kama ilivyoelekezwa awali na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Hamad Masauni, wakati wa ziara katika vituo vya polisi jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa takwimu hadi jana mahabusi nchi nzima 16,480 wapo gerezani. Hivi karibuni Naibu Waziri huyo alitoa agizo kwa Polisi na Jeshi la Magereza kuachia mahabusi ambao kesi zao sio za msingi ili kupunguza msongamano kwa ajili ya kuepuka ugonjwa wa corona.

Akizungumza jana na Nipashe, msemaji wa Jeshi la Magereza, Amina Kavilondo, alisema Magereza hawana mamlaka ya kuwaachia mahabusi bila ya hati ya mahakama (remove order) ili kuwaruhusu watoke.

"Sisi kweli hatuna mamlaka ya kuwaachia mahabusi tunasubiri order kutoka sehemu husika ikifika sie hatuna tatizo lolote,"alisema Kavilondo.

Alifafanua kuwa Magereza hawana tatizo la kuwaachia huru mahabusi, lakini mpaka wapewe ruhusa toka mahakamani au sehemu husika ambayo iliwapeleka gerezani kwa mujibu wa sheria.

Alisema mahabusi waliopo wote ni kwa mujibu wa sheria na waliletwa gerezani kwa hati maalumu na kutoka kwao kunatakiwa hati ya mahakama.

Alisema magereza zipo kwa ajili ya kuwahifadhi mahabusi na waliopo wako kwa ajili ya amri maalumu, wakipewa agizo watatekeleza.

"Hili naliomba watu walielewe, kila mahabusi anayeingia Magereza lazima awe na hati ya Magereza, haiwezi kupokea mahabusi bila ya kuwa na hati kutoka mahakamani au Polisi,"alisema Kavilondo.

Hivi karibuni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Mhandisi Hamad Masauni, alitoa agizo kuwa mahabusi wote waachiwe huru ambao wana makosa yasiyotaka mtu kuwekwa ndani ili kuepuka msongamano kwa ajili ya ugonjwa wa corona.

Katika ziara hiyo pia alisema hakuna sababu ya kumuweka mtu ndani kwa kosa dogo, huku akitolea mfano wa mahabusi mmoja ambaye alipita bungeni na kukamatwa na kukaa ndani kwa muda wa siku tatu wakati kesi yake haikuwa ya msingi kulingana na adhabu waliokuwa wakimpatia.

# Jafo: Haya ndiyo yamefanyika Tamisemi miaka minne ya JPM

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, ametaja mafanikio ambayo wizara yake imeyapata katika miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha, Jafo alisema mafanikio hayo yameonekana katika miradi iliyotekelezwa kwenye sekta za afya, elimu, ujenzi wa majengo ya utawala, miundombinu ya barabara na kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara nchini.

Alisema katika kipindi hicho cha miaka minne, Ofisi ya Rais - Tamisemi imesimamia ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 98, vituo vya afya 433 na zahanati 368 na kwamba upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umekuwa wa uhakika kwa asilimia 92.

Jafo pia alisema katika kipindi hicho cha kuanzia Desemba 2015 hadi Februari mwaka huu, serikali imetumia Sh. trilioni 1.01 kugharamia Mpango wa Elimumsingi Bila Ada, maarufu elimu bure.

Kwa upande wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari, Jafo alisema serikali imejenga na kukamilisha vyumba vya madarasa 19,808 na vyumba 1,313 vipo katika hatua za ukamilishaji, maabara za masomo ya sayansi 227 zimejengwa na shule za sekondari 1,258 zimepatiwa vifaa vya maabara, matundu ya vyoo 7,922 yamejengwa na kukamilika na matundu ya vyoo 571 yanaendelea kukamilishwa.

Alisema madawati 5,070,896 yametengenezwa na shule kongwe za sekondari 73 zimekarabatiwa, huku Tamisemi ikisimamia ukarabati na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 74,940.06 ambapo kati ya hizo kilometa 485 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

"Jumla ya madaraja 232 na makalavati 7,168 yamejengwa na kukamilika. Serikali imejenga majengo ya utawala 86 ya Ofisi za wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi wa halmashauri. Kati yake, majengo 29 yamekamilika na 57 yapo katika hatua za ukamilishaji," alisema.

Jafo alisema katika kipindi cha miaka minne, jumla ya ajira za kudumu na za muda 2,347,334 zimezalishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa.

Alibainisha kuwa katika mwaka huu wa fedha, watumishi 7,280 wameajiriwa katika ajira za kudumu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwamo walimu wa shule za msingi na sekondari 4,945, watumishi wa kada za afya 765 na watendaji wa kata 1,570.

Alisema ajira hizo zinafanya watumishi walioajiriwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia 28,673 katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 wakiwamo walimu 18,181, watumishi wa afya 8,922 na watendaji wa kata 1,570.

Alisema katika mwaka ujao wa fedha, Ofisi ya Rais-Tamisemi imepanga kutekeleza kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D) na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alisema ofisi yake pia itaratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu ya msingi na sekondari katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa mpango wa utoaji

Alisema wizara yake pia itaratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, elimu inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya mikoa, wilaya na halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala zikiwamo halmashauri 30 ambazo zimeelekezwa na serikali kuhamia katika maeneo yao ya utawala.

Vilevile, waziri huyo alisema Ofisi ya Rais - Tamisemi imetengewa jumla ya Sh. bilioni 61.76 kwa ajili ya kulipa kiinua mgongo cha madiwani watakapomaliza muda wao wa uongozi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Pia, alisema Ofisi ya Rais - Tamisemi itahuisha Kanuni na Sheria Ndogo ili ziendane na mahitaji ya uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka ujao wa fedha, Jafo aliliomba Bunge kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya jumla ya Sh. trilioni 7.019. Kati yake, Sh. trilioni 4.729 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayojumuisha mishahara Sh. trilioni 3.878 na Sh. bilioni 851.142 kwa ajili ya matumizi mengineyo huku Sh. trilioni 2.289 zikiombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Katika mwaka huu wa fedha, wizara hiyo iliidhinishwa na Bunge matumizi ya Sh. trilioni 6.2. Kati yake, Sh. trilioni 3.81 ni kwa ajili ya mishahara, Sh. bilioni 707.95 ni matumizi mengineyo na Sh. trilioni 1.69 ni za miradi ya maendeleo.


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## AUDITED RESULTS
### FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2019

**CHAIRMAN'S STATEMENT**
Despite strong competition in the cement manufacturing industry, Tanzania Portland Cement Public Limited Company (TPC PLC) delivered a record performance compared to the year 2018 both in terms of revenue and volume growth. Revenue and sales volume increased by 6% and operating profit increased by 9%. This growth demonstrates TPC PLC strength and market leadership in the industry.

Efforts were made to increase the production of clinker combined with the overall machine availability, good customer service, selling of high quality products and maintaining strong customer relationship ensured the improved performance and results for the year.

| INCOME STATEMENT | 2019 TZS'000 | 2018 TZS'000 |
|---|---|---|
| Revenue | 348,828,076 | 328,499,013 |
| Cost of sales | (215,395,398) | (203,559,476) |
| **Gross profit** | **133,432,678** | **124,939,537** |
| Other operating income | 4,293,998 | 4,442,850 |
| Selling and administrative expenses | (2,746,244) | (2,517,845) |
| Administrative expenses | (22,930,877) | (24,703,567) |
| Depreciation and amortisation | (18,257,703) | (17,806,015) |
| Other operating expenses | (6,536,148) | (4,293,923) |
| **Operating profit** | **87,255,704** | **80,061,037** |
| Financial items | (1,380,718) | 1,683,745 |
| **Profit before tax** | **85,874,986** | **81,744,782** |
| Taxes on income | (26,171,702) | (24,878,687) |
| **Profit for the year** | **59,703,284** | **56,866,095** |
| Other comprehensive income , net of tax | (988,050) | (403,822) |
| **Total Comprehensive Income** | **58,715,234** | **56,462,273** |

| BALANCE SHEET | 2019 TZS'000 | 2018 TZS'000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| Intangible fixed assets | 849,314 | 1,304,535 |
| Tangible fixed assets | 137,094,378 | 140,948,038 |
| Right of use assets | 7,430,771 | - |
| Non-current financial assets | 5,905,187 | 7,513,661 |
| **Non.current assets** | **151,279,650** | **149,766,234** |
| Inventories | 61,598,827 | 55,104,226 |
| Trade and other receivables | 52,006,440 | 44,712,022 |
| Other current financial assets | 4,721,453 | 7,191,052 |
| Cash and cash equivalents | 72,684,693 | 65,987,258 |
| **Current assets** | **191,011,413** | **172,994,558** |
| **TOTAL ASSETS** | **342,291,064** | **322,760,792** |
| **EQUITY & LIABILITIES** | | |
| **Equity** | **231,473,287** | **224,935,758** |
| Lease liabilities | 3,097,244 | - |
| Long term provisions | 7,620,008 | 8,205,223 |
| Provision for deferred taxes | 17,573,518 | 21,035,003 |
| **Non-current liabilities** | **28,290,770** | **29,240,226** |
| Lease liabilities | 4,974,507 | - |
| Current income tax payable | 1,027,428 | 3,575,758 |
| Trade and other payables | 73,307,570 | 61,158,088 |
| Dividend payable | 3,217,502 | 3,850,962 |
| **Current liabilities** | **82,527,007** | **68,584,808** |
| **TOTAL EQUITY & LIABILITIES** | **342,291,064** | **322,760,792** |

**Prospects**
The cement demand in Tanzania and in the East-African region has been growing steadily in recent years. TPC PLC is well placed to meet this growing demand and will continue to work to maintain its market leadership and position.

**Dividend**
The Board proposes a dividend for year 2019 of TZS 290 per share, same as the rate declared in 2018.

The Register of Members will close on 6 May 2020, and the last day of trading cum dividend will be 30 April 2020. The dividend will be paid on or about 30 June 2020.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support during the past year. We have every confidence that TPC PLC will continue to deliver value for the shareholders in the future.

BY ORDER OF THE BOARD

Alfonso Velez on behalf of Hakan Gurdal
Chairman of the Board
08.04.2020

**Tanzania Portland Cement Public Limited Company**
**P.O.Box 1950**
**Dar-es-salaam**
**Tanzania**
**www.twigacement.com**
**Email: info@twigacement.com**

# RC awaasa waganga tiba asili corona

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, amewaagiza machifu na waganga wa tiba asili katika mkoa huo, kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.

Amewataka kuhakikisha wanakuwa na ndoo za maji yanayotitirika na sabuni katika maeneo yao ya kazi ili kuwahamasisha na kuwaelimisha wateja wao wanaowapa huduma kuelewa umuhimu wa kunawa mikono ili kujikinga na ugonjwa huo.

Aliongeza kuwa, haitakuwa na maana kama wamepata elimu halafu hawaitumii hali ambayo hakutakuwa na wa kumlaumu endapo ugonjwa huo utasambaa na kuangamiza watu, alisisitiza kuwa, kutowaelimisha wateja wao na kushindwa kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo ni sawa na kulisaliti taifa wakati serikali inaendelea kutimiza wajibu wake wa kutoa elimu ya ugonjwa huo kwa kutumia njia mbalimbali.

"Kwa upande wa maji mimi kwangu ni agizo, machifu wote muwe na ndoo ya maji tiririka na sabuni, muonyeshe mfano, waganga wa tiba za asili, na nyinyi wote kwa umoja wenu mkawe na ndoo za maji tiririka na sabuni na elimu mmeipata vizuri," alisema.

"Haitakuwa na maana kama mmepata elimu halafu kule mnakokwenda hamuitumii, halafu ugonjwa unakuja unatuangamiza, utamlaumu nani na elimu tumekupa, itabidi ujute kwamba wewe ni msaliti, umelisaliti taifa, umemsaliti na Mungu pia," alisema.

Wangabo alitoa maagizo hayo kwa nafasi yake kuwa kiongozi wa machifu mkoani Rukwa, katika kikao kilichofanyika kutoa elimu ya ugonjwa wa corona kwa machifu pamoja na viongozi wa waganga wa tiba asili wakiwamo wa Chama cha Waganga/ Wakunga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala Mkoani Rukwa (CHAWATIRU).

Aidha, Wangabo aliwataka machifu hao kukemea mila zinazowezesha kusambaa kwa ugonjwa wa corona kwa haraka, ikiwamo watu zaidi ya mmoja kutumia chombo kimoja kunywa pombe za asili, familia kutumia chombo kimoja kutumbukiza mikono kwaajili ya kunawa, pamoja kutumia chombo kimoja cha kuchotea na kunywea maji katika mtungi.

Kadhalika, aliwataka waganga wa tiba asili kuwa na utaratibu wa kulipwa kwa kutumia huduma za mitandao ya simu ama benki ili kuepuka kushika fedha za wagonjwa ambao hawajulikani ugonjwa wao, huku akisisitiza kutotowa dawa zinazopelekea mtu kupiga chafya mara kwa mara.

Kaimu mganga Mkuu wa mkoa wa Rukwa, Dk. Emanuel Mtika, aliwatahadharisha kuwa kuwatibu wagonjwa wa corona ni gharama kubwa sana kiasi ambacho endapo ugonjwa huo utasambaa, watu wengi wanaweza kupotea kwa kushindwa kufuata maelekezo ya wataalamu juu ya kujikinga na ugonjwa huo.



Lundo la takataka zilizoletwa na mafuriko ya mvua katika daraja la Mto Ng'ombe, linalounganisha eneo la Kijitonyama Ali Maua na Tandale kwa Mtogole, jijini Dar es Salaam, zikiwa zimetelekezwa kwa muda mrefu bila ya kuondolewa. **PICHA: JOHN BADI**

# Walioshambulia polisi, wapima ardhi wasakwa

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Msafiri Mtemi, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoa wa kipolisi Tarime/Rorya, kuwasaka na kuwafikisha mahakamani watu wanaodaiwa kushambulia askari polisi na watumishi wa halmashauri ya wilaya, wakati wakipima mipaka ya utawala.

Kundi la watu lililokuwa na silaha za jadi, liliwashambulia na kuwajeruhi maofisa wapima ardhi, Joseph Mulazi na Sylivatus Mafuru, wakati wakitekeleza majukumu yao ya upimaji wa mipaka ya utawala inayotenganisha vijiji vya Murito na Gibaso.

Mtemi alisema, tayari kamati ya usalama inafanya ziara katika maeneo hayo ambayo mfaka ya nyuma ilikabiliwa na vita baina ya koo mbili za Wairegi na Wanyamongo, iliyosababisha mali ya mamilioni ya fedha kuteketea na wanakijiji kadhaa kujeruhiwa.

Alisema serikali wilayani hapo haitavumilia vitendo vyoyote vya uchochezi vya kuvuruga amani na utengamano wa kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli zao za kila siku za kujipatia kipato.

Alionya kwamba katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu, uchunguzi wa vyombo vya usalama umebaini baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakitoa kauli za kuwaongezea mipaka ya kiutawala wananchi ikiwa watachaguliwa kinyume na utaratibu wa kisheria.

"Serikali itawachukulia hatua washukiwa wote wa uhalifu ukiwamo uchochezi bila kujali nafasi zao za kisiasa kwa kuwa matendo kama haya yalisababisha uvunjifu wa amani na upotevu wa mali na maisha bila sababu yoyote siku za nyuma," alisema.

Kwa mujibu wa diwani wa eneo hilo, Rashid Bogomba, ukosefu wa amani katika eneo hilo lililo karibu na mgodi wa kimataifa wa North Mara, unaomilikiwa na Barrick, umesababisha kukatisha tamaa wawekezaji wa ndani.

Serikali wilayani Tarime iliratibu mpango kazi wa miaka mitano iliyopita ikiwa ni pamoja na kuwezesha wawekezaji wa ndani ikiwamo shamba kubwa la zaidi ya ekari 500 linalomilikiwa na kampuni ya wazawa ya Isaack and sons kufunguliwa eneo hilo na kuwezesha kutenganisha uhasama wa kila mara baina ya koo hizo.

Mwenyekiti wa kijiji cha Murito, Jacob Irondo, alisema uanzishwaji wa shamba hilo umewezesha ajira kwa vijana zaidi ya 200 kujipatia kipato na kuboresha maisha badala ya kutumia muda mwingi katika makabiliano ya koo wakigombea mipaka.

Alisema kupitia kamati za usalama za vijiji vyote jirani vimeazimia kubaini wahusika wa uchochezi na kukabidhi majina yao katika vyombo

# Hasunga ammiminia sifa Pinda kwa kilimo

**Na Mathias Canal,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amemtembelea Waziri Mkuu mstaafu ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mizengo Pinda, nyumbani kwake eneo la Zuzu jijini Dodoma.

Katika ziara hiyo Waziri Hasunga alimpongeza Pinda kwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika sekta ya kilimo hususani katika kilimo cha mboga na matunda kupitia kitalu nyumba (Green Houses), huku akisisitiza umuhimu wa uwekezaji huo kwa wakulima wa maeneo jirani kujifunza mbinu bora za kilimo kupitia yeye.

Pamoja na kutembelea ujenzi wa vitalu nyumba, kadhalika Waziri Hasunga alijionea uwekezaji mkubwa wa ufugaji wa kisasa wa samaki.

Akizungumza shambani hapo juzi, Pinda alipongeza juhudi za Wizara ya Kilimo kuanzisha mchakato wa kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo, itakayotoa suluhisho la changamoto zinazomkabili Mkulima na Sekta hiyo kwa ujumla itakayopelekea kuunganisha Bodi za mazao ili kuwa na mamlaka za mazao.

Kadhalika, Pinda alisema kuwa kuna ulazima wa kuendelea kusimamia kwa weledi sekta ya Ushirika nchini, kwani huo ndio umoja pekee unaowaunganisha wakulima na kuwa na nguvu ya pamoja hususani katika kupanga bei ya mazao yao kadhalika kuimarisha masoko ya mazao.

Kuhusu sekta ya umwagiliaji, Pinda alisema kuwa serikali inapaswa kuendelea kutilia mkazo zaidi kwani ndio njia pekee itakayomnusuru mkulima katika sekta hiyo ili kuondokana na kutegemea kilimo cha msimu wa mvua pekee.

# Sheria ya upandikizaji viungo vya binadamu yakaribia

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho za kuandaa Muswada wa sheria ya uvunaji, utunzaji, usafirishaji na upandikizaji wa viungo vya binadamu.

Viungo hivyo ni pamoja na figo, moyo, maini, mapafu, sclera ya macho, uroto, na vingine na utaweka utaratibu mzuri wa namna ya kufanya kazi hiyo.

Hayo yalielezwa bungeni jana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika majibu yake kwenye swali la Mbunge wa Viti Maaalum (CCM), Rose Tweve (pichani chini).

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema Serikali imekuwa ikihimiza wananchi kuchangia damu na kuihifadhi katika benki za damu kwa ajili ya Watu wenye uhitaji.

"Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha utaratibu maalum wa kuvuna viungo kama vile figo na moyo kutoka kwa watu waliopata ajali na wapo kwenye hali ya kupoteza maisha au kutoka kwa watu walioridhia kutolewa viungo hivyo na kuvihifadhi kwa ajili ya Watanzania wenye uhitaji wa viungo hivyo?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema kuwa Sheria itaelekeza vitu vya kuzingatia kwa mpokeaji na mtoaji wa viungo.

"Sheria hii itaweka utaratibu kwa watu wanaoridhia kutolewa viungo vyao pindi wanapokaribia kupoteza maisha ikiwa mchangiaji huyo atakuwa ameridhia viungo vyake vitumike kwa ajili ya jamii inayohitaji viungo hivyo pindi akipoteza maisha,"ilisema.

Ilifafanua kuwa nchi inaheshimu haki za binadamu ikiwamo haki ya kuishi, mtu kupata ajali na kutolewa viungo vyake litafanywa pale ambapo mhusika atakuwa ameridhia akipata ajali na akawa hana uwezo wa kupona atolewe viungo.

Wizara hiyo iliongeza kuwa hatua za kisheria na kitabibu zitatumika ili kutoa viungo hivyo na kuvihifadhi kwa ajili ya matumizi ya mtu atakayehitaji.



# Wazee 349 wahudumiwa kwenye makazi 13 nchini

BUNGE limeelezwa kuwa, hadi kufikia Machi, 2020, kuna wazee wasiojiweza 349 wanahudumiwa na Serikali kwenye makazi 13 ya wazee nchini.

Wazee hao ni wale ambao hawana watoto, ndugu wala jamii ya karibu ya kuwahudumia.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwenye majibu ya swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Joyce Sokombi (pichani).



Mbunge huyo alisema kumekuwa na wimbi kubwa la wazee wanaoishi katika mtaa ambao wanaishi katika mazingira magumu.

"Je, Serikali inajipanga vipi kuweza kusaidia wasiendelee kuteseka?" alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na Wizara hiyo, ilisema kati ya wazee hao 349, wanawake 149 na wanaume 200, na mpaka sasa hakuna tathmini rasmi kitaifa iliyofanyika kuwatambua wazee wanaoishi mitaani.

"Kwa kuwa miongoni mwao hutokea katika familia na jamii zao kuja mitaani kuomba mchana na kurudi makwao jioni au kulala pembezoni mwa maduka na katika masoko," ilisema.

Aidha, ilitumia fursa hiyo kutoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kuwatambua wazee na kuwaunganisha na huduma za msingi, pia familia na jamii kutekeleza wajibu wao wa kutoa matunzo kwa wazee hususan wale wasiojiweza.

"Serikali imeendelea kuweka mikakati madhubuti kuhakikisha kuwa wazee wote nchini wanafurahia maisha ya uzee hasa tukizingatia kuwa wazee ni hazina ya Taifa," ilisema.

Ilieleza kuwa katika kuhakikisha kuwa haki, ustawi, ulinzi na usalama wa wazee unaimarishwa, Serikali kupitia mamlaka za Serikali za Mitaa imekuwa ikifanya utambuzi na uandikishaji endelevu wa wazee wasiokuwa na uwezo wa kujimudu kimaisha katika jamii.

Iliongeza kuwa mamlaka hizo zilielekezwa ziwapatie huduma za msingi za ustawi ikiwamo vitambulisho vya matibabu bila malipo, malazi katika makazi ya wazee wasiojiweza, pamoja na msaada wa kisaikolojia.

# Serikali yaipa IFM jukumu la uwekezaji viwanda vya pamba

WIZARA ya Kilimo imekipatia Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kazi ya kuandaa taarifa ya kina ya uwekezaji katika viwanda vya zao la pamba ili kukuza soko lake.

Aidha, imesema taarifa hiyo itatoa dira ya namna ya kuanzisha viwanda vikiwamo vya kusindika pamba na inatarajiwa kukamilika kabla ya Julai, 2020.

Wizara hiyo ilitoa kauli hiyo bungeni wakati ikijibu swali la Mbunge wa Busega (CCM), Dk. Raphael Chegeni.

Katika swali lake, Chegeni alisema zao la pamba linakabiliwa na kero nyingi kutokana na kukosekana uhakika wa bei yake.

"Je, Serikali inawaambia nini wakulima wa pamba?," alihoji.

Kwa mujibu wa majibu ya Wizara hiyo, lengo la kazi hiyo ni kukuza soko la pamba na taarifa hiyo itatoa dira ya namna ya kuanzisha viwanda hivyo.

Wizara hiyo ilisema inaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuimarisha huduma za ugani na upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji kwa kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza kipato kwa wakulima.

Ilisema serikali inatambua tatizo la kuyumba kwa bei ya pamba katika soko la kimataifa.

Aidha, kufuatia tatizo hilo, ilisema serikali iliingilia kati ununuzi wa Pamba katika msimu wa ununuzi wa 2019/20 ili kuhakikisha mkulima anapata bei yenye tija.




Ilifafanua kuwa, suluhisho la kudumu kuhusu bei ya pamba ni kuongeza kiasi cha pamba inayochakatwa ndani ya nchi ili kuzalisha bidhaa zitakazotumika hapa nchini na hivyo kupunguza utegemezi wa soko la nje.

Ilieleza kuwa, ili kutekeleza Mpango huo, Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na wa nje kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya zao la Pamba kwa kufuta tozo na kodi mbalimbali.

"Pia kuzalisha umeme wa uhakika na bei nafuu, kuendelea kuongeza mitaji katika Taasisi za kifedha na maendeleo kama vile Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Benki ya Rasilimali ili kutoa mkopo ya muda mrefu na kati kwa Viwanda ili kuongeza soko," taarifa hiyo ilieleza.

Pia, ilisema kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuongeza tija na uzalishaji ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza bei na kipato kwa wakulima wa pamba.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA

# Askofu aomba waumini kutii maelezo ya watalaamu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isaac Amani, amewaomba waumini kutii na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona (Covid -19).

Akizungumza jana na Nipashe jijini hapa, Askofu Amani alisema, ni vyema kila mmoja akazingatia ushauri na maelekezo yanayotolewa na viongozi wa serikali na wataalamu wa afya, kujikinga bila kupuuza.

"Kupitia ugonjwa huu tunaona ndoa zimeimarika, maana wanaume wanatulia nyumbani na familia zao kusali pamoja, katika hili inatufundisha kumrudia Mungu na kujitafakari, japo tumerudishwa kwa njia ngumu ya corona," alisema.

Alisema katika kipindi hiki ambacho uhai umetikishwa na corona, kila mmoja atumie nafasi yake kuliombea taifa na dunia nzima.

Alihimiza watu kupendana, kutambuana na kuwa wamoja bila kujali vyeo walivyo navyo, huku wakitanguliza uzalendo ili kupigana pamoja kwenye vita dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema kila mmoja anapaswa kusafisha roho yake kama wanavyosafisha mikono kwa ajili ya kujikinga na corona ili taifa liwe imara zaidi.

Askofu Amani alisema kwa sasa taifa lipo kimya kwa sababu ya ugonjwa huo, hivyo aliwakumbusha waumini kutumia muda huo kuomba ili ugonjwa huo utoweke.

"Ugonjwa huu umetoa fundisho kuwa, pamoja tunaweka mageti na uzio wa nyumba zetu wa kila aina, kwa ajili ya usalama wetu, lakini mdudu corona anatuchukua, hii maana yake tunapaswa kujinyenyekeza kwa Mungu na kupitia hili nimeona watu wanasali sana na tuendelee kuomba tuondokane na ugonjwa huu," alisisitiza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, mkoani Arusha, Emmanuel Mkongo (kulia), akizungumza kuhusu masuala mbalimbali, likiwamo la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona katika kikao cha baraza la madiwani wa Halmashauri hiyo, juzi. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# Serikali yaombwa kusaidia wakulima kukopesheka

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA.

SERIKALI na Taasisi za fedha zimeombwa kushirikiana kutengeneza mazingira rafiki yatakayowezesha wakulima kukopesheka kwa urahisi, kwa kuweka dhamana mashamba yao, ili kuboresha kilimo chao.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Huduma katika Kijiji cha Kilimatembo, Kata ya Rhotia wilayani Karatu, Fabiano Petro, wakati akizungumza na wakulima kijijini hapo alipotembelea shamba darasa na kujifunza mbinu bora za kilimo na changamoto zinazowakabili.

Petro alisema wakulima wengi hususani walioko vijijini wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha, kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo hali inayosababisha kuendelea kulima kimazoea.

"Sasa hivi gharama za pembejeo za kilimo zipo juu sana, hali inayosababisha wakulima kushindwa kulima kisasa na kuishia kilimo cha mazoea ambacho mwisho wa siku wanaishia kupata hasara na kutokuwa na ari ya kupenda kilimo," alisema.

Meneja masoko wa kampuni ya kizalendo ya usambazaji na uzalishaji wa mbegu za mahindi katika kampuni ya IFFA, Luhenda Yangole, aliwataka wakulima kuyatumia mashamba darasa yaliyoandaliwa kama mfano, kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima, ili walime kilimo cha kibiashara na kuondokana na kilimo cha mazoea cha kuishia kuhudumia kaya zao.

Yangole alisema, changamoto kubwa iliyopo kwa wakulima wengi ni kutofanya kilimo kama biashara kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha ya mbegu bora za kisasa na matumizi bora ya zana za kilimo.

"Wakulima wengi wanalalamikia changamoto ya ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua pembejeo, katika hili sisi tupo tayari kuwakopesha pembejeo kupitia vyama vyao vya ushirika na mtapatiwa kwa bei rahisi kwa kuwa watachukua moja kwa moja kwenye kampuni yetu na kwa kufanya hivyo kunawahakikishia usalama wa mbegu zetu pia," alisema Yangole.

Kwa upande wa Ofisa mazao wa Wilaya ya Karatu,Twilumba Ngwale, aliwataka wakulima hao kubadilika na kutumia kanuni bora za kilimo, kama wanavyoelekezwa na wataalamu mbalimbali na kutumia mashamba darasa kujifunza na kujua mbegu bora za kilimo zinazowafaa kwenye maeneo yao.

Mmoja wa wakulima katika Kijiji cha Kilimatembo, Jackson Musa, aliomba kampuni hizo za mbegu, kuendelea kuwatembelea wakulima vijijini na kutoa elimu ya matumizi bora ya mbegu za kutumia, ili walime kilimo chenye tija na kuondokana na mazoea.

## Wajasiliamali washauriwa kuboresha vifungashio

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI wadogo na wa kati nchini, wameshauriwa kuboresha vifungashio vya bidhaa zao wanazozalisha, ili kuvutia soko la ndani na nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana jijini hapa na Meneja wa Shirika la kuhudumia Viwanda vidogo nchini (Sido), mkoani hapa, Nina Nchimbi, wakati akizungumza na wajasiriamali wa kutengeneza sabuni za maji na kipande, dawa za kuua wadudu chooni na dawa za kusafisha vigae.

Nchimbi alisema, wajasiriamali wanapaswa kuwa wabunifu kila wanapozalisha bidhaa zao, ili kuongeza ubora katika biashara zao na kuwavutia wateja zaidi kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema wengi wao wanajitahidi kuzalisha, lakini changamoto kubwa ni katika uboreshaji wa vifungashio na kuwataka kuwa wabunifu zaidi, ili kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi pia.

"Unapozalisha bidhaa yako kila wakati inakuwa na muonekano ule ule, inakuwa ngumu kupata wateja wapya, ni lazima mbadili muonekano wa vifungashio hivyo, viwe vya tofauti na zivutie wateja na kwa kufanya hivyo, mtapata soko la uhakika," alisema Nchimbi.

Naye Mkufunzi wa mafunzo hayo, yaliyotolewa na Sido, Bahati Mkopi, alisema, mafunzo hayo ya utengenezaji sabuni ni awamu ya nne sasa, zaidi ya wajasiriamali 80 wamehitimu mafunzo hayo na kuleta manufaa makubwa, ikiwamo kuanzisha viwanda vidogo na vya kati zaidi ya 10.

Alisema mafunzo hayo yamewasaidia vijana kujiajiri na kupata uhakika wa kipato, kwa kujishughulisha wenyewe. Akisoma risala yake, mmoja wa wajasiriamali, Mboka Mwakalinga, alisema kupitia mafunzo hayo wamepata utambuzi wa kitaaluma wa vyeti ambavyo vitawawezesha katika mambo ya usajili na kuanzisha viwanda vidogo.

Alisema wanakabiliwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa vifungashio, uhaba wa baadhi ya malighafi na gharama kubwa ya malighafi hizo, hivyo waliomba serikali kupitia Sido na wadau wengine wajengewe mazingira mazuri, kwa ajili ya wawekezaji wa malighafi na vifungashio, ili wapate kwa urahisi.

## Walioteleleza majengo kupokwa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

WAKAZI wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Hai mkoani Kilimanjaro, waliokwama kumalizia ujenzi wa nyumba za makazi na biashara kisha kutelekeza majengo hayo kwa muda mrefu, wapo hatarini kupokwa maeneo hayo na serikali.

Kauli hiyo ya kuwataka waliojenga majengo hayo na kuyaacha kubaki kama magofu, kumalizia ujenzi wake ili kuepuka mkono wa dola, ilitolewa jana na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hiyo, Noel Nnko.

"Niwatake wote waliocha majengo yao kama magofu kwa muda mrefu wayamalizie haraka. Sheria inataka kufanya hivyo, wanaodhani ni utani wasubiri hatua zitakapochukuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Hai," alisema Nnko.

Kwa mujibu wa Mtendaji huyo, katika mji huo, kuna nyumba zimejengwa zaidi ya miaka 20 bila kumalizika ujenzi wake na kuwa maficho ya wahalifu.

Nnko alisema Sheria ya Ardhi na Makazi, Namba 4 ya Mwaka 1994 inawapa mamlaka ya kutaifisha nyumba ambazo hazijaendelezwa kwa muda mrefu.

"Tumewaomba mwenyeviti wa vitongoji na mitaa watusaidie kuweka mabango ya matangazo katika nyumba hizo na ikiwezekana wapewe notisi kupitia ofisi za kata, angalau siku 12 waweke madirisha na milango.

Zaidi alisisitiza: "Tayari agizo la kutaka majengo hayo kufanyiwa usafi limeshatolewa, kama watashindwa kuyafanyia usafi tutayataifisha haya majengo, hatuwezi kuendelea kuangalia majengo hayo."

Aidha, alisema mamlaka hiyo imejipanga kutekeleza mkakati huo na kwamba hawawezi kukaa na majengo katikati ya mjini, halafu hayajaendelezwa.

# Hai yachukua hatua zaidi kukabili tishio la corona

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, imechukua hatua zaidi katika kukabiliana na kasi ya maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu.

Hatua hizo ni kuelekeza fedha za umma kununua matanki ya maji na vitakasa mikono katika masoko ya kwa Sadala na Bomang'ombe.

Masoko hayo likiwamo soko la mazao la kimataifa la kwa Sadala, linalobeba idadi kubwa ya wafanyabiashara kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yohana Sintoo, alitangaza uamuzi wa kuongeza umakini zaidi kwenye masoko hayo kuhofia kujitokeza maambukizi kutokana na mwingiliano mkubwa wa watu.

"Kimsingi tumeongeza umakini katika maeneo hatarishi hasa masoko. Tumepanga kufanya zoezi la uwekaji wa matenki ya kunawa mikono," alisema na kuendelea: "Wakati wa kuingia na kutoka katika soko la kwa sadala ambalo linaingiza wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya mkoa wa Kilimanjaro, hivyo kusababisha mkusanyiko mkubwa."

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya Corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov corona virus mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Dalili za ugonjwa huo, huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.



Mkuu wa mkoa wa Mara, Adam Malima (mwenye balaghashia), akijadiliana jambo na Mkuu wa wilaya ya Musoma, Dk. Vicent Anano (kulia) na Mratibu wa shughuli za Shirika la Msalaba Mwekundu mkoani humo, Sarah Waryoba, baada ya uzinduzi wa kampeni ya kutoa elimu kwa Wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona katika soko la Saanane, Kata ya Nyakato, Manispaa ya Musoma, jana. **PICHA: ROBINSON WANGASO**

# Same wapata ukombozi huduma afya

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAKAZI zaidi 1,200 wanaoishi katika Kata ya Mtii, Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, ambao walikuwa wakitegemea huduma za afya kwenye kata ya jirani, hatimaye wameanza kunufaika na huduma hiyo baada ya serikali kukamilisha taratibu zote.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, alisema zahanati hiyo iliyojengwa kwa nguvu za wananchi ilianza rasmi kutumika siku chache zilizopita.

"Ingawa bado hatujafanya ufunguzi rasmi wa kiserikali, lakini tumeruhusu huduma zianze ili wananchi wasiendelee kuteseka kufuata huduma za afya mbali na makazi yao," alisema Senyamule.

Kwa sasa zahanati hiyo inatoa huduma za dharura za tiba kwa saa 24, baada ya kukamilika jengo la wagonjwa wa nje (OPD).

Mbali na nguvu za wananchi, jengo hilo lilipata ufadhili wa fedha Sh.milioni 25 kutoka Benki ya Posta Tanzania. Rahel Mbaga na Emmanuel Mghamba, wakieleza kufurahishwa kwao na huduma hiyo, wameeleza kuwa wananchi walipata wazo hilo baada ya kuibuka changamoto za baadhi yao kukosa tiba nyakati za usiku pale wanapouguliwa ama wajawazito kushikwa na uchungu.

Kwa mujibu wa Mbaga, baada ya kusoma muongozo wa sera ya afya na kubaini kuwa zahanati haziruhusiwi kulaza wagonjwa, walihamasishana kila kaya kuchangia fedh ambazo zitajenga jengo hilo.

Meneja wa Benki ya TPB, Kanda ya Kaskazini, Ayub Mkwawa, alisema waliguswa kusaidia juhudi hizo za wananchi hasa kutokana na umuhimu wa huduma za afya vijijini.

# ama

ALHAMISI APRILI 9, 2020

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Klorokwini kutajwa tiba corona, kizaazaa kizito matumizi yake**



Ukurasa 16

Ruwasa katika ushindi unaomtua ndoo mwanamke wa Shinyanga



Ukurasa 17

**Corona yaleta mapya ndani ya uzazi mpya**



# Makali ya kuugua yanaendana na kiasi virusi vilivyomo mwilini

Ukurasa 18



Dk. Amir Khan. **PICHA: MTANDAO.**

## Utata maambukizi corona mjamzito kwa mtoto

**Mwandishi Wetu**

KUNA maswali ambayo yameibuliwa, kuhusu namna ambavyo virusi vya corona vinaweza kupita kutoka kwa mama mjamzito, hadi kwa mtoto tumboni mwake.

Tabibu bingwa wa binadamu, ambaye pia ni Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu nchini Uingereza, Dk Amir Khan, ameifuatilia na kuibua majibu ya awali, kwamba hadi sasa hakuna jibu la moja kwa moja.

Anasema, katika uhalisia uliozeleka kitaalamu, kuna aina ya virusi na bakteria vinavyovuka kutoka kwa mama, hadi kwa mtoto na wengine hawavuki.

Dk. Amir anatoa mfano, virusi vinavyopenya kwa mtoto ni pamoja na HIV, tetekuwanga na rubella (surua ya siki tatu), lakini kwa corona, Dk. Amir anasema bado hakujawaapo ushahidi wa kisayansi kulithibitisha hilo.

Kwa mujibu wa chapisho la kisayansi kutoka jarida huru la Lancet la nchini China, ambako ndiko kwenye mzizi wa corona, hakuna mtoto aliyezaliwa akiwa na virusi hivyo.

Pia, utata wa ushahidi huo unaenda mbali, kwamba hata unyevu unaomzunguka mtoto tumboni, hadi sasa haku ushahidi wa kisayansi kutetea kumuambukiza mtoto aliye tumboni au la. Ni aina hiyo ya utata, kwamba haujafanyika utafiti kamili kujua kama mgonjwa corona na nafasi ya kumwabukiza mtoto wake kwa njia ya kumnyonyesha.

AFYA

# Klorokwini kutajwa tiba corona, kizaazaa kizito matumizi yake

• WHO inasema feki, Trump aweka oda maalum India



Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

CORONA inazua lake na kila mmoja anaibua yake. Kumekuwapo wimbi la uhitaji wa dawa zinazotumika dhidi ya ugonjwa malaria, kwa madai vinaweza kukabili mapambano na virusi vya corona, wakati serikali mbalimbali duniani zikitafuta tiba.

Klorokwini na baadhi ya dawa zimekuwa zikitazamwa hasa pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), kama zinaweza kutibu, lakini hakuna ushahidi wa dawa hizo kunafanya kazi.

Ushahidi ulioko sasa kuhusu ufanisi wa tiba yake dhidi ya virusi vya corona ni kwamba vinaweza pia kuzuia virusi vinavyosababisha covid-19, lakini kuna ushahidi mdogo zaidi unaojitokeza kumnusuru mtumiaji na hatari kama vile kuharibika ini na figo.

Wastani wa wiki tatu zilizopita, iliripotiwa na shirika la habari la Kimarekani, kuwa Rais Donald Trump, alitangaza majaribio ya awali ya klorokiwini, iliyoonekana kuwa na uwezo kutibu virusi vya Corona na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya nchi hiyo ikaidhinisha.

> “Nchini Nigeria kumeshuhudiwa ongezeko la bei za dawa hiyo, bada aya kutangazwa sifa za kuweza kutibu.




Dawa aina ya klorokwini.

Hata hivyo, baada ya muda mfupi, mamlaka hiyo ilitoa taarifa nyingine kuhusu ufanisi tajwa kwamba unafanyiwa kazi kabla ya kuidhinishwa

Rais Trump mara kadhaa, amekuwa akieleza umuhimu wa dawa aina ya 'hydroxychloroquine' ambayo ndiyo jirani na chapa klorokwini ya malaria na kufanya uhitaji wake kuongezeka kama dawa muhimu ya kutibu virusi vya covid-19

Klorokwini imekuwa ikipatikana kwa kiasi kikubwa kwenye maduka ya dawa, hasa katika nchi zinazoendelea, kwa ajili ya kutibu malaria, lakini ghafla zimetoweka baada ya janga la corona kuibuka.

Ingawa dawa hizo hazikuwa na ufanisi dhidi ya malaria kutokana na ugonjwa kuzidi kuwa sugu, nchi kama Jordan imepiga maruku uuzwaji wa 'hydroxychloroquine' kwenye maduka ya dawa ili kukabili hali hiyo ya mlipuko wa matumizi yake.

Vivyo hivyo, Wizara ya Afya ya Kuwait, imeamua kuondoa dawa zote zenye aina hiyo kutoka kwenye maduka ya dawa binafsi na kudhibiti upatikanaji wake kwenye hospitali na vituo vya afya.

Kenya nayo imepiga marufuku uuzaji wa chhloroquine na kwa sasa inapatikana kwa ruhusa maalumu ya wataalamu wa afya, huku taifa la India ni taifa ambalo ni mzalishaji mkubwa wa dawa hizi, nayo imeweka marufuku kuzisafirisha nje dawa hizo.

Hata hivyo, Rais Trump, amemuelekezea ombi binafsi kiongozi mwenziwe, Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, apate dawa hizo kwa matumizi ya nchi yake na India imemjibu inatafakari ombi lake.

Taarifa ya utafiti wa mwezi Februari nchini China kuhusiana na matumizi ya klorkwini, kupambana na virusi vya corona, ilisababisha mjadala mkubwa jijini Lagos, Nigeria, hata kuwafanya watu kununua dawa hizo kwa wingi.

Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa Nchini Nigeria, kimewaambia watu kuacha kutumia dawa hiyo ambayo bado haijaidhinishwa na WHO, katika kudhibiti maradhi ya corona.'

Wastani wa wiki mbili na nusu zilizopita, maofisa katika jimbo la Lagos, walisema kumekuwapo watu kadhaa walioathiriwa na matumizi ya kuvuka kiwango kinachopaswa cha dawa za klorokwini, watatu wakilazwa baada ya kumeza vidonge vingi.

Nchini humo kumeshuhudiwa ongezeko la bei za dawa hiyo, bada aya kutangazwa sifa za kuweza kutibu.

Meneja wa Mradi wa Opereshenі wa WHO, Michel Yeo, anasema takribani kuna jumla ya dawa 20 ikiwemo klorokwini, zinazifanyiwa majaribio ya kitabibu dhidi ya corona.

AFYA

# Corona sasa kuamua hatima ya elimu, maisha mtaani duniani

- Kila mahali mshikemshike, hakushukiki
- Madaktari, wauguzi wastaafu maelfu waitwa

Na Maulid Mmbaga

UGONJWA wa homa kali ya mapafu unaosababishwa na virusi vya corona (Covid-19), umekuwa tishio duniani na hata kulazimisha shughuli mbalimbali za kijamii kusimama, ikiwamo lililo nyeti la utoaji wa elimu.

Katika kutekeleza jitihada za kupambana na kuenea ugonjwa huo, nchi nyingi duniani zilitangaza kusitisha utoaji elimu shuleni, katika vyuo na hadi vyuo vikuu kwa dhumuni la kuepusha misongamano, ambayo ni wakala mkuu wa kuenea ugonjwa.

Ni hekaheka ambayo Tanzania siyo kisiwa. Nayo imesitisha utoaji elimu katika mjumuiko. Tarehe 18 mwezi uliopita, ikiwa zaidi ya siku 30 zimeshapita, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitangaza kufungwa shule na vyuo, kama sehemu ya jitihada kudhibiti na kupambana na ueneaji virusi vya corona nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, siku chache zilizopita alitangaza kuwa wasafiri wote kutoka nchi zilizoathirika na corona, watalazimika kukaa karantini kwa siku 14 katika hosteli za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) maarufu 'Hosteli za Magufuli.'

Anasema, utaratibu uliowekwa wa kukaa hotelini kwa sasa hautakuwepo, tena kwa lengo la kudhibiti mienendo ya saa 24 za washukiwa.

"Tumeona kule Iringa kuna wasafiri tuliwaweka hotelini wakatoroka, ili kudhibiti mienendo ya wasafiri hao na kulinda Watanzania wengi tumeona tuwaweke eneo moja 'Hosteli za Magufuli' ambako kutakuwa na ulinzi wa saa 24, RC (Mkuu wa Mkoa) Makonda atasimamia kwa karibu chini ya Wizara ya Afya," anasema.

Pia, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, mwanzoni mwa wiki hii alitangaza rasmi kuahirisha mitihani ya kidato cha sita, iliyotarajiwa kuanza kufanyika tarehe 4, mwezi ujao.

Ni hali inayowaacha wanafunzi nchini katika mjadala usiokuwa na majibu, kuhusu hatma ya wao kurudi shuleni, iwapo corona itaendelea kuongezeka na hadi sasa kufikia 24. Hivi sasa zimebaki wastani wa wiki mbili kumaliza siku 30 zilizotolewa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

#### UGHAIBUNI KULIVYO

China ni miongoni mwa nchi zilizositisha kwa muda shughuli za elimu kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ikipambana na virusi vya corona, yenyewe ikiwa muasisi na sehemu iliyoathirika zaidi na ugonjwa huo.

Kuanzia Machi 28, 2020 serikali ya China ilitangataza kusitisha viza na hati zote za ukazi na kuzuia ndege kutoka mataifa mengine kuingia nchini humo, hali iliyowafanya wanafunzi wa nchi mbalimbali wanaosoma huko, ikiwamo Tanzania kushindwa kurejea China kuendelea na masomo.



Wataaluma katika Idara ya Afya ya Dunia katika Chuo Kikuu cha Washington, Marekani wakiwa maabara, wanafanyia kazi nyendo za ugonjwa corona.. **PICHA: MTANDAO**

> **Waziri Mkuu Boris Johnson, aliyeingia wodini Jumatatu wiki hii, baada ya kugundulika ni mgonjwa, Jumanne alikuwa na hali mbaya ya kupekewa wodi maalumu.**

Serikali ya nchi hiyo ilifikia hatua hiyo mara baada ya kuona corona, umekuwa tishio nchini humo.

"Katika kudhibiti kuenea kwa corona, serikali ya China imetangaza kisitisha viza (ruhusa ya kuingia nchini) na hati za ukazi, hivyo safari zote za kimataifa hazitaendelea.

"Kwa mujibu huo, wanafunzi wote wa Tanzania wanaosoma China, wasitishe mipango ya kurejea China hadi itakapotangazwa tena," ubalozi wa Tanzania nchini China ulisema.

Nchini Italia, Waziri wake, Giuseppe Conte, alitoa wito kwa Umoja wa Ulaya (EU) kutumia uwezo wao imara wa fedha, kupambana na mlipuko wa corona.

Anasema janga hilo limekuwa tishio kuanzia Kaskazini hadi Kusini, Mashariki na Magharibi mwa dunia kwa wastani na maambukizi hayo yameendelea kuzua wasiwasi katika mataifa yote duniani, hasa Ulaya na mipaka yote

Ni hali inayofanya shughuli mbalimbali za Italia kufungwa na hata kuwazuia watu kutoka nje, jambo lililowaathiri hadi wanafunzi, hali iliyowafanya kushindwa kuendelea na masomo hadi pale hali itakapotengemaa.

Nchini Uingereza nako si shwari, hata imefikia hatua ya kuwaomba madaktari wastaafu warudi kazini, kusaidia kukabiliana na janga la corona.

Pia, Baraza la Wauguzi Wakunga nchini humo liliwaandikia barua zaidi ya wauguzi 50,000 pamoja na madaktari 15,000 wastaafu, ili warudi kusaidia kupambana na suala hilo.

Ni hali iliyowafanya wanafunzi nchini humo kushindwa kuendelea na masomo kwa kuepusha misongamano.

Waziri Mkuu Boris Johnson, aliyeingia wodini Jumatatu wiki hii, baada ya kugundulika ni mgonjwa, Jumanne alikuwa na hali mbaya ya kupekewa wodi maalumu.

Wengine wazito kiserikali waliogswa na corona nchini humo ni mwanamfalme, Prince Charles na Naibu Waziri wa Afya, Nadine Dorries.

Marekani maambukizi yamezidi maradufu na sheria ya kuwalazimisha watu wakae nyumbani, ndiyo imeendelea kutolewa, wanafunzi pia ni miongoni mwa waathirika wa agizo hilo.

Kando na majiji ya New York, Washington na California, ni miongoni mwa majimbo yaliyozongwa na janga la corona.

Meya wa New York, Bill de Blasio, alikiambia chombo cha habari cha CNN siku chache zilizopita kuwa, jimbo hilo maarufu nchini Marekani litakosa vifaa vya kimatibabu katika kipindi cha wiki tatu ikiwa mlipuko wa maambukizi utaendelea kwa kiwango kikubwa.

Kwa maana hiyo, aliitaka serikali kuu kulisaidia jiji hilo kupata vifaa vya kusaidia kupumua 15,000, barakoa milioni 50 na magauni mengi na vifaa vya madaktari kujikinga.

Nchini Afrika Kusini, kama ilivyo nchi nyingine kuwa na maambukizi ya virusi na hivyo Rais wa Afrika Kusini, Cyrille Ramaphosa, alitangaza kusitishwa kwa safari kutoka katika mataifa yenye tishio kubwa la covid-19 kama Italia, Ujerumani, China na Marekani.

Vilevile walitangaza kusitisha mikusanyiko jambo ambalo liliwafikia hadi wanafunzi shuleni, mtu yeyote ambaye ataeneza habari za uwongo kuhusu corona atakabiliwa na adhabu ya miezi sita gerezani, kulingana na sheria mpya ya nchi hiyo.

Katika jimbo la Berlin nchini Ujerumani, hadi kufikia April 7 taasisi ya Robert Loch nchini humo, inaripoti kwamba idadi ya mikasa ya virusi vya corona vilivyothibitishwa, vimefika 99,225 na wagonjwa 1,607 wamekufa

Aidha, mkoa wa Bavaria, umeendelea kuwa kitovu cha maambukizi mapya ya ugonjwa huo, mikasa kukiwapo 26,168 iliyothibitishwa, ikifuatiwa na North Rhine, Westphalia na Bedan Wurttemberg, ambako napo shughuli za kukusanya watu zilizuiliwa.

Hapo inajumuisha shuleni, hali inayofanya wanafunzi waendelee kukaa nyumbani hadi pale tatizo la corona litakapoisha.

MAZINGIRA

KUTOKA VIJIJINI...

# Ruwasa katika ushindi unaomtua ndoo mwanamke wa Shinyanga

• Waliofuata maji km. 3, imewajia mlangoni • DC akoshwa, aja na ziara ya ushuhuda



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (kushoto), akiangalia wananchi wanaochota maji katika Kijiji cha Lyabusalu, Shinyanga, kwenye mradi unaotekelezwa na Ruwasa.

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

SERA ya Maji ya Mwaka 2002, inasema asilimia 85 ya wananchi vijijini wapatiwe maji safi na salama ifikapo mwaka 2020, huku mijini kukilengwa asilimia 100.

Serikali hivi sasa imeshaanzisha Wakala wa Maji Vijijini (Ruwasa), lengo ni kuongeza kasi ya utekelezaji miradi ya maji vijijini ili katika mwaka uliopo 2020, wananchi wake wafikiwe na maji safi na salama kwa asilimia 85 kama sera inavyoainisha.

Ruwasa wilayani Shinyanga, imekuwa na kasi kubwa ya utekelezaji miradi mingi kuondoa changamoto ya uhaba wa maji, pamoja na 'kumtua ndoo kichwani' mwanamke wa kijijini, hali inayomuokolea muda na safari ndefu ya kufuata maji.

Emmanuel Nkopi ni Kaimu Meneja wa Ruwasa, wilaya ya Shinyanga, anayesema miradi mingi ya maji wanayoitekeleza kwa wananchi, ni ya maji kutoka Ziwa Victoria.

Nkopi anasema, kuna baadhi ya miradi imeshaanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi, ikiwamo katika vijiji cha Mwiseme na Lyabusalu, huku miradi inayotarajiwa kukamilika mwezi huu, ni iliyoanza ujenzi Februari mwaka huu.

> **Tunashirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shuwasa), ambao wao wametoa Sh. milioni 100 na sisi Ruwasa milioni 50.**

Anasema miradi hiyo iliyoko katika vijiji vya Uzogole, Mwang'osha, Lyabusalu, Mwiseme na Masengwa, ipo kwenye hatua ya uunganishwaji mabomba na anafafanua: "Katika mradi wa maji kijiji cha Uzogole gharama yake ni Sh. milioni 150.

"Tunashirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (Shuwasa), ambao wao wametoa Sh. milioni 100 na sisi Ruwasa milioni 50.

"Mradi wa Maji kijiji cha Mwang'osha tunautekeleza sisi wenyewe ambao una gharama ya Sh. milioni 40; Lyabusalu Sh. milioni 39; Mwiseme Sh. milioni 41 na mradi mkubwa wa Masengwa, wenyewe una gharama ya Sh. bilioni 4.19 na miradi yote hii mwezi huu itakuwa imekamilika."

Nkopi anasema, kuna mikakati mikubwa ya utekelezaji miradi ya maji vijijini katika wilaya ya Shinyanga, ili kuhakikisha Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inatekelezwa ipasavyo na kuondoa changamoto ya uhaba wa maji vijijini.

Taarifa ya Jimbo la Solwa wilayani Shinyanga, iliyosomwa na mbunge wake, Ahmed Salum, mbele ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ni kwamba kuna vijiji 126 na kati yake, 93 ndio vina maji safi na salama.

Salum anasema, mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria unatekelezwa katika Kata ya Masengwa, ambao utakapokamilika mwaka huu, kuna matarajio ya kunufaisha vijiji 14 vitakavyopitiwa na bomba kuu la maji, ikiwa ni hatua ya upatikanaji maji safi na salama.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (wa pili kushoto), akiwa na Kaimu Meneja wa Ruwasa, Emmanuel Nkopi, kukagua ufukiaji mabomba, kwenye mradi wa maji Kata ya Masengwa. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**

### DC MBONEKO

Jasinta Mboneko, ni Mkuu wa Wilaya Shinyanga, katika ziara ya kukagua utekelezaji miradi ya maji wilayani kwake, anasisitiza itekelezwe kwa wakati, ili kuondoa adha ya kupoteza muda wa shughuli za kiuchumi, kwa sababu ya kutafuta maji safi na salama.

Mkuu wa Wilaya, anaipongeza Ruwasa kutekeleza miradi mingi ya maji kwa muda mfupi walioanza kufanya kazi, akiwataka waendeleze kasi hiyo, huku akisisitiza vituo watakavyovitenga kwa wananchi kuchota maji, viwe karibu na makazi ya watu, ili kumtua ndoo mwanamke.

"Nimefanya ziara hii, ili kukagua kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji katika wilaya ya Shinyanga. Nimeona inaridhisha na Ruwasa wanafanya kazi vizuri.

"Baadhi ya miradi nimeona imeshaanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi, licha ya kutokamilika kwa asilimia 100 jambo ambalo ni hatua nzuri.

"Lengo la utekelezaji wa miradi hii ya maji, ni kukakikisha wananchi hawapotezi tena muda wa kufanya shughuli za kiuchumi, kwa sababu ya kutafuta maji safi na salama kutoka umbali mrefu, bali maji yawe karibu na wachape kazi," anaeleza.

Pia, rai yake kwa wananchi wanaotekelezewa miradi hiyo ya maji safi na salama, watunze miundombinu iliyopo wasiiharibu, iweze kudumu kwa muda mrefu kutoa huduma ya maji safi na salama.

### MWANAKIJIJI

Margret Maige, ni mwanamke mkazi wa kijiji cha Mwang'osha, Shinyanga eneo unakotekelezwa mradi wa maji safi na salama, anasema, wamekuwa wakifuata maji umbali mrefu takriban kilomita tatu na kuna wakati wanatumia maji ya bwawa.

Anasema, kukamilika mradi huo mpya utakuwa msaada mkubwa kwao, ukiokoa muda ambao wamekuwa wakipoteza katika mbadala wa shughuli za kiuchumi, ikiwamo kilimo.

Sambamba na hiyo, Margret anasema, huduma ya maji itakuwa karibu pamoja na kutoingia tena kwenye migogoro ya ndoa kwa kuhisiwa vibaya na waume wao.

"Tunaipongeza sana serikali kwanza... sababu tatizo la maji likitokea wa kuhangaika ni mwanamke na siyo mwanaume. Sisi ndio tunalea familia na ndio maana nimekuja kuchimba mtaro wa mabomba na kuyafukia ili tupate maji haraka," anasema Margret.

Mwingine, Mariam Madoshi, mkazi wa kijiji cha Mwiseme, anasema mradi kijijini humo utakuwa mkombozi kwao, kwa kuondokana na matumizi ya maji ambayo siyo salama kwa afya zao na kuepuka safari ndefu waliyotumia kufuata.

### MWENYEKITI KIJIJI

Mwenyekiti wa kijiji cha Mwiseme katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Deus Nyema, anaipongeza serikali kupitia wakala huyo wa maji vijijini Ruwasa, akilalamika kijiji hicho kilikuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa maji safi na salama.

Anasema, wakati wanaletewa mradi huo wa maji kijijini hapo, ilibidi wahamasishe wananchi kujitolea kuchimba mitaro ya maji umbali wa kiliomita tano, kuonyesha uzalendo wao wa hamu ya kupata maji yao safi na salama kijijini humo.

"Tulikuwa tunapata shida sana ya kutafuta maji ya kunywa umbali mrefu na wake zetu ndio walikuwa wakihangaika kufuata maji hayo, wakiamua mida ya usiku, lakini sasa hivi shida hiyo imekwisha kabisa," anasema Nyema.

Diwani wa Kata ya Solwa, Awadhi Abood, anasema miradi ya maji vijijini inawakomboa wananchi katika kuinua uchumi, kwa sababu hawatapoteza muda, mbadala wake watajikita katika shughuli za maendeleo.

> **Nimefanya ziara hii, ili kukagua kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji katika wilaya ya Shinyanga.**

Anasema suala la ukuaji uchumi katika jamii, lina uhusiano mkubwa sana na upatikanaji wa maji, hivyo kuwapo vijiji au jamii inayokosa huduma ya maji, wanarudi nyuma kimaendeleo.

"Nampongeza sana Kaimu Meneja wa Ruwasa," anasema Abood na kuendelea: "Yaani ndani ya kipindi hiki kifupi ametekeleza miradi mingi ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini."

Huku akitoa kauli ya 'kujipigia debe' kwamba katika kipindi kilichopo cha lala salama ya awamu yake ya uongozi, anaahidi kuendeleza ushirikiano wa wananchi kujitolea katika kufanikisha miradi hiyo.

---

# Corona yaleta mapya ndani ya uzazi mpya



Mama mjamzito. **PICHA: AL JAZEERA**

**Na Mwandishi Wetu**

JANGA corona hadi sasa limevuruga mipango mingi duniani, ikiwamo ya mama wajawazito.

Kada hiyo ya wazazi ilikuwa na mipango mingi ya kukaribisha watoto wao wapya, huku katika mataifa mengine, tayari walishaanza kupata huduma za afya majumbani mwao.

Katika maeneo mbalimbali sasa duniani, imekuwa jambo gumu kwa familia kutenganishwa hasa pale katika utamaduni unaokusanya watu, kuonyesha upendo.

Wakati uliopo, ghafla imekuwa tofauti kwa wanawake wanaojifungua kuwa na mazingira magumu, hata kutembelea kwenda kumuona mtoto mpya nyumbani au hospitalini, mahali aliko kwa wakati huo.

Kwani utamaduni, hasa jamii za Kiafrika safari za wageni na zawadi mkononi kumkaribisha 'kadogoo' huyo.

Sheria za kuona wagonjwa hospitalini zimebadilika. Zinazuia idadi ya watu na hata mama anapojifungua bado, wageni ni ngumu kwenda kumuona mtoto mpya au kumpa hongera mama kama amejifungua salama.

Kizazi cha sasa ni kile ambacho hakikubali watu wawe karibu 'social distance generation'. Sasa wazazi wanapohitajika kujitenga wawezavyo, ili kuepuka maambukizi haya kwa watoto na mama, ni mtihani mkubwa.

Kwenye mitandao ya kijamii watu wamekuwa wakirushiana masihara ya majina yanayoweza kupewa watoto wapya wa zama hizi za corona.

Maana kihistoria, katika jamii nyingine za kiafrika, mtoto anapewa majina kulingana na msimu au tukio fulani. Hapo ndio unasikia kina Chausiku, aliyezaliwa usiku, Shida, Majuto na Furaha, ambaye kizungu ndiye Happy.

Wapo walioibuka na mashihara, ikizingatiwa kuna baadhi wanaobadilisha mitandao kwa staili wanavyopenda, wakidai wanaweza kuibuka na majina Barakoa kwa Waswahili, pia Mask na Sanitizer kwa wanaoongea Kizungu. Nini imezaa hilo?... yatokanayo na hekaheka za corona.

Katika mtandao wa 'Tweeter', kuna wazazi wa mtoto mpya waliandika kuwa wamejitenga na familia kwa muda wa siku 14 kwa kuwa wakati huo ni wa kizazi cha 'social distancing'(kutengwa na jamii) na watu zaidi ya 700,000 walifanya hivyo duniani.

Ni sehemu ya mageuzi mengi ya muda, yanaweza kushuhudiwa katika zama zilizopo za mlipuko wa virusi corona.

Kwa baadhi ya wanawake, sasa wanapaswa kujifungua wenyewe bila kusindikizwa na wenza wao na wale wanaochagua kujifungua kwa upasuaji, nafasi hiyo ni ya mjadala kitaalamu.

Matarajio zaidi watayapata pale kwenye matatizo ya kujifungua kawaida na wanalazimika kuhamia katika operesheni.

Maeneo mengine kwenye utamaduni wa kuamini kujifungulia nyumbani ni salama zaidi ya kwenda hospitalini, umekuwa ni wakati wa hofu kubwa kwa wazazi wapya,

Awali mama anayekaribia kujifungua, alikuwa anaweza kupata wakati wa kujiandaa kwa mahitaji ya watoto kuzinunua au kuangalia kinachomfaa katika hilo. Leo, hali imebadilika.

Wapo waliofanya sherehe kwa mama kabla au baada, sasa sherehe hizo hazipo tena.

Mzazi mmoja aliyepata maambukizi ya corona na wahudumu wa afya walimshauri asijifungue kwa upasuaji, bali asubiri ili ajifungue kawaida.

Hofu yake kuwa ilikuwa mtoto wake kuja duniani na kukutana na janga la corona, huku mama na baba yake akiwa amevalia barakoa.

Nikki na mume wake walitengwa kwa muda wa siku 14, wakiwa pamoja na mtoto mchanga.

**Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.**

AFYA

# Makali ya kuugua yanaendana, kiasi virusi vilivyomo mwilini

• Hali maambukizi ilikofika, dalili na kinga zilikosimamia...



Mhudumu wa afya, akipima joto la mwananchi kwenye eneo la mpakani mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Uganda, pindi lilipozuka janga la Ebola, Februari, mwaka jana. **PICHA: UNICEF**

**Na. Jackson Paulo**

UGONJWA wa Corona au COVID-19 unasababishwa na virus, vinavyoenea kwa kasi duniani kote, huku idadi ya vifo nayo ikionyesha dalili za kupungua hadi sasa.

Wakati janga hilo likiendelea kupamba moto, kuna tafiti tayari zinaendelea kufanywa kwa kasi, ili kubaini tabia za virusi hivyo, ikiwa ni pamoja na kuujua vizuri ugonjwa wenyewe, kuanzia maambukizi, dalili, tiba hata kinga.

Katika siku za hivi karibuni, utafiti mpya uliofanyika nchini China na kuchapishwa katika jarida la kitabibu la nchini Uingereza la Lancet mwezi Machi, ulionyesha kuna uhusiano kati ya kiasi cha virusi ambacho mtu anaambukizwa kwa mara ya kwanza na makali ya dalili za ugonjwa kwa mhusika.

Kitaalamu, mzigo wa virusi au kitaalamu 'viral load' ni kiasi kinachomuingia mtu mwilini pindi anapoambukizwa ugonjwa kwa mara ya kwanza.

Utafiti umebaini kuwa, watu wanaweza kuwa na dalili tofauti za corona, kulingana na kiasi cha virusi kilichowaingia wakati wa maambukizi.

**KUJITENGA JE?**

Wanasayansi wanasema, njia ya kupunguza maambukizi ya corona kwa utaratibu wa 'kujitenga kijamii' au wenyewe wasomi wanaita 'social distancing' imeonekana kusaidia kwa kuwafanya watu kupata dalili za kiwango cha kawaida, pale wapatapo maambukizi ya virusi vya corona.

> **“Ili kujizuia kuambukizwa 'mzigo mkubwa' wa virusi, jambo bora mtu analioelezwa anaweza kufanya, ni kuepuka kukaa karibu na wanaohofiwa kuwa nao au ambao tayari ni wagonjwa.**

Hiyo inatokana na sababu kwamba, dhana ya kujitenga kijamii, imeonekana kuwafanya watu kupata maambukizi yenye kiasi kidogo cha 'mzigo wa virusi.'

Mtu anaweza kupunguza uwezekano wa kupata maambukizi makubwa kwa kuepuka kusogeleana na yule ambaye kwake yawezekana akawa mgonjwa wa corona au kwa kufuata ushauri na sheria mbalimbali zinazohusu kuepuka mikusanyiko, ambazo mamilioni ya watu duniani kote wameshauriwa kufuata.

Kupata mzigo mkubwa wa virusi mwilini wakati wa maambukizi kunaipa virusi nguvu kubwa ya kuanza kukudhuru (jump start), hivyo inaongeza hatari ya mfumo wa kinga ya mwili kuzidiwa uwezo wa kupambana.

Kupata virusi 'vichache' wakati wa maambukizi ya ugonjwa kunaweza kusaidia kinga ya mwili kushtuliwa mapema hivyo kujiweka tayari au kujiandaa vyema dhidi ya mashambulizi, hali inayochangia uwezekano wa mwili kudhibiti ugonjwa kabla ya kuzidiwa au kabla dalili kuanza kuonekana.

Wataalamu wanabainisha kuwa, watu wanaweza kupokea mwilini kiwango tofauti cha virusi vya corona kutokana na njia waliyopita kupata virusi hivyo.

Hiyo ina maana kuwa, mtu aliyeambukizwa virusi vya corona moja kwa moja kupitia kugusa kitasa cha mlango, anaweza kuishia kupata dalili za kiwango kidogo kuliko aliyeambukizwa kupitia kuvuta hewa, baada ya mtu mwenye corona kukohoa au kupiga chafya

Tafsiri iliyoko ama kwa wauguzi au madaktari waliopata maambukizi kupitia wagonjwa wanaoumwa sana corona, wapo kwenye uwezekano wa kupata dalili kali za ugonjwa, kwa maana wanakuwa katika mazingira hatarishi ya kukutana na mzigo wa virusi vingi, pale mgonjwa anapopumua karibu na nyuso zao wakati wa matibabu.

Kadhalika, viongozi wa kidini wanaangukia katika hatari ya kuambukizwa vijidudu vya magonjwa ya njia ya hewa na kuingia katika hatari ya kupata corona yenye dalili kali.

Hadi kufikia hivi sasa, kuna viongozi wa kidini 60 walioathiriwa nchini Italia na nchini Uingereza, matabibu wawili wamekwishafariki dunia baada ya kuugua ugonjwa huo.

Pia, nchini Uingereza Jumatatu iliyopita, sasa imethibitika Waziri Mkuu Boris Johnson, aliyejitenga kujihisi ana virusi hivyo, sasa ni rasmi amethibitika anavyo na kuingizwa katika ulingo wa matibabu.

Kwa ujumla ni kwamba, virusi vinavyoshambulia mfumo wa upumuaji kama corona, huwa na matokeo tofauti kutegemeana na kiasi cha virusi mtu alivyopata wakati wa maambukizi.

Ni sawa na kulinganisha idadi ya askari au ukubwa wa vikosi vya pande mbili. Hii ina maana kuwa jeshi la virusi likiwa kubwa zaidi, ndivyo inakuwa vigumu kwa jeshi la kinga ya mwili kumudu mashambulizi.

**KAZI YA VIRUSI**

Virusi vinapoingia mwilini, vinachangia mtu kuanza kuugua baada ya virusi kuongezeka idadi kwa haraka, hivyo kinga mwilini inashuka na kufanya kazi katika sura ya 'kasi iliyopitiliza' ili kupambana navyo.

Hapo inaibua dalili kama homa, uchovu, na maumivu ya mwilini.

Mara baada ya virusi kuzaliana kwa kasi mwilini, kinga ya mwili huzidiwa uwezo na inachukua juma kadhaa kuangamiza 'vijidudu' vyote.

Katika nadharia, kinga ya mwili inaweza kukabiliana na hata kuvishinda virusi mapema tu, mara baada ya kupata maambukizi, hivyo, hata mtu asijue kama anaugua ugonjwa fulani.

Tafiti zimeonyesha kuwa, virusi vya corona vimeonekana kuwa na tabia inayofanya baadhi ya wagonjwa kuchukua muda mrefu kuanza kuonyesha dalili au kuhisi ni wagonjwa na hiyo limekuwa likiwafanya watu wengi kuendelea kueneza corona pasipo kujijua.

Mtu anapopata maambukizi ya virusi 'vichache' anapata nafasi ya kuushinda ugonjwa na anapopata maambukizi ya 'mzigo mkubwa' wa virusi sio tu inakuwa hatari kwa mgonjwa mwenyewe, bali pia walio karibu naye, kwa sababu inamfanya aambukize wengine haraka zaidi.

Kadri unavyokuwa na virusi vingi ndani ya mwili wako, ndivyo unavyotoa nje virusi zaidi wakati wa kupumua, kukohoa au kupiga chafya, Ni hali inayojulikana kitaalamu kama 'kumwagwa kwa virusi' au 'viral shedding'.

Ili kujizuia kuambukizwa 'mzigo mkubwa' wa virusi, jambo bora mtu analioelezwa anaweza kufanya, ni kuepuka kukaa karibu na wanaohofiwa kuwa nao au ambao tayari ni wagonjwa.

Mzigo wa virusi unakuwa mkubwa ikiwa mtu amekukoholea karibu na uso, kuliko anapokuwa umbali wa mita mbili au zaidi, maana virusi hutawanyika zaidi hewani.

**JINSI YA KUJIHAMI**

Inashauriwa kuwa, kila wakati mtu anapaswa kuhakikisha yupo umbali wa mita moja au mbili kutoka kwa wengine na ikiwa anaishi na aliyeambukizwa corona, anapaswa kuepuka kuwa karibu naye, kwa kukaa umbali wa mita mbili (miguu sita), ikiwa inawezekana.

Pia, mtu anashauriwa kuacha kukumbatiana au kumbusu mtu, kulala vitanda tofauti inapobidi na kuhakikisha unasafisha kila

INAENDELEA UK.19

AFYA

# Makali ya kuugua yanaendana, kiasi virusi vilivyomo mwilini

INATOKA UK.18

mara kwa mara sehemu zote zinazoweza kuguswa kwa mikono kama vile vitasa vya milango.

Mantiki ya 'kujitenga kijamii' au 'social distancing' ni kwamba kusimama mbali na mtu mwingine wakati anapumua, kukohoa ama kupiga chafya kunatoa uwezekano wa chembe chache za virusi kuweza kufikia au kuingia mwilini.

Kwa kawaida, watu wanapopata virusi vya corona, huwa vinazaliana ndani ya miili, japokuwa kila mtu anaambukizwa kiasi tofauti cha mzigo wa virusi.

Mtu anayepata virusi vya corona, aliyekohoa au kupiga chafya , hasa akiwa na homa kali ni hatua anayokuwa na virusi zaidi, akipokea kiasi kikubwa cha virusi kuliko mtu aliyepata kupitia kugusa kitasa cha mlango kilichoguswa na mgonjwa siku mbili zilizopita.

Dalili za corona husababishwa na majibu yatolewayo na kinga ya mwili, pale tu virusi vinapogundulika mwilini.Katika nia ya kuangamiza virusi mwili hubadili joto lake la ndani ili kuwaua virusi hali ambayo hupelekea mtu kupata homa.

Pia, mwili unatumia kiwango kikubwa cha nguvu ya kalori kwa lengo la kupeleka seli za kinga kwenye damu ili kushambulia virusi, kitendo ambacho husababisha hali ya uchovu na mwili kuuma. Kwa maana hiyo, inapokea idadi ndogo ya virusi wakati wa maambukizi na kusaidia kinga ya mwili kuanza mapambano kwa kiwango cha chini, hivyo mtu anapata homa kali, uchovu au mwili kuuma.

Hiyo ni sawa na kusema kuwa mtu anapopata maambukizi yenye 'mzigo mkubwa' wa virusi, mapambano huwa ni makubwa, yanayosababisha dalili kama homa kali.

**MAAMBUKIZI YALIVYO**

Shirika la Afya Duniani (WHO), hadi kufikia Machi 31 mwaka huu, linaripoti mikasa ilivyothibitishwa duniani kote, kuwapo waathirika 750,890 na idadi ya vifo 36,405.

Barani Afrika, idadi ya visa kwa kipindi hicho tajwa ilifikia watu 3,786 huku idadi ya vifo ikifikia 77. Nchini Tanzania, kumeripotiwa idadi ya visa 19 na kifo kimoja.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mtandao Worldometer, hadi Aprili 6, tayari duniani kulikuwapo waathirika 1 291, 845 na jumla ya vifo 70, 675 na kati yao waliofariki ni 272 426, hivyo kufanya wagonjwa waliobaki hadi alasiri ya Jumatatu wiki hii kuwa 949,138.

Nchini Tanzania hadi Jumatatu kuna ongezeko la waliopatwa na ugonjwa huo kufika 24 na kifo bado ni kimoja.

**FAHAMU DALILI ZA COVID-19**

Baadhi ya watu walioambukizwa virusi vya corona hawaonyeshi dalili. Hata hivyo, virusi vinaposababisha dalili za kawaida, huwa ni pamoja na homa ya kiwango cha kawaida, maumivu ya mwili, kukohoa, kutoka kamasi puani na kupata maumivu ya kooni.

Hata hivyo, pale virusi vya corona vinaposababisha dalili kali zaidi, huwa ni pamoja na homa kali, kikohozi kikali, na kubanwa pumzi ambayo mara nyingi inaashiria homa ya mapafu.



Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, wakati wa mlo hospitalini, Jumatatu wiki hii alipolazwa, Baada kugundilika kuwa na corona. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Mara baada ya virusi kuzaliana kwa kasi mwilini, kinga ya mwili huzidiwa uwezo na inachukua juma kadhaa kuangamiza 'vijidudu' vyote.**



Wakazi wa jijini Lilongwe, Malawi wakinawa mikono kujihami na maambukizi ya corona.

**KUJIKINGA**

• Unatakiwa kuosha mikono yako kila mara kwa sabuni na maji tiririka au kwa kutumia kitakasa mikono 'sanitizer.'

• Epuka kukaribiana na mtu (kaa angalau mita moja dhidi ya mwenzako).

• Epuka kugusa macho yako, pua au mdomo kwa mikono ambayo haijasafishwa vizuri.

• Kaa nyumbani, ikiwa unajihisi mgonjwa.

• Funika kinywa wakati wa kukohoa au kupiga chafya (kwa kutumia kiwiko)au piga chafya kutumia tishu, kisha utupe tishu hizo kwenye chombo cha taka.

• Safisha kwa dawa ya kuua vijidudu vitu au sehemu zote zinazoguswa mara kwa mara kama kitasa.

***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za afya kimataifa, ikiwamo kutoka WHO. Mwandishi anapatikana kwa anwani ya barua pepe: jacpole@gmail.com***

AFYA

# Kabichi: Mlo, tiba, kinga afya



Kabichi iliyokwishaandaliwa. **PICHA ZOTE : MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

UNAPOTAMKA kabichi, mzizi wake unaanzia katika lugha ya Kiingereza neno 'cabbage.' Hiyo kiasilia ni mboga yenye umbo la mviringo mkubwa na ina rangi ya kijani au nyekundu asili yake ni zaidi ya miaka 1000 huko barani Ulaya.

Kabichi inaweza kuliwa baada ya kupikwa au ikiwa mbichi na ina manufaa mengi kwa afya ya binadamu. Kwa kawaida, kichwa chake huwa na wastani wa uzito kati ya nusu kilo hadi kilo nne na historia inaonyesha, mwaka 2012, lilikuwa na uzito kilo 62.71.

Kwa kawaida, inavunwa katika mwaka wa kwanza wa mzunguko wa maisha ya mmea huo na ile inayoachwa kuendelea kwa ajili ya mbegu inaruhusiwa kukua mwaka wa pili.

### UTAJIRI LISHE

Kabichi inaweza kuliwa likiwa bichi pindi linapochanganywa kwenye kachumbari au kupikwa. Ina utajiri wa Vitamini muhimu kwa wingi; A, B, C, E na K, ambazo zina faida kubwa mwilini.

Wakati Vitamini A husaidia kuimarisha ngozi na uwezo wa kuona, Vitamini B inaimarisha uwezo wa kutafakari na kuboresha utendaji kazi wa ubongo, huku ikizuia msongo wa mawazo kwa binadamu.

Pia, Vitamini C inaimarisha kinga ya mwili na kuzuia visababishi vya saratani na Vitamin E, inaifanya ngozi kuwa nyororo zaidi.

Nyingine ni Vitamini K, inayoimarisha mifupa na kusaidia damu kuganda mtu anapoumia. Pia kuna Vitamini B1 na B2.

> **Kabichi imeonekana kuwa na uwezo wa kipekee katika kupambana na ugonjwa huo, kutokana na kuwa na kiasi kikubwa cha aina tatu muhimu za virutubisho.**

Mengine ni madini ya kambalishe (fiber), manganizi, potasiamu na aina ya tindikali maarufu 'fatty-3 acids' vyote vikiwa ni kinga ya mwili dhidi ya magonjwa nyemelezi.

Kabichi, pia inatibu michubuko mbalimbali ya mwili na inasaidia kupunguza uzito au unene, kwani ina kiwango kidogo sana cha kabohaidreti na mtu anayetaka kupunguza unene na uzito, anashauriwa kula saladi ya kabichi kwa wingi.

Pia, ni mlo inaokabili tatizo la kufunga choo, kutokana na 'kambakamba' zinazosaidia kulainisha choo na vilevile madini ya salfa na chuma yanayosaidia kusafisha utumbo.



Kabichi kutoka shambani.

### JUISI KABICHI

Wataalam wanasema, kabichi lina madini ya calcium na chuma, yanayoponyesha vidonda vya tumbo linapotumika katika mfumo wa juisi.

Kutengeneza juisi, ni vyema kunywa mara moja kabla haijakaa sana na glasi moja inasaidia kuondoa mhemko au msongo kwenye akili na ina uwezo wa kumuondolea mtu woga na hata kuumwa kichwa, hasa muda wa mchana.

Mtu anapojisikia vibaya kunywa juisi ya kabichi, ni vyema akachanganya na asali au juisi ya karoti, kwani nayo ina faida nyingi kwa afya ya mwanadamu.

Kuna mengine yanatajwa ni tiba ya vidonda tumbo, kwani kuna utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Tiba cha Stanford, Marekani ukionyesha jumla ya wagonjwa 13 waliopona vidonda vyao.

Hiyo inatokana na dozi ya kunywa juisi ya kabichi, wastani wa mara tano kwa siku kwa muda wa siku kati ya saba na 10 au katika lugha ya kawaida ni kati ya wiki moja hadi wiki moja na nusu.

TIBA YAKE

Ni katika kipindi cha miezi mitatu, mtu anaweza kula kachumbari ya kabichi na spinachi, iliyochanganywa na nyanya na kitunguu, maji na limao kidogo, bila ya chakula kinginecho kwa muda mrefu.

Hiyo inaendana na matumizi ya juisi ya karoti milimita 200, ikiongezwa na milimita 100 za juisi ya spinachi, ikitumiwa mara tatu kwa siku.

Katika miji mikubwa, kabichi inatumika zaidi kwa walaji wa chips. Hata hivyo, inaelezwa hawaitumii ipasavyo, kwa sababu inapikwa na kukaangwa kwa mafuta kwa muda mrefu na kupoteza baadhi ya virutubisho vyake muhimu.

Faida nyingine ya mlo kabichi (nyeupe na nyekundu) ni kutoa kinga dhidi ya ugonjwa wa saratani, kukiwepo na majibu yake.

Inaelezwa kuwa, tafiti nyingi zimeshafanyika kuhusu virutubisho vinavyopatikana kwenye kabichi na kuthibitisha vina uwezo wa kuzuia ugonjwa wa saratani.

Kabichi imeonekana kuwa na uwezo wa kipekee katika kupambana na ugonjwa huo, kutokana na kuwa na kiasi kikubwa cha aina tatu muhimu za virutubisho.

Mbali ya kuwa na uwezo wa kutoa kinga dhidi ya ugonjwa wa saratani, juisi ya kabichi inaelezwa kuwa na faida nyingi kwa wenye matatizo ya vidonda vya tumbo.

Kuna utafiti uliofanyika na kuonyesha mboga hiyo inaimarisha mfumo wa moyo kwa kudhibiti utengenezaji lehemu mwilini, ambayo inapozidi mwilini, husababisha matatizo ya moyo.

Ili kupata faida za kabichi na kujenga kinga imara dhidi ya magonjwa ya saratani, mtu anatakiwa kuwa na mazoea ya kula kabichi kila mara, walau mara tatu kwa wiki kwa namna ambayo mtu ataona inamfaa, iwe kama mboga au kachumbari.

***Ni kwa mujibu wa taarifa za mtandao.***

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

## VIONGOZI WA OFISI YA RAIS-TAMISEMI



WAZIRI WA NCHI, OR-TAMISEMI
MHE. SELEMANI S. JAFO (MB)



NAIBU WAZIRI, (A) OR-TAMISEMI
MHE. JOSEPHAT KANDEGE. (MB)



NAIBU WAZIRI, (E) OR-TAMISEMI
MHE. MWITA WAITARA. (MB)



KATIBU MKUU, OR-TAMISEMI
ENG. JOSEPH NYAMHANGA.



NAIBU KATIBU MKUU (E) OR-TAMISEMI
MH. GERALD MWELI



NAIBU KATIBU MKUU (A) OR-TAMISEMI
DKT. DOROTHY GWAJIMA

## HOTUBA YA OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais-TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2020/21.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao madhubuti ambao umekuwa dira katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri katika kuongoza Mhimili wa Bunge. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa mchango wao mkubwa katika kuchambua Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2020/21. Kamati hii ilijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na kuyapitisha kwa kauli moja. Aidha, Kamati imekuwa ikitoa ushauri ambao umesaidia kuboresha utendaji wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kuwahudumia wananchi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mheshimiwa Rashidi Ajali Ahkbar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini. Naungana na wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wote walioguswa na msiba huo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kutoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilivyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha miaka minne iliyopita. Kwa mujibu wa Ibara ya 48 ya Ilani ya CCM, Ofisi yangu ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma bora za kiuchumi na kijamii ili kuchangia jitihada za kuondoa umaskini na kuharakisha maendeleo ya wananchi. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni katika sekta za afya, elimu, ujenzi wa majengo ya utawala, miundombinu ya barabara, na kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imesimamia ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Halmashauri 98, Vituo vya Afya 433 na Zahanati 368. Aidha, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umekuwa wa uhakika kwa **asilimia 92.**

8. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba 2015 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** kugharamia Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kwa upande wa miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari, Serikali imejenga na kukamilisha vyumba vya madarasa **19,808** na vyumba **1,313** vipo katika hatua za ukamilishaji, maabara za masomo ya sayansi **227** zimejengwa na Shule za Sekondari **1,258** zimepatiwa vifaa vya maabara, matundu ya vyoo **7,922** yamejengwa na kukamilika na matundu ya vyoo **571** yanaendelea kukamilishwa. Aidha, madawati **5,070,896** yametengenezwa na shule Kongwe za Sekondari **73** zimekarabatiwa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imesimamia ukarabati na ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa **74,940.06** ambapo kati ya hizo kilometa **485** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, jumla ya madaraja **232** na makalvati **7,168** yamejengwa na kukamilika.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imejenga majengo ya utawala 86 ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri. Kati ya majengo hayo, majengo 29 yamekamilika na 57 yapo katika hatua za ukamilishaji.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2019/20, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 2.99**. Hadi Februari 2020, makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri yalikuwa **Shilingi trilioni 2.54** sawa na **asilimia 85** ya lengo. Aidha, jumla ya **Shilingi bilioni 93.3** imewezesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

12. ***Mheshimiwa* Spika,** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imebuni, kusanifu na kujenga miundombinu na mifumo ya TEHAMA inayotumika katika maandalizi ya bajeti na mipango, ukusanyaji wa mapato na matumizi, usimamizi wa fedha za umma na Utawala na Bora. Mifumo iliyosanifiwa na kujengwa ni mtandao kiambo (LAN) na mtandao mpana (WAN) ambayo imeunganisha Mikoa 26, Halmashauri 185 za Tanzania Bara na Taasisi za Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Mifumo hii imechangia katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, usimamizi wa fedha, kupunguza gharama za mawasiliano na uendeshaji wa Ofisi.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, jumla ya ajira za kudumu na za muda **2,347,334** zimezalishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa. Wananchi wamenufaika na upatikanaji wa ajira hizo na kuboresha maisha yao.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za maendeleo zilizotekelezwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimegharimu takriban **Shilingi trilioni 6.31** katika kipindi cha miaka minne.

**B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA OFISI YA RAIS-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zilizo chini yake iliendelea kutekeleza vipaumbele vyake kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kusimamia na kuratibu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019; uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya msingi na elimu katika Shule za Msingi na Sekondari; kusimamia mpango wa utoaji Elimumsingi Bila Ada, usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha; kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi; uwezeshaji wananchi kiuchumi; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; kujenga miundombinu ya kiuchumi na kijamii ili kufungua fursa za kiuchumi mijini na vijijini na kuziwezesha Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kutekeleza majukumu yake.

**Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 802.6**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 36.46** ni za Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake**, Shilingi milioni 213.30** ni za Mikoa na **Shilingi bilioni 765.48** ni mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi bilioni 491.59** zimekusanywa sawa na **asilimia 61.28** ya bajeti iliyoidhinishwa.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa **Shilingi Trilioni 6.20** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo **Shilingi trilioni 3.81** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi bilioni 707.95** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi trilioni 1.69** ni za miradi ya maendeleo. Hadi Februari 2020, **Shilingi trilioni 3.89** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 62.59** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 563.29.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 496.56** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi bilioni 66.73** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi bilioni 413.65** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 73** ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 35.91** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 377.73** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake imekusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 25.06** sawa na **asilimia 80** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 31.23.** Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, mauzo ya huduma, ada za wanafunzi na tozo mbalimbali.

**Bajeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Utumishi wa Walimu ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 15.90** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 9.89** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi bilioni 6.00** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi Februari 2020, Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 7.04** sawa na **asilimia 44** ya bajeti. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha **Shilingi bilioni 4.41** za Mishahara na **Shilingi bilioni 2.63** za Matumizi Mengineyo.

**Bajeti za Mikoa**

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tawala za Mikoa ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 196.20** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 128.87** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 67.33** zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi bilioni 100.04** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi bilioni 84.97** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 15.06** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Mikoa imekusanya maduhuli ya **Shilingi milioni 77.29** sawa na **asilimia 35.29** ya lengo la kukusanya **Shilingi milioni 219.30.** Makusanyo ya maduhuli yametokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu.

**Bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**
**Makusanyo ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha, 2019/20, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya mapato ya ndani jumla ya **Shilingi bilioni 765.48** kutokana na ushuru, tozo na vyanzo mbalimbali vya mapato kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Hadi Februari 2020, Halmashauri zilikuwa zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 466.45** sawa na **asilimia 61.28** ya lengo la mwaka wa fedha 2019/20 ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.1).*** Makusanyo haya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 73.54** ikilinganishwa na **Shilingi bilioni 392.90** zilizokusanywa hadi Februari 2019, kwa mwaka wa fedha 2018/19.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kununua mashine za kielektroniki (POS) **7,227** ambazo zimetolewa kwenye Halmashauri zote ambapo Halmashauri zenye makusanyo madogo ya mapato ya ndani zimepatiwa kipaumbele kwenye mgao. Lengo ni kuzisaidia Halmashauri hizo kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Ruzuku ya Serikali Kuu**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 5.48.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 4.32** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zikijumuisha Mishahara **Shilingi trilioni 3.66** na **Shilingi bilioni 650.92** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa maendeleo, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi trilioni 1.16** ambazo zinajumuisha fedha za ndani **Shilingi bilioni 669.55** na **Shilingi bilioni 492.48** fedha za nje. Hadi Februari 2020, jumla ya **Shilingi trilioni 3.36** sawa na **asilimia 61** zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Shilingi trilioni 2.87** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 494.96** ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

**Matumizi**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizopokelewa na kukusanywa zimetumika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia misingi ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019; ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na elimu katika Shule za Msingi na Sekondari; Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada, ujenzi wa majengo ya utawala na makazi ya viongozi kwenye Mikoa, Wilaya, Tarafa na Halmashauri; kuratibu na kusimamia utekelezaji wa majukumu kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; uwezeshaji wananchi kiuchumi; uboreshaji mazingira ya biashara na uwekezaji; usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha, huduma za utawala, ujenzi wa miundombinu ya barabara, na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Taasisi.

**Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019**

25. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu na kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019 kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288 kwa mafanikio makubwa. Uchaguzi wa mwaka 2019 ni wa sita (6) tangu ulipofanyika kwa mara ya kwanza chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1994.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali la maeneo ya utawala Na. 536 na 537, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulihusisha Mitaa **4,263,** Vijiji **12,319** na Vitongoji **64,384.** Uchaguzi huo ulihusisha Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji, Wajumbe wa Serikali za Vijiji na Wajumbe wa Kamati za Mitaa. Katika uchaguzi huo, Chama cha Mapinduzi kilipata ushindi kwa wastani wa **asilimia 99.9** kwa nafasi zote zilizoshindaniwa yaani za Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliowezesha na kufanikisha uchaguzi kufanyika kwa usalama na amani wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia (AZAKI) na Taasisi za Serikali. Kazi iliyobaki ni kuendelea kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kutimiza azma ya kuwaletea wananchi maendeleo wanayotarajia.

**Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kukuza ajira na kipato kwa wananchi. Hadi Februari 2020, mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 25.38** sawa na **asilimia 31.3** ya malengo ya mwaka wa fedha 2019/20 ilikuwa imetolewa kati ya lengo la kutoa mikopo ya **Shilingi bilioni 62.2**. Mikopo hiyo ilitolewa kutokana na **asilimia 10** ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 12.92** zimetolewa kwa vikundi **8,207** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 9.54** zimetolewa kwa vikundi **4,266** vya Vijana na **Shilingi bilioni 2.91** zimetolewa kwa vikundi **915** vya Watu Wenye Ulemavu. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya **Shilingi bilioni 9.39** zilirejeshwa kutoka kwenye mikopo ya vikundi **10,530**.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka zaidi ya minne kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020, Serikali imefanikiwa kutoa mikopo ya jumla ya **Shilingi bilioni 93.3** ambayo imenufaisha vikundi **32,553** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya mikopo hiyo, **Shilingi bilioni 54.08** zilitolewa kwa vikundi **20,542** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 34.98** zilitolewa kwa vikundi **10,741** vya Vijana na **Shilingi bilioni 4.24** zilitolewa kwa vikundi **1,270** vya Watu Wenye Ulemavu. Mikopo hiyo imechangia kukuza uwekezaji mdogo na mkubwa na kuongeza kipato cha wananchi.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** mikopo hiyo imewekezwa kwenye viwanda vidogo, kilimo na ufugaji wa kisasa, biashara, utunzaji wa mazingira, huduma za kifedha na huduma za usafiri. Baadhi ya Vikundi vimeanza kuwekeza katika miradi mikubwa yenye tija ya kuongeza kipato na ajira ikiwemo mradi wa kuwezesha Wajasiriamali katika Halmashauri ya Mji Kahama ambapo ekari 500 zimetengwa na kuendelezwa. Mradi huo umewezesha utoaji wa mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.29** kwa vikundi 403 vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu vinavyoendesha shughuli zao katika kituo kimoja cha Zongomela ambapo ajira 1,692 zimezalishwa; mradi wa Vijana wa kike wa ushonaji nguo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga wenye gharama ya **Shilingi milioni 100** na wanufaika **30**, mradi wa kilimo cha mboga mboga katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala wenye uwekezaji wa **Shilingi milioni 150,** mradi wa kuzalisha sabuni *(Mafinga Soap)* ambao umewekeza zaidi ya **Shilingi milioni 70** katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, mradi wa kiwanda cha kuchakata kokoto katika Halmashauri ya Mji wa Makambako wenye uwekezaji wa zaidi ya **Shilingi milioni 45**, mradi wa ununuzi wa mashine ya kuchanganya malighafi wenye uwekezaji wa **Shilingi milioni 30.0** katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, mradi wa kiwanda cha uchomeleaji cha *Five Youth Innovators* katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wenye mtaji wa **Shilingi milioni 20** na mradi wa usafirishaji katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke uliogharimu **Shilingi milioni 229.**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilifanikiwa kufuta malimbikizo ya fedha za mikopo ya miaka ya nyuma yaliyotokana na uwezeshaji wa **asilimia 10** ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa vikundi vya Wanawake na Vijana kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Malimbikizo yaliyofutwa yalitokana na fedha ambazo Halmashauri hazikuchangia kabla ya kutungwa kwa Sheria ya kusimamia mikopo hiyo.

**Maeneo ya Uwekezaji**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (BLUEPRINT) ambao lengo lake ni kuhakikisha vikwazo na kero mbalimbali za biashara na uwekezaji zinaondolewa ili kurahisisha mazingira ya kufanyia biashara. Hadi Februari 2020, tozo mbalimbali zimeondolewa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo ushuru wa huduma kwa biashara za nyumba za kulala wageni, ushuru wa mabango yanayoelekeza mahali huduma inapopatikana, ushuru kwa wafanyabiashara wadogo, marekebisho ya ushuru wa mazao kati ya asilimia 3 hadi 5 wa awali hadi asilimia 3 kwa mazao ya biashara na chakula yasiyopungua tani moja (1). Tozo na ushuru huo umeondolewa kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2017. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ili kuondoa kodi zenye kero zinazokwamisha ufanyaji wa biashara na uwekezaji zikiwemo tozo zinazotozwa na Taasisi zaidi ya moja.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya hekta **854,821.59** zimetengwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya uwekezaji zikiwemo hekta **403,784.92** kwa ajili ya viwanda vikubwa, vidogo na vya kati. Aidha, hekta **45,231.33** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa masoko, minada, hoteli, ujenzi wa stendi za mabasi, maduka na biashara. Vilevile, hekta **405,805.34** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika sekta za kilimo, misitu, ufugaji, umwagiliaji, madini na gesi. Hivyo, wadau mbalimbali wanahamasishwa kutumia fursa hiyo ya uwekezaji.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kaulimbiu ya ***Mkoa Wetu, Viwanda Vyetu,*** iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/18, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia na kutoa hamasa kwa wadau na wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika mkakati wa ujenzi wa viwanda ili kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Hadi Februari 2020, viwanda **4,876** vimeanzishwa na kuvuka lengo la kuanzisha viwanda **2,600** lililowekwa sawa na viwanda **100** katika kila Mkoa kwa Mikoa yote **26** Tanzania Bara. Kati ya viwanda hivyo, viwanda vikubwa ni **108**, viwanda vya kati ni **236**, viwanda vidogo **2,522** na viwanda vidogo sana **2,010.**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Mikoa **8** ya Tabora, Ruvuma, Simiyu, Mtwara, Geita, Songwe, Morogoro na Dodoma imefanikiwa kuandaa wasifu wa kiuchumi *(Regional Economic Profile)* ili kubainisha fursa za kiuchumi na uwekezaji. Mikoa hiyo iliandaa makongamano ya uwekezaji yaliyotumika kuwatangazia wadau fursa za uwekezaji zinazopatikana katika Mikoa hiyo ili waweze kuzitumia. Hivyo, nawahamasisha wadau mbalimbali watumie fursa hiyo ili kuwekeza katika miradi itakayochangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, wafanyabiashara wadogo **1,551,126** wamepatiwa vitambulisho ambavyo vimewezesha kukusanywa kwa **Shilingi bilioni 31.02** katika Mikoa yote **26.** Lengo la azma hii ni kuwatambua wafanyabiashara wadogo na kuwawekea mazingira rafiki ya ufanyaji biashara. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa Kanuni za kusimamia wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo ili kutambua mchango wa biashara hizo katika ukuaji wa uchumi.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi ulioanza kutekelezwa mwaka 2018 kwenye Halmashauri 184 Tanzania Bara. Mwongozo umesaidia kupunguza muda wa kushughulikia kibali cha ujenzi kutoka wastani wa siku **180** hadi wastani wa siku **7**. Hadi Februari 2020, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa zimetoa vibali **11,737** vya ujenzi ikilinganishwa na vibali **2,425** vya ujenzi vilivyotolewa hadi Februari 2019.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio hayo yametokana na uwepo wa Kamati ya pamoja ya wataalam inayoshughulikia utoaji wa vibali katika Halmashauri. Hadi Februari 2020, Halmashauri

# HOTUBA YA OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

zimekusanya ada ya vibali vya ujenzi jumla ya **Shilingi bilioni 3.20** sawa na **asilimia 57** kati ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 5.64.** Ufanisi katika utoaji wa vibali vya ujenzi umesaidia kuboresha mazingira ya uwekezaji kutokana na kuondolewa kwa urasimu na kupungua kwa muda uliokuwa unatumika awali kutoa vibali vya ujenzi.

**Miradi ya Kimkakati**

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi ya kimkakati inajenga dhana ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kujitegemea na kupunguza utegemezi kutoka katika ruzuku ya Serikali Kuu na Wadau wa Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2019/20, ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 70** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi **38** ya Kimkakati. Hadi Februari 2020, **Shilingi bilioni 25.36** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 36.24** ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi **13** katika Halmashauri **11** za Wilaya za Ruangwa, Chato, Kakonko na Nanyumbu; Halmashauri za Manispaa za Ilemela, Ubungo, Kinondoni, Ilala, Moshi; Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam; na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Aidha, miradi mingine **9** ya kimkakati inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri **8** za Wilaya za Maswa, Momba, Songwe, Kakonko, Buhigwe, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Halmashauri ya Mji wa Tunduma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 22.41** kwa kutumia fedha za bakaa ya mwaka wa fedha 2018/19.

**Usimamizi wa Watumishi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya watumishi **7,280** wameajiriwa katika ajira za kudumu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya hao, walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walikuwa **4,945,** watumishi wa kada za afya walikuwa **765** na Watendaji wa Kata walikuwa **1,570.** Ajira hizo zinafanya watumishi walioajiriwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia **28,673** katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 wakiwemo walimu **18,181,** watumishi wa afya **8,922** na Watendaji wa Kata **1,570**. Ajira hizo zimesaidia kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, nafasi **88** za Wakuu wa Idara na Vitengo zilizokuwa zinakaimiwa zimejazwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ili kuboresha utendaji na uwajibikaji.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne kuanzia Novemba, 2015 hadi Februari 2020, jumla ya ajira **2,347,334** za mikataba/muda zimezalishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekta zilizoongoza kwa kuzalisha ajira nyingi ni uwezeshaji wananchi kiuchumi **(ajira 1,551,126),** ujenzi wa miundombinu ya barabara mijini na vijijini **(ajira 729,160),** elimu **(ajira 53,578),** afya **(ajira 12,820)** na ujenzi wa majengo ya utawala ya Mikoa na Halmashauri **(ajira 650).** Watanzania wamenufaika na ajira hizo kupitia utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi na matumizi ya utaratibu wa *Force Account* katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Kuzijengea Uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, mafunzo ya kuboresha utendaji yametolewa kwa watumishi **880** katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Kilimanjaro, Manyara, Dar es Salaam, Pwani, Iringa, Mbeya, Njombe, Katavi, Ruvuma, Lindi, Mtwara na Rukwa kuhusu Mfumo wa Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi wa Watumishi wa Umma (OPRAS). Mafunzo hayo yamesaidia kuimarisha utendaji na ufanisi katika utekelezaji wa kazi za Serikali. Aidha, mafunzo mengine yametolewa kwa Kamati za Kudhibiti Uadilifu katika Halmashauri **185** ili kuimarisha weledi na kupunguza viashiria vya rushwa katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Vilevile, Wakurugenzi, Maafisa Utumishi na Wakaguzi wa Ndani kutoka Halmashauri **185** wamepatiwa mafunzo ya uongozi na usimamizi wa rasilimaliwatu na fedha ili kuimarisha shughuli za kiutumishi na mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, wahudumu wa afya **2,689** kutoka Mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro na Rukwa wamepatiwa mafunzo kuhusu masuala ya lishe. Aidha, Maafisa Ugani **297** na wakulima wadogo **1,761** wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji wa mboga mboga na matunda kupitia mashamba darasa yapatayo **111** yaliyoanzishwa Vilevile, wakulima na wafugaji **71,091** wamepatiwa mafunzo kuhusu kilimo bora na ufugaji endelevu ili kuongeza tija ya uzalishaji na kudhibiti migogoro inayotokana na mwingiliano katika matumizi ya ardhi.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, Maafisa Ustawi wa Jamii **711** wamejengewa uwezo wa namna ya kushughulikia mashauri ya watoto wanaokinzana na Sheria na waliofanyiwa vitendo vya ukatili. Aidha, makabati **1,500** yamenunuliwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 765.23** na kusambazwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuimarisha utunzaji wa nyaraka za huduma za ustawi wa jamii. Lengo ni kuwawezesha Maafisa hao kusimamia haki za watoto na kuelimisha jamii kushiriki katika kuwalinda watoto na kuwapa haki yao kikatiba ya kupata elimu.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya walimu **31,824** sawa na **asilimia 98** kati ya walimu **32,314** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu za ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika Shule za Msingi hususan Darasa la Kwanza na Darasa la Nne. Aidha, walimu **14,275** wa Shule za Sekondari sawa na **asilimia 77** ya walimu **18,540** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu za ufundishaji wa masomo ya Lugha, Hisabati na Elimu ya Viumbe. Vilevile, walimu **1,500** wamepatiwa mafunzo ya namna ya kutumia Kompyuta na kufanya matengenezo madogo ya vifaa vya TEHAMA.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya magari **155,** yamenunuliwa kwa ajili ya Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya magari hayo, magari **15** yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa, magari manne **(4)** kwa Makatibu Tawala wa Mikoa, magari **26** kwa Makatibu Tawala Wasaidizi (Elimu), magari **24** kwa Wakuu wa Wilaya, magari **55** kwa Makatibu Tawala wa Wilaya na magari **13** yamenunuliwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri. Aidha, magari **20** yamenunuliwa kupitia Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya usimamizi wa taka na kuhudumia dampo na gari moja **(1)** limenunuliwa kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya pikipiki **484** zimenunuliwa ambapo pikipiki **448** zimetolewa kwa ajili ya Maafisa Tarafa, pikipiki **20** zimetolewa kwa ajili ya Maafisa Ugani wa kilimo na pikipiki **16** zimetolewa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii. Aidha, baiskeli **2,689** zimetolewa kwa Maafisa Ustawi wa Jamii zikiwemo jaketi **2,805** zinazoakisi mwanga kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shughuli za lishe kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Ushughulikiaji wa Malalamiko ya Wananchi**

49. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha na kusimamia madawati ya malalamiko katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2020, malalamiko **317** kutoka kwa wananchi na wadau mbalimbali yalikuwa yamepokelewa na kushughulikiwa. Malalamiko hayo yameshughulikiwa kupitia Kamati zilizoundwa kila Mkoa na Halmashauri kwa usimamizi wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri. Aidha, ziara za Viongozi wa Kitaifa, Mikoa na Wilaya zimetumika kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi. Utaratibu huu ni utekelezaji wa Ibara ya 8 (1)(C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayoelekeza Serikali kuwajibika kwa wananchi.

**Usimamizi wa Fedha Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa fedha kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; na Kanuni zake pamoja na miongozo mingine ya Serikali. Lengo ni kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ili kuhakikisha kazi zinazotekelezwa zinalingana na thamani ya fedha iliyotumika *(Value for Money).*

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamia matumizi ya fedha za Serikali kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Fedha za Umma wa *Epicor* ambao umeunganishwa kwenye Halmashauri zote **185** ili kuleta uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika matumizi ya fedha za umma. Kwa sasa mfumo wa *Epicor* umeunganishwa na Mfumo wa Mipango na Utoaji Taarifa *(PlanRep)* ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa ya mapato na matumizi.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI pia imefanikiwa kuandaa Mwongozo wa Uhasibu na Usimamizi wa Mapato ambao umesambazwa kwenye Halmashauri zote **185.** Hadi Februari 2020, Waweka Hazina na Wahasibu **370** wamepatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya miongozo hiyo pamoja na ufungaji wa hesabu za mwisho za Halmashauri. Sambamba na utoaji wa miongozo, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unaofanywa kwa pamoja kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na wataalam umesaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha usimamizi wa fedha za umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 usimamizi wa fedha za umma umeimarika kutokana na kuongezeka kwa Halmashauri zinazopata Hati zinazoridhisha kutoka **asilimia 81** mwaka wa fedha 2015/16 hadi **asilimia 95** kwa mwaka wa fedha 2018/19, Hati zenye mashaka zimepungua kutoka **asilimia 19** katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi **asilimia 5** katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2018/19.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua za kinidhamu zimeendelea kuchukuliwa kwa watumishi wanaokiuka Sheria na Kanuni za utumishi wa umma. Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020, jumla ya watumishi **26** wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu. Hatua hizo zimechukuliwa kwa lengo la kuimarisha maadili na nidhamu ya watumishi katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

**Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Viongozi**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekamilisha ujenzi wa Ofisi katika eneo la Mji wa Serikali-Mtumba. Mradi umetekelezwa kwa utaratibu wa *Forcé Account* na kupunguza gharama za mradi kutoka wastani wa **Shilingi bilioni 3.6** endapo Makandarasi wangetumika kutekeleza mradi hadi **Shilingi bilioni 1.5.** Viongozi Wakuu wote sita **(6)** wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI wamepata mahali pa kufanyia kazi pamoja na Wakurugenzi na watumishi wengine wapatao **100.**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile katika mwaka wa fedha 2019/20, TARURA imekamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya TARURA Makao Makuu katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.1** kwa kutumia utaratibu wa *Force Account* katika kiwanja chenye ukubwa wa **ekari 3.** Kukamilika kwa Ofisi hizo kutaiwezesha TARURA kuokoa jumla ya **Shilingi milioni 552.64** kwa mwaka zilizokuwa zinatumika kama kodi ya pango. Aidha, watumishi wa TARURA watakuwa na mazingira yaliyoboreshwa ya kufanyia kazi.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Songwe na Njombe na Ofisi za Wakuu wa Wilaya za Kigamboni na Nyamagana zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Aidha, Ofisi **48** za Tarafa zimejengwa katika Mikoa ya Mtwara (**5**), Shinyanga (**14**), Kigoma (**5**) na Tanga (**24**). Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hiyo kutawezesha Mikoa na Wilaya hizo kuwa na Ofisi kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na wadau mbalimbali.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, nyumba nne **(4)** za Wakuu wa Mikoa zimejengwa katika Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Songwe na Njombe. Aidha, nyumba tatu **(3)** za Makatibu Tawala wa Mikoa zimejengwa katika Mikoa ya Simiyu, Songwe na Njombe. Vilevile, nyumba tatu **(3)** za Wakuu wa Wilaya zimejengwa katika Wilaya ya Malinyi, Gairo na Momba. Kadhalika nyumba **21** za Maafisa Waandamizi zimejengwa katika Mikoa ya Simiyu (nyumba **7**), Singida (nyumba **2**), Katavi (nyumba **10**) na Songwe (nyumba **2**).

59. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Ofisi na nyumba hizo za viongozi ambao umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 4.18** umewezesha viongozi na watumishi wa Tawala za Mikoa kuwa na mahali pa kuishi na kufanyia kazi katika kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Halmashauri **10** za Wilaya za Mpanda, Wanging'ombe, Kibaha, Magu, Itigi, Pangani, Bumbuli, Ruangwa na Halmashauri za Miji za Tarime na Mbinga zilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 3.76** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa majengo ya utawala. Aidha, jumla ya Halmashauri **21** ziliendelea na ukamilishaji wa majengo ya utawala kwa kutumia bakaa ya mwaka wa fedha 2018/19 zikiwemo Halmashauri za Wilaya za Buchosa, Busokelo, Chalinze, Handeni, Kibiti, Madaba, Malinyi, Mbulu, Misungwi, Mpimbwe na Songwe; Halmashauri za Miji za Bunda, Ifakara, Kasulu, Kondoa, Mafinga, Nanyamba, Newala na Nzega na Halmashauri za Manispaa za Kigamboni na Ubungo.

**Huduma za Afya ya Msingi**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za afya ya msingi ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa maisha ya watu kwa kuiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka kipaumbele katika uboreshaji wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya kwa kuweka mkazo katika kuimarisha afya ya mama na mtoto, kudhibiti magonjwa sugu kama vile Malaria, UKIMWI, Kifua Kikuu na magonjwa yasiyoambukiza ambayo ndiyo chanzo kikuu cha vifo na kuchukua hatua za kutatua tatizo la uhaba wa miundombinu na watumishi wa sekta ya afya.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kusimamia ujenzi wa Hospitali za Halmashauri **71** na kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **27** za Halmashauri. Ujenzi huo utakapokamilika utawezesha kuwa na Hospitali mpya **98** za Halmashauri ambazo zimejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 155.45**. Ujenzi huu umefanyika sambamba na ukarabati wa Hospitali **13** za Halmashauri uliogharimu **Shilingi bilioni 5.4.**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi huo utakapokamilika utaongeza idadi ya Hospitali za Halmashauri kutoka Hospitali **77** zilizokuwepo mwaka 2015 hadi Hospitali **175** kufikia Juni, 2020. Uboreshaji wa Hospitali za Halmashauri umesaidia kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi na kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Mikoa.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali inaendelea na ujenzi wa Vituo vya Afya **81.** Kati ya vituo hivyo, vituo **52** vinaendelea kujengwa na Serikali kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10.4** ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.2)*** na vituo **29** vinaendelea kujengwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa gharama ya **Shilingi bilioni 12.4**.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, idadi ya Vituo vya Afya vya Serikali imeongezeka kutoka **535** mwaka 2015 hadi **968** Februari 2020. Hivyo, katika kipindi hicho cha miaka minne Serikali imefanikiwa kujenga na kukarabati Vituo vya Afya **433.** Mpango huo umesogeza huduma karibu zaidi kwa wananchi na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga hususan maeneo ya vijijini.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Zahanati zilizojengwa na kukarabatiwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni **38** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 5.40.** Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano, Zahanati za Serikali zimeongezeka kutoka Zahanati **4,554** za Serikali mwaka 2015 hadi Zahanati **4,922** hadi Februari, 2020. Mkakati wa uboreshaji wa Zahanati umesaidia kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi na kuwapunguzia wagonjwa umbali mrefu kufuata huduma.

**Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya unafanyika sambamba na kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka **asilimia 30** mwaka 2015 hadi **asilimia 92** hadi Februari, 2020. Ufanisi huo umechangiwa na matumizi ya Mfumo wa Mshitiri *(Prime Vendor System)* katika Mikoa **26** ya Tanzania Bara ikiwa ni utaratibu wa kuondoa upungufu wa dawa pale unapotokea katika Bohari ya Taifa ya Dawa (MSD). Utaratibu wa mshitiri umewezesha vituo vya kutolea huduma za afya vya Serikali kununua dawa na vifaa tiba kutoka wauzaji binafsi walioteuliwa katika kila Mkoa pale inapothibitika dawa hizo kukosekana MSD. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 53.11** zinazojumuisha **Shilingi bilioni 27.11** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba na **Shilingi bilioni 26** kwa ajili ya ununuzi wa dawa muhimu.

**Afya na Usafi wa Mazingira**

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Afya na Usafi wa Mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Lengo la mpango huu ni kuikinga jamii na magonjwa ya mlipuko ya kipindupindu, kuhara, kuhara damu, minyoo, kichocho, matende, trakoma na Polio. Hadi Februari 2020, idadi ya Kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka **asilimia 51** hadi **asilimia 62** na Kaya zisizokuwa na vyoo zimepungua kutoka **asilimia 2.6** hadi **asilimia 1.9** katika kipindi hicho**.** Mikoa iliyofanya vizuri katika utekelezaji wa Kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira ni Njombe, Kilimanjaro, Iringa, Katavi na Dodoma. Serikali imetumia jumla ya **Shilingi milioni 350.0** kwa ajili ya kuboresha afya na usafi wa mazingira kupitia Mpango wa Maji na Usafi wa Mazingira.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio haya yamechangia kupunguza magonjwa ya milipuko kama Kipindupindu ambapo kutoka Julai, 2019 hadi Februari, 2020 hakuna Halmashauri yoyote iliyoripoti kuwa na mlipuko wa Kipindupindu. Aidha, idadi ya wagonjwa wa kuhara imepungua kutoka wagonjwa **4,550** waliokuwepo Julai 2019 hadi wagonjwa **2,037** kufikia Februari 2020, kichocho kimepungua kutoka wagonjwa **4,112** hadi wagonjwa **2,204** na homa ya matumbo (Typhoid) imepungua kutoka wagonjwa **21,291** hadi wagonjwa **11,368.**

**Huduma za Chanjo**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na wadau wengine iliendesha kampeni ya utoaji wa chanjo ya Surua na Rubella iliyofanyika Oktoba, 2019 ambayo imegharimu **Shilingi bilioni 8.93** na kuwafikia watoto **4,410,095** sawa na asilimia **113** ya watoto **3,920,040** waliolengwa. Kampeni hii ni moja ya mkakati wa kuwakinga watoto wenye umri chini ya miaka mitano dhidi ya magonjwa ya Rubella na Surua.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI vilevile imeendelea kutoa huduma za chanjo nyingine kwa kufuata utaratibu wa huduma tembezi, mkoba na kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari 2020, jumla ya watoto **8,663,356** wenye umri kati ya miezi **9** hadi **59** walipatiwa chanjo kati ya lengo la watoto **8,082,838** sawa na asilimia **107.1.** Chanjo hizi hutolewa ili kuwalinda watoto wasipatwe na magonjwa nyemelezi yakiwemo nimonia, ngozi, macho na masikio ambayo yasipodhibitiwa mapema huchangia udumavu na vifo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

**Udhibiti wa Magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria, Serikali imetoa mgao wa viuadudu vya kibailojia **lita 96,000** zenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.26** na kusambazwa kwenye Mikoa yenye maambukizi makubwa ya malaria ambayo ni Kagera **(Lita 12,308),** Mtwara **(lita 11,536),** Dar es Salaam **(lita 11,400),** Lindi **(lita 9,048),** Geita **(lita 8,092**), Kigoma **(lita 7,616**). Aidha, Mikoa iliyokuwa na maambukizi ya ugonjwa wa Dengue ilipewa kipaumbele na kupatiwa dawa za kudhibiti ugonjwa wa Dengue ikiwemo Mikoa ya Tanga **(lita 7,040),** Mwanza **(lita 6,640),** Morogoro **(lita 6,240)**, Dodoma **(lita 5,960),** Ruvuma **(lita 5,320)** na Tabora **(lita 4,800).** Mkakati huu umesaidia kudhibiti mazalia ya mbu wanaosababisha magonjwa ya Malaria na Dengue.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mingine iliyotekelezwa ni pamoja na kugawa vyandarua **5,681,712** vyenye dawa kwa mama wajawazito waliohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza na watoto wenye umri wa miezi **9** walioandikishwa na kupatiwa chanjo ya Surua Rubella katika vituo vya kutolea huduma za afya. Utekelezaji wa mikakati hiyo umepunguza kiwango cha maambukizi ya malaria Tanzania Bara kutoka **asilimia 14** mwaka 2015 hadi **asilimia 7.3** mwaka 2020. Aidha, vyandarua vingine **7,095,565** vinategemewa kusambazwa katika Mikoa 10 ya Dodoma **(1,508,754),** Tanga **(1,336,926),** Mbeya **(1,124,024),** Rukwa **(719,254)**, Singida **(695,188),** Iringa **(573,400),** Songwe **(412,264),** Manyara **(304,673),** Kilimanjaro **(298,665)** na Njombe **(123,417)** kabla Juni, 2020**.** Mikoa hiyo imepewa kipaumbele kutokana na kuwa na vyandarua chini ya asilimia **85** ya mahitaji.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutekeleza malengo ya kimkakati ya kudhibiti UKIMWI ya **asilimia 90** ya wanaoishi na UKIMWI wawe wanafahamu hali zao, **asilimia 90** ya watu wanaofahamu hali zao wapate dawa za kufubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (ARV) na **asilimia 90** ya wanaotumia ARV kutoambukiza wengine ifikapo mwaka 2020. Hadi Februari, 2020 Tanzania imefanikiwa kufikia **asilimia 77** ya lengo la kwanza, **asilimia 98** ya waliopima UKIMWI wanatumia dawa (ARVs) na **asilimia 91** wamefubaza virusi vya UKIMWI. Lengo la Mpango huu unaosimamiwa na Umoja wa Mataifa ni kuhakikisha maambukizi mapya ya UKIMWI yanadhibitiwa na watu wanaoishi na maambukizi wanapatiwa huduma ili kuzuia maambukizi mapya.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI) zimeendelea kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI ili kujenga uelewa miongoni mwa jamii kupima ili kutambua hali zao za kiafya na kwa walioambukizwa kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata ushauri wa wataalam na dawa. Aidha, utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na UKIMWI umeboreshwa kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoko katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya. Elimu kuhusu ugonjwa wa UKIMWI imesaidia kupunguza unyanyapaa katika jamii na kuongeza idadi ya wagonjwa wanaojitokeza kupima afya zao. Vilevile, elimu imesaidia kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa Mama kwenda kwa mtoto.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na ugonjwa wa homa ya mapafu unaosababishwa na Virusi vya Corona (COVID - 19), Ofisi ya Rais TAMISEMI imeweza kuainisha na kuviandaa vituo **182** kwa ajili ya kuwatenga na kuwahudumia washukiwa na waliothibitika kuwa na ugonjwa wa Corona. Aidha, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto zimetambuliwa hoteli zinazotumika katika kutenga wageni na wenyeji wanaoingia nchini ili kuzuia kuenea kwa virusi hivyo vya Corona.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imetumia jumla **Shilingi milioni 184.85** kwa ajili ya mafunzo kwa watoa huduma za afya **200** kuhusu utambuzi wa wagonjwa wa Kifua Kikuu. Lengo la Serikali ni kuendelea kuwatambua wagonjwa wenye vimelea vya Kifua Kikuu na kuwapa matibabu kwa kuzingatia miongozo ya tiba ya Kifua Kukuu ili kuzuia maambukizi mapya hapa nchini

**Huduma za Lishe**

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia (AZAKI) inasimamia afua za uboreshaji wa lishe kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kupunguza kiwango cha udumavu. Kwa mujibu wa takwimu zinazotokana na Utafiti wa Lishe wa Taifa wa mwaka 2018 hali ya udumavu imepungua kutoka **asilimia 34** hadi **asilimia 31.8** kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutatua changamoto hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeongeza rasilimali fedha za kutekeleza afua za lishe kutoka **Shilingi bilioni 15** kwa mwaka wa fedha

# HOTUBA YA OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

2018/19 hadi **Shilingi bilioni 16.8** kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, Ofisi yangu imeendelea kusaini mikataba ya utendaji na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kila mwaka kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika kutekeleza shughuli za lishe.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza mkakati unaohakikisha wananchi wanatumia chumvi iliyowekewa madini joto. Jumla ya mashine **70** za kupima chumvi zimesambazwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar katika Wilaya ya Wete na Chakechake. Mashine hizo zimenunuliwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 97.24** sawa na wastani wa **Shilingi 1,389,200** kwa kila mashine. Vilevile, Serikali imesambaza vifaa vya kupimia chumvi *(Rapid Test Kits)* ambapo kiasi cha boksi **124** zenye vifaa **62,000** vimesambazwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini.

**Huduma za Watu Wenye Ulemavu**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Watu Wenye Ulemavu wapatao **10,035** wametambuliwa ambapo wanawake ni **6,100** na wanaume **3,935;** Watu Wenye Ualbino ni **2,400** wanawake **1,300** na wanaume **1,100**; Watu Wenye Ulemavu wa Viungo ni **5,233** wanawake **3,133** na wanaume **2,100;** Wasioona ni **510** Wanawake **203** na Wanaume **307**; Viziwi ni **1,500** wanawake **785** wanaume **715;** na Wenye Ulemavu wa Akili ni **392** wanawake **281** wanaume **111.** Watu hao Wenye Ulemavu wamepatiwa vifaa kama miwani, miamvuli, mafuta ya ngozi, fimbo nyeupe na baiskeli za miguu mitatu ili kuwawezesha kujimudu. Aidha, Kamati **5,024** za Watu Wenye Ulemavu zimeundwa katika Vijiji na Kamati **2,284** katika Mitaa. Lengo la Kamati hizo ni kusimamia masuala ya Watu Wenye Ulemavu na kusaidia kutatua changamoto zinazowakabili katika maeneo yao.

**Huduma za Ustawi wa Jamii**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha huduma na haki kwa makundi maalum, hadi Februari 2020, Serikali imefanikiwa kuwatambua jumla ya watoto **2,398,354** walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 2.31** kwa kuwapatia huduma mbalimbali ikiwemo ujuzi kupitia vyuo vya VETA, chakula, ada, vifaa vya shule, mavazi, huduma za msaada wa kisaikolojia na kuwaunganisha na familia zao.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya mashauri **22,060** ya watoto waliofanyiwa ukatili na watoto **3,892** wanaokinzana na Sheria yamepokelewa na kushughulikiwa ambapo kati ya hayo mashauri **13,342** yametolewa hukumu. Aidha, jumla ya watoto **25,979** waliofanyiwa vitendo vya ukatili na watoto wanaokinzana na Sheria walipatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii na kuunganishwa na familia zao. Vilevile, Kamati za Ulinzi na Usalama wa mwanamke na watoto zimeundwa katika Halmashauri.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wazee **1,540,435** pia wametambuliwa na kati yao, Wazee **856,052** sawa na **asilimia 55.6** wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bila malipo na Wazee **684,383** sawa na **asilimia 44.4** wamepatiwa kadi za bima ya afya. Aidha, jumla ya mabaraza **171,655** ya Ushauri ya Wazee yameundwa kwa ajili ya usimamizi wa masuala ya wazee katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, jumla ya watu **4,338,752** wamepatiwa msamaha wa matibabu kutoka makundi mengine ambapo kati yao wanaume ni **1,424,891** na wanawake ni **2,913,861.** Jumla ya **Shilingi bilioni 6.33** zimetumika kugharamia matibabu bila malipo kwa makundi maalum yanayohusisha wazee wenye umri wa miaka zaidi ya **60** na wasio na uwezo, wafungwa, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito, wasiojiweza kiuchumi, watu wenye magonjwa sugu na Watu Wenye Ulemavu.

**Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020 wanachama **milioni 9.6** wameandikishwa sawa na kaya **milioni 1.6** katika Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa katika Mikoa 26. Kaya hizo zimechangia jumla ya **Shilingi bilioni 1.3** kupitia malipo yaliyofanyika kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya. Kati ya fedha hizo, Hospitali za Halmashauri zimekusanya **Shilingi milioni 407.06** na **Shilingi milioni 910.45** zimekusanywa kwenye Vituo vya Afya na Zahanati. Katika kipindi cha miaka minne kuanzia Novemba, 2015 hadi Februari, 2020 jumla ya wanufaika **milioni 28.08** katika Kaya **milioni 6.73** wanatumia kadi za CHF.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,* asilimia 80** ya fedha zinazokusanywa zinatumika kununua dawa, vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Kupitia CHF iliyoboreshwa mapato yote yanakusanywa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki *(Government Electronic Payment Gateway - GePG)* na fedha hizo zinatunzwa katika akaunti iliyoko Benki Kuu.

**Sekta ya Elimu**

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina jukumu la kusimamia utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari nchini. Jukumu hilo linahusisha utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada, uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari. Lengo ni kuwa na jamii iliyoelimika yenye maarifa, uzalendo, ujuzi na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa viwanda uliofungamanishwa na maendeleo ya watu.

**Elimu ya Msingi**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya Shule za Msingi imeongezeka kutoka **16,857** (Shule **15,802** za Serikali na Shule **1,055** za binafsi) mwaka 2016 hadi **17,771** (shule za Serikali **16,155** na shule za binafsi **1,616**) hadi Februari, 2020 sawa na ongezeko la shule **914** katika kipindi cha miaka minne. Idadi ya wanafunzi pia imeongezeka kutoka **10,201,972** mwaka 2016 hadi **12,034,599** mwezi Februari, 2020 katika shule za Serikali na binafsi. Ongezeko la idadi ya wanafunzi linatokana na utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ulioanza kutekelezwa Desemba, 2015.

**Uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Machi 2020, wanafunzi **1,196,278** sawa na **asilimia 86.2** walikuwa wameandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi **1,389,913.** Kati ya hao, wanafunzi **1,018** ni wenye mahitaji maalum ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.3).*** Katika kipindi cha miaka minne uandikishaji wa rika lengwa la watoto wa darasa la Elimu ya Awali umeongezeka kutoka **asilimia 45** mwaka 2015 hadi **asilimia 86.2** mwezi Machi, 2020.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** wanafunzi wa Darasa la Kwanza walioandikishwa hadi Machi, 2020 ni **1,557,453** sawa na **asilimia 97.5** ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi **1,597,612.** Kati ya hao, wanafunzi **2,897** ni wenye mahitaji maalum ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.4).*** Uandikishaji wa rika lengwa la watoto wa Darasa la Kwanza umeongezeka kutoka **asilimia 95** mwaka 2015 hadi **asilimia 97.5** mwezi Machi, 2020.

**Uboreshaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi**

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, vyumba **3,232** vya madarasa vimejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 30.32** katika Shule za Msingi na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa vilivyopo kutoka **122,487** mwaka 2019 hadi **125,719** hadi Februari, 2020. Aidha, vyumba **224** vya madarasa vinaendelea kujengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi na Wadau wa Maendeleo. Ongezeko la vyumba vya madarasa limefanyika sambamba na ongezeko la madawati kutoka madawati **2,994,266** yaliyokuwepo mwaka 2019 hadi madawati **3,052,541** hadi Februari 2020. Miundombinu hiyo ya madarasa na madawati imechangia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa vilivyokuwepo.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi vimeongezeka kutoka **108,504** mwaka 2016 hadi **125,719** mwezi Februari 2020, sawa na ongezeko la **asilimia 13.7**. Ongezeko la vyumba vya madarasa limefanyika sambamba na ongezeko la madawati kutoka madawati **3,024,311** yaliyokuwepo mwaka 2016 hadi madawati **8,095,207** kufikia Februari, 2020. Miundombinu hiyo ya madarasa na madawati imechangia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kupunguza msongamano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa vilivyokuwepo.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya matundu ya vyoo **7,922** yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10.62** katika Shule za Msingi na kuongeza idadi ya matundu ya vyoo yaliyopo kutoka **197,741** hadi **205,663** yakijumuisha vyoo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum na vyumba maalum kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusisitiza umuhimu wa kunawa mikono kwa kutumia vibuyu chirizi na vyanzo vingine vya maji vinavyopatikana. Aidha, matundu ya vyoo **571** yanaendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2020. Ujenzi wa miundombinu ya vyoo umesaidia kuboresha afya na mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kusisitiza umuhimu wa kuwa na vyumba maalum kwa watoto wa kike na usambazaji wa taulo za kike. Aidha, shule zimeelekezwa kutumia sehemu ya fedha ya ruzuku ya uendeshaji wa shule iliyotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa baridi itumike kununua taulo za kike. Vilevile, miundombinu ya shule inayojengwa inazingatia kuwa na chumba maalum cha wasichana ili kuboresha mazingira ya wanafunzi wa kike kupata muda kuhudhuria shule kwa siku zote za masomo.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Serikali imetoa **Shilingi bilioni 9.1** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **364** ya nyumba za walimu yaliyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi katika Shule za Msingi ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.5)*** na kuongeza idadi ya nyumba za walimu zilizopo kutoka nyumba **161,007** mwaka 2015 hadi nyumba **161,371** hadi Februari, 2020. Ujenzi wa nyumba hizo umechangia kuboresha mazingira ya kuishi walimu ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa lengo la kuinua kiwango cha taaluma. Aidha, mabweni matatu **(3)** ya Shule za Msingi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **80** kila moja yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 225** katika Mikoa ya Arusha, Iringa na Tanga kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia ujenzi wa shule nne **(4)** za Msingi katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Mtwara na Kigoma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.82** sawa na **Shilingi milioni 706** kwa kila shule. Aidha, Shule ya Msingi Mwisenge iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imefanyiwa ukarabati mkubwa kwa jumla ya **Shilingi milioni 706.** Shule hizo za mfano zimejengwa na kuwekewa miundombinu yote muhimu ili ziwe mfano wa shule bora zitakazojengwa kila Mkoa kwa lengo la kuboresha mazingira ya shule.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya vituo shikizi **164** kati ya vituo **251** vimesajiliwa kuwa Shule za Msingi baada ya kukidhi vigezo. Vituo hivyo vilijengwa ili kuwaondolea wanafunzi kero ya kutembea umbali mrefu katika maeneo ambayo Vijiji viko mbali na shule.

**Mtihani wa Upimaji wa Darasa la Nne na Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba**

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **1,531,120** sawa na **asilimia 91.9** walifaulu Mtihani wa Upimaji wa Taifa wa Darasa la Nne kati ya wanafunzi **1,665,863** waliofanya mtihani huo. Aidha, wanafunzi **759,737** sawa na asilimia **81.5** walifaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba uliofanyika Septemba 2019, kati ya wanafunzi **933,369** waliofanya mtihani huo. Ufaulu wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba umeongezeka kutoka **asilimia 57** mwaka 2015 hadi **asilimia 81.5** mwaka 2019. Ongezeko la ufaulu limetokana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano za kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

**Elimu ya Sekondari**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka **4,773** (shule za Serikali **3,601** na shule za binafsi **1,172**) mwaka 2016 hadi shule **5,001** (shule za Serikali **3,742** na shule za binafsi **1,259**) hadi Februari 2020. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la shule **228** katika kipindi cha miaka minne. Aidha, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka **1,806,955** mwaka 2016 hadi **2,023,457** hadi Februari 2020. Ongezeko la Shule za Sekondari limetoa fursa zaidi kwa wanafunzi wote wanaofaulu kuchaguliwa kujiunga na elimu ya Sekondari.

**Usajili wa Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza**

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya wanafunzi **759,737** sawa na **asilimia 100** ya waliofaulu walichaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza Januari, 2020. Kati ya hao, wanafunzi **666,206** sawa na **asilimia 87.7** wameripoti katika shule walizopangiwa. Kati ya wanafunzi walioripoti shuleni, wanafunzi wenye mahitaji maalum ni **1,341** ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 6).*** Idadi ya wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza imeongezeka kutoka **asilimia 60** ya waliofaulu mwaka 2015 hadi **asilimia 87.7** kufikia Machi 2020.

**Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Shule za Sekondari**

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Sekondari ili kuwezesha wanafunzi waliochaguliwa kuendelea na masomo. Hadi Februari 2020, vyumba vya madarasa **2,593** vilikuwa vimejengwa na kukarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 27.73** katika mwaka wa fedha 2019/20. Idadi hiyo inajumuisha vyumba vya madarasa **273** vilivyojengwa kuanzia Desemba, 2019 hadi Februari, 2020 ili kuwawezesha wanafunzi **58,699** waliokosa nafasi ya kujiunga na Kidato cha Kwanza kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa kupata nafasi. Aidha, vyumba vingine **1,089** vya madarasa vinaendelea kukamilishwa.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya matundu ya vyoo **2,601** yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.87** na mabweni **253** yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **80** kila moja yamejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 8.22.** Kazi nyingine zilizotekelezwa ni ujenzi wa nyumba za walimu **153,** ujenzi wa majengo ya utawala **64** na ujenzi wa Daharia (Hosteli) (**55** zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 kila moja ambapo miradi hiyo imegharimu **Shilingi bilioni 10.96.**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, ukamilishaji wa vyumba vya maabara za masomo ya sayansi **227** umefanyika kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.63**. Ujenzi huo, umeongeza idadi ya vyumba vya maabara kutoka **4,237** mwaka 2015 hadi **4,464** hadi Februari 2020, sawa na ongezeko la vyumba vya maabara **227.** Aidha, Shule **1,258** za Sekondari ambazo zimekamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara zimepatiwa vifaa vilivyogharimu **Shilingi bilioni 3.13** kwa ajili ya masomo ya Baiolojia, Fizikia na Kemia. Ujenzi wa vyumba vya Maabara na usambazaji wa vifaa vya maabara umewezesha wanafunzi wa Shule za Sekondari kusoma kwa vitendo masomo ya sayansi.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shule za Sekondari Kongwe **9** zinaendelea kukarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.71** ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 7).*** Aidha, katika kipindi cha miaka minne jumla ya Shule za Sekondari Kongwe **73** zimekarabatiwa kati ya shule **89** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 84.3** hadi Februari 2020. Ukarabati huo umefanyika kwa kuboresha miundombinu iliyokuwepo na kuongeza miundombinu mipya ili kuzirejesha katika hali ya awali. Ukarabati wa Shule za Sekondari Kongwe umesaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia pamoja na idadi ya wanafunzi.

**Mtihani wa Upimaji wa Kidato cha Pili na Mtihani wa Taifa Kidato cha Nne na Sita**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **514,251** walifaulu kati ya wanafunzi **571,137** waliofanya mtihani huo sawa na **asilimia 90.04.** Aidha, wanafunzi **340,914** kati ya wanafunzi **422,722** waliofanya mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne sawa na **asilimia 80.65.** Katika kipindi cha miaka minne, ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha Nne umeongezeka kutoka **asilimia 69.8** mwaka 2015 hadi **asilimia 80.65** mwaka 2019.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Kidato cha Sita katika mwaka 2019, jumla ya wanafunzi **78,666** sawa na **asilimia 98.6** ya wanafunzi **79,770** waliofanya Mtihani huo walifaulu ikilinganishwa na wanafunzi **34,787** waliofaulu sawa na **asilimia 98.9** ya wanafunzi **35,188** waliofanya mtihani huo mwaka 2015.

**Utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi bilioni 169.67** kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 81.68** zimetumika katika Shule za Msingi ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.8)*** na **Shilingi bilioni 87.99** kwa Shule za Sekondari (***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.9)***. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 53.91** zimetumika kwa ajili ya ruzuku ya uendeshaji, **Shilingi bilioni 52.61** kwa ajili ya chakula cha wanafunzi, **Shilingi bilioni 21.82** kwa ajili ya fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na wa bweni na **Shilingi bilioni 41.33** kwa ajili ya posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, Wakuu wa Shule za Sekondari na Maafisa Elimu Kata. Mpango wa Elimumsingi Bila Ada umewezesha ongezeko la wanafunzi hasa wanaotoka katika Kaya zenye kipato cha chini.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne kuanzia Desemba, 2015 hadi Februari 2020, Serikali imetumia jumla ya **Shilingi trilioni 1.01** kwa ajili ya kugharamia utoaji wa Elimumsingi Bila Ada kwa Shule za Msingi na Sekondari. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 460.63** zimetumika kwa Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 549.07** zimetumika kwa Shule za Sekondari. Mpango huu umewawezesha watoto wa Kitanzania kupata fursa ya masomo ya Shule za Msingi na Sekondari kutokana na kuondolewa kwa vikwazo vilivyokuwepo awali hasa michango kwa wanafunzi na ada. Aidha, Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ni utekelezaji wa Lengo la Nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) linalosisitiza *"Kuhakikisha elimu bora yenye usawa na kutoa fursa kwa watu wote kujiendeleza"*.

**Elimu Nje ya Mfumo Rasmi**

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2020, wanafunzi **11,777** wameandikishwa kupitia mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Idadi hiyo imepungua kutoka wanafunzi **69,492** waliondikishwa mwaka 2016 hadi wanafunzi **11,777** mwezi Machi 2020, kunatokana na mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ambao umewezesha wanafunzi wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa kila mwaka.

**Elimu ya Watu Wazima**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Serikali kupitia Programu ya Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Mfumo Rasmi wa Shule, imewawezesha vijana **28,220** kupata mafunzo ya ujasiriamali ikilinganishwa na vijana **36,055** waliosajiliwa mwaka 2016. Aidha, vijana wenye umri wa miaka **14** hadi **19** wamewezeshwa kupata mafunzo ya ujasiriamali, stadi za maisha pamoja na masomo ya ufundi yakiwemo ufugaji nyuki, samaki na kuku; ufundi seremala na uashi, utengenezaji mishumaa, sabuni, batiki, mafuta ya kujipaka, usindikaji vyakula pamoja na ushonaji. Walimu wapatao **216** wamejengewa uwezo wa utoaji wa mafunzo kwa kundi hilo la vijana ili kuwawezesha kupata ujuzi. Vilevile, jumla ya wanafunzi **9,939** wamesajiliwa na kuanza kusoma katika vituo **72** kwenye Mikoa nane (8) ya Kigoma, Tabora, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Dar es Salaam, na Dodoma. Lengo la mpango huu ni kuwawezesha vijana kupata elimu ya ujasiriamali ili waweze kujiajiri na kujipatia kipato.

**Elimu Maalum**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia pia utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hadi sasa, tunazo Shule **46** na Vitengo **682** kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hadi Machi 2020, shule na vituo hivyo vimeandikisha jumla ya wanafunzi **55,185** wa Shule za Msingi na wanafunzi **920** wa Shule za Sekondari. Idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum imeongezeka kutoka **49,655** walioandikishwa mwaka 2019 kutokana na kuongezeka kwa uelewa miongoni mwa jamii kuhusu haki za watoto wenye mahitaji maalum na kuboreshwa kwa miundombinu.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule za Msingi na Sekondari, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/20 imechapa na kusambaza rimu **7,664** katika Shule **416** za Sekondari. Aidha, karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu zimesambazwa kwa wanafunzi wasioona kwa gharama ya **Shilingi milioni 54.12** na nakala **53,104** ya vitabu vya kiada kwa Darasa la Kwanza hadi la Tano vilivyoandikwa kwa maandishi ya nukta nundu na vilivyoandikwa kwa maandishi makubwa *(large print)* zilisambazwa katika Shule za Msingi.

**Michezo Shuleni**

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeratibu na kusimamia michezo katika Shule za Msingi na Sekondari kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa. Katika mwaka 2019, mashindano ya michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA yalifanyika kitaifa katika Mkoa wa Mtwara na kuhusisha wanafunzi **2,662** na walimu **1,047** wa Shule za Msingi na wanafunzi **2,728** na walimu **965** wa Shule za Sekondari. Aidha, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeshiriki mashindano ya Michezo ya Shule za Msingi na Sekondari kwa Nchi za Afrika Mashariki yaliyofanyika mwezi Agosti, 2019 katika Mkoa wa Arusha. Michezo hiyo ilishirikisha jumla ya wanafunzi **4,448** kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (FEASSSA) za Kenya, Rwanda, Burundi, Sudani ya Kusini na Tanzania yenyewe. Michezo iliyoshindaniwa ni pamoja na soka, netiboli, mpira wa wavu, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, mpira wa magongo, raga, mpira wa meza, tenisi, kuogelea na riadha.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** mashindano hayo yamekuwa chachu ya kukuza na kuibua vipaji vya watoto wetu katika umri mdogo ambapo kwa mfano timu ya UMISSETA Copa Coca Cola Tanzania ilifanikiwa kushiriki fainali za mashindano ya Copa Coca Cola Afrika yaliyofanyika mwaka 2019 nchini Kenya na kutwaa ubingwa wa Afrika kati ya nchi **11** zilizoshiriki fainali za mashindano hayo. Aidha, zaidi ya **asilimia 80** ya wachezaji wanaounda timu za soka kwa vijana wenye umri chini ya miaka **19** kwa wasichana na wavulana wametokana na mashindano ya UMISSETA na UMITASHUMTA.

**Matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari**

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeweka msisitizo wa matumizi ya TEHAMA katika Shule za Msingi na Sekondari ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia ambayo ni muhimu katika uchumi wa viwanda. Hadi Februari 2020, jumla ya Shule **153** za Sekondari zinafundisha somo la **TEHAMA** kwa wanafunzi **36,101** wakiwemo wasichana **17,108** na wavulana **18,993**. Aidha, Shule za Sekondari zimejengewa uwezo wa kufundisha TEHAMA kwa kupatiwa Kompyuta **92,667** za Mezani, meza **5,346** za Kompyuta, Kompyuta Mpakato *(Laptops)* **46,207**, mashine za kudurufu **7,209**, *printer* **8,927**, *Projectors* **11,132**, Luninga *(Television)* **7,863** na Simu Janja (*Smart Phones*) **58,879**. Aidha, Shule za Msingi zimepatiwa Kompyuta za Mezani

# HOTUBA YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**3,148**, Kompyuta Mpakato (*laptops*) **3,570**, Mashine za Kudurufu **478**, *Printers* **603**, *Projectors* **891**, Televisheni **478** na Simu Janja (*Smart Phones*) **10,082.**

**Huduma za Kiuchumi na Uzalishaji**

**Sekta ya Kilimo**

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Februari 2020, mashamba darasa **357** yalikuwa yameandaliwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 458.0** ili kuelimisha wakulima kwa vitendo kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya kilimo katika Halmashauri za Wilaya za Chunya, Geita, Hai, Iringa, Kilolo, Kiteto, Mbarali, Mufindi, Mbinga, Rombo, Sumbawanga, Ulanga, Mbozi; Halmashauri za Miji ya Mafinga, Njombe na Tarime na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia ujenzi na ukarabati wa vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata katika Halmashauri za Majiji ya Arusha (katika Kata ya Themi) na Mbeya (katika Kata ya Igeyo) kwa gharama ya **Shilingi milioni 28.553.** Aidha, vituo vingine vimekarabatiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa (katika Kata ya Kibakwe) kwa gharama ya **Shilingi milioni 2.3** na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (katika Kata ya Kinyamwezi) kwa **Shilingi milioni 35**. Vituo hivyo vinatumika kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za kilimo kwa wakulima na wadau wengine wanaojihusisha na kilimo ili kuimarisha matumizi ya mbinu bora za kilimo.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya miche **3,115,240** ya mazao ya biashara ilikuwa imesambazwa kwa wakulima kwa gharama ya **Shilingi milioni 100.2.** Miche iliyosambazwa ni pamoja na miche **275,150** ya kahawa kwa gharama ya **Shilingi milioni 33.02** ambayo imesambazwa katika Halmashauri za Wilaya za Rombo, Karagwe, Mbozi na Halmashauri ya Mji wa Mbulu; miche **859,500** ya mikorosho imesambazwa kwa gharama ya **Shilingi milioni 11.895** katika Halmashauri za Wilaya za Mbarali, Kongwa na Mpwapwa; miche **1,955,536** ya pareto kwa gharama ya **Shilingi milioni 19.4** katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu; na miche **25,384** ya Miparachichi imeandaliwa na kusambazwa katika Halmashauri za Wilaya ya Ileje na Ukerewe kwa gharama ya Shilingi **milioni 35.920.**

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, maghala sita **(6)** ya kuhifadhia mazao yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Nyang'hwale, Ruangwa, Kiteto, Kilombero na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa gharama ya **Shilingi bilioni 7.39.** Aidha, masoko matano **(5)** ya mazao yamejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Geita, Ulanga, Muheza na Halmashauri ya Mji wa Kibaha ambayo yamegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 1.35.**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imezijengea uwezo Halmashauri **7** za Wilaya za Hanang, Babati, Karatu, Meru, Siha, Hai na Kilindi kuhusu uandaaji wa mipango bora ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Wilaya kwa gharama ya **Shilingi milioni 48.9**. Lengo la mipango hiyo ni kuboresha mazingra wezeshi katika uwezekezaji, uzalishaji na tija katika sekta hizo kwa kuzingatia malengo ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini.

**Uendelezaji Ardhi Mijini na Vijijini**

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, jumla ya viwanja **11,903** vimepimwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo uwekezaji na makazi katika Halmashauri za Manispaa za Ilemela **(viwanja 1,200),** Shinyanga (**viwanja 308**), Sumbawanga **(viwanja 254),** Iringa **(viwanja 253)**, Halmashauri za Miji za Kahama **(viwanja 2,300),** Bariadi **(viwanja 1,446),** Nzega **(viwanja 779),** Kondoa **(viwanja 172),** Halmashauri za Wilaya za Msalala **(viwanja 400),** Busega **(viwanja 1,186),** Misungwi **(viwanja 71),** Magu **(viwanja 1,535**), Ukerewe **(viwanja 1,434)** na Halmashauri ya Jiji la Mbeya **(viwanja 565).**

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe (*Master Plan*) wa Uendelezaji wa Jiji la Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mpango huo umekamilika na kuzinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuhakikisha uendelezaji wa Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya Nchi unafanyika kwa kuzingatia mpango huo. Aidha, Halmashauri nyingine **13** zikiwemo Majiji ya Mwanza na Arusha; Halmashauri za Manispaa za Singida, Musoma, Mtwara/Mikindani, Iringa, Kigoma/Ujiji, Tabora na Songea; na Halmashauri za Miji za Bariadi, Korogwe, Kibaha na Tunduma zimekamilisha maandalizi ya Mipango Kabambe na kuitangaza kwa ajili ya uendelezaji wa ardhi katika maeneo hayo.

**C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) umeendelea kusimamia matengenezo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja ili kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Februari 2020, TARURA ilikuwa imekamilisha matengenezo ya jumla ya kilomita **4,998.60** za barabara kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili ziweze kupitika katika kipindi chote cha mwaka. Kati ya barabara hizo, kilomita **1,396.38** zimefanyiwa matengenezo ya sehemu korofi, kilomita **730.19** zimefanyiwa matengenezo ya muda maalum na kilomita **2,872.03** zimefanyiwa matengenezo ya kawaida. Kazi nyingine zilizotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni ujenzi wa kilomita **31** za barabara za lami, madaraja **57**, makalvati **238** pamoja na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **9.3.** Ujenzi na matengenezo haya umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 154.13**

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** matengenezo, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya barabara umesaidia kuboresha usafiri na usafirishaji pamoja na utoaji huduma za kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Hata hivyo, mvua nyingi zinazoendelea kunyesha nchini zimeharibu sana miundombinu ya barabara za vijijini na mijini. Barabara hizo zilizoharibiwa na mvua zitafanyiwa matengenezo baada ya msimu wa mvua kumalizika. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini unaendelea kufanya matengenezo katika maeneo korofi katika kipindi hiki cha mvua ili barabara zilizoharibika ziendelee kupitika.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne, Serikali imetumia **Shilingi bilioni 799.37** kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara kupitia fedha za Mfuko wa Barabara. Fedha hizo zilitumika kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilometa **72,916.94.** Aidha, barabara zenye urefu wa kilometa **1,538.12** zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na barabara zenye urefu wa kilometa **485** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Vilevile, madaraja makubwa **7,** madaraja madogo **225,** makalvati **7,168** yamejengwa na kukamilika.

**Ujenzi wa Barabara Katika Mji wa Serikali Mtumba**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara katika Mji wa Serikali katika eneo la Mtumba zenye urefu wa kilometa **40.** Kati ya barabara hizo, barabara zenye urefu wa kilometa **11.2** zitakuwa za njia nne zitakazopitisha magari mawili kila upande na barabara zenye urefu wa kilometa **28.8** zenye njia mbili zitakazopitisha gari moja kila upande. Kwa mantiki hiyo, urefu halisi wa barabara zinazojengwa ni kilometa **51.2.** Miundombinu mingine itakayojengwa ni pamoja na: Makalvati makubwa **20,** makalvati madogo **52,** njia za watembea kwa miguu zenye upana wa **mita 1.5** kila upande wa barabara, njia za waendesha baiskeli zenye upana wa **mita 2.71** kila upande wa barabara, vituo vya kupakia na kushusha abiria **50**, taa za barabarani **739**, maeneo **mawili (2)** yenye taa za kuongoza magari, mifereji ya maji ya mvua yemye **kilometa 98** iliyojengwa kwa zege na makutano ya barabara ya mzunguko (*Roundabout*) **mbili (2).** Mradi huo umeanza kutekelezwa Februari, 2020 kupitia Mkandarasi *China Henan International Group Co. Ltd (CHICO)* kwa gharama ya **Shilingi bilioni 89.13** zinazojumuisha ujenzi na usimamizi wa mradi. Kati ya fedha hizo, Serikali imekamilisha malipo ya awali ya kiasi cha **Shilingi bilioni 13.21** na mradi unaendelea kutekelezwa. Mradi umepangwa kukamilika katika kipindi cha miezi **18** kulingana na mkataba. Mradi huu unasimamiwa na Mhandisi Mshauri *Afrisa Consulting* kwa gharama ya **Shilingi milioni 998.55.** Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuboresha eneo la Mji wa Serikali kwa miundombinu ya barabara na kuvutia uwekezaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa **asilimia 100.**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, TARURA imeanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa **64** kwa fedha za ndani katika Halmashauri **64** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 33** ikiwa ni utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Miradi hii itakapokamilika itawezesha Makao Makuu ya Halmashauri na Miji Midogo kuwa na barabara za kiwango cha lami na kuboresha usafiri na usafirishaji pamoja na utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii.

**Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya kilomita **47.59** za barabara ziliendelea kujengwa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya **Shilingi bilioni 85.67**. Kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa masoko **6** ya kisasa, ujenzi wa vizimba **33** vya kukusanyia taka ngumu na ujenzi wa vituo viwili **(2)** vya mabasi katika maeneo ya Kijichi na Mbagala.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha miaka minne cha Serikali ya Awamu ya Tano, mradi wa DMDP umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 357.26** ambazo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa kilomita **187.59** za barabara kwa kiwango cha lami, kati ya lengo la kujenga kilomita **210.** Aidha, madaraja mawili ya Tuangoma na Mwanamtoti yamejengwa na kukamilika katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **14**, ujenzi wa masoko **9** ya kisasa maeneo ya Kijichi, Makangarawe, Mbagala Kuu, Kilakala, Kigilagila, Bomubom, Minazi Mirefu, Mbagala na Bwawani katika Halmashauri za Manispaa ya Temeke, Ilala na Kinondoni. Aidha, umeandaliwa Mpango Kabambe wa Mfumo wa Maji ya Mvua na Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya kutatua changamoto ya mafuriko. Mpango huo utatekelezwa katika kipindi cha miaka **17** na ulianza kutekelezwa mwaka 2018 hadi mwaka 2035.

**Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)**

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, TARURA ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 92.57** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Miji ya Kimkakati (TSCP) katika Halmashauri za Majiji ya Tanga, Dodoma, Mbeya, Arusha na Mwanza na Halmashauri za Manispaa za Mtwara/Mikindani, Ilemela na Kigoma/Ujiji. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kilomita **89.22** za barabara kwa kiwango cha lami ambapo kilomita **85.82** zimekamilika, mifereji mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **16.47** na ujenzi wa madaraja **6** ya waenda kwa miguu ambao umekamilika.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, ujenzi wa masoko mawili ya kisasa umekamilika katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara/Mikindani. Utekelezaji wa mradi wa soko la kisasa katika Jiji Dodoma umefanyika katika kiwanja chenye ukubwa wa **ekari 27** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 14.64.** Mradi huo utanufaisha watoa huduma na wafanyabiashara **400.** Aidha, soko hilo litakuwa na uwezo wa kuegesha magari binafsi **600**, magari madogo ya abiria (daladala) **348** na malori **18**. Mradi huo utasaidia Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, TARURA imesimamia ujenzi wa Kituo Kikuu cha mabasi cha kisasa katika Jiji la Dodoma ambacho kitagharimu **Shilingi bilioni 24.03**. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia mabasi **100** na abiria **6,000** kwa wakati mmoja, kuegesha magari madogo **850,** bajaji **100** na pikipiki **150**. Aidha, kituo hicho kitakuwa na sehemu maalum kwa ajili ya abiria mahsusi (VIP) **80** kwa wakati mmoja. Aidha, kwa kipindi cha miaka mitatu, mradi wa TSCP umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 211.39** kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya barabara katika Miji minane (8) ya kimkakati.

**Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Miji 18 (ULGSP)**

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia TARURA imetekeleza Mradi wa Kuendeleza Miundombinu katika Miji 18 *(Urban Local Government Strengthening Programme - ULGSP)* katika Halmashauri za Miji **6** ya Babati, Bariadi, Geita, Kibaha, Njombe na Korogwe na Manispaa **12** za Bukoba, Lindi, Iringa, Morogoro, Moshi, Mpanda, Musoma, Shinyanga, Singida, Songea, Sumbawanga na Tabora kwa fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mwaka wa fedha 2019/20, jumla ya **Shilingi bilioni 120.35** zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa **kilometa 49.3**, ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya mabasi **5,** masoko **3** katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Iringa na Njombe; machinjio ya kisasa **matano (5);** kituo kimoja cha malori katika Halmashauri ya Mji Bariadi na kituo kimoja cha daladala katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Shughuli nyingine zilizofanyika ni pamoja na maandalizi ya Mpango Kabambe (General Planning Scheme - GPS) katika miji **10**, ununuzi wa malori **10** ya kubeba taka ngumu, ununuzi wa mitambo ya kuchakata taka ngumu **2,** ununuzi wa vifaa vya kukusanya taka ngumu **31** na ukarabati wa madampo **mawili (2)** katika Halmashauri za Manispaa za Moshi na Shinyanga.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne Mradi wa ULGSP umetumia jumla ya **Shilingi bilioni 419.44** kwa ajili ya ujenzi wa barabara zenye urefu **kilometa 175.34** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa vituo **11** vya mabasi, ujenzi wa masoko manne **(4)** katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Iringa na Miji ya Njombe na Korogwe; machinjio ya kisasa **matano (5),** vituo **viwili (2)** vya malori katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Mji Bariadi; vituo **viwili (2)** vya daladala katika Halmashauri ya Manispaa za Singida na Morogoro, maandalizi ya Mpango Kabambe (General Planning Scheme-GPS) katika Miji **18**, ununuzi wa malori **34** ya kubeba taka ngumu, ununuzi wa mitambo **10** ya kuchakata taka ngumu, ununuzi wa vifaa **231** vya kukusanyia taka ngumu, ukarabati wa madampo **matatu (3)** katika Halmashauri za Manispaa za Lindi, Moshi na Shinyanga na ujenzi wa bustani moja ya kupumzikia katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

**Mradi wa Kimkakati Katika Maeneo ya Uzalishaji wa Kilimo (Agri-Connect Programme)**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** TARURA kupitia mradi wa kimkakati wa kuboresha maeneo ya uzalishaji wa kilimo kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya inajenga barabara zenye urefu wa kilomita **87.6** kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Rungwe na Mbeya. Hadi Februari, 2020 jumla ya **Shilingi bilioni 40.7** zilikuwa zimetolewa ili kuanza utekelezaji wa mradi huo. Lengo la mradi huu ni kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yanayozalisha mboga mboga, chai na kahawa ili kuimarisha mnyonyoro wa thamani wa mazao ya kilimo na upatikanaji wa masoko. Hadi Februari 2020, taratibu za ununuzi zilikuwa zimekamilika na mikataba ilikuwa imesainiwa. Makandarasi wapo hatua ya kupeleka vifaa vya ujenzi maeneo ya kazi. Kazi za ujenzi wa barabara hizo zinategemewa kukamilika ifikapo mwezi Mei 2021.

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam (DART)**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam (DART) umeendelea kusimamia utoaji huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) inayohusisha barabara za Kimara-Kivukoni; Magomeni-Morocco na Fire-Kariakoo zenye urefu wa kilometa **20.9.** DART pia imeendelea na maandalizi ya kumtafuta mtoa huduma wa kudumu atakayekuwa na uwezo kutoa huduma ya mabasi **305** ikilinganishwa na mtoa huduma wa sasa ambaye ana uwezo wa kutoa huduma ya mabasi **140**. Zabuni ya kumpata mtoa huduma imetangazwa na taratibu za ununuzi zinaendelea. Vilevile, DART imeshughulikia ulipaji wa fidia na uhamishaji wa miundombinu ya kijamii ambapo hadi Februari 2020, **Shilingi bilioni 28.84** zilitumika katika Awamu ya Pili ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) wenye urefu wa kilometa **20.3** ambao unahusisha barabara za Kilwa, Gerezani, Sokoine, Bandari, Chang'ombe na Kawawa.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya Awamu ya Tatu ya mradi wa BRT utakaohusisha barabara za Azikiwe, Maktaba, Lindi, Shaurimoyo, Uhuru, Bibi Titi, Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto zenye urefu wa kilomita **23.6** yanaendelea. Hadi Februari, 2020 malipo ya fidia ya **Shilingi bilioni 5.29** yalikuwa yamefanyika kwa wananchi **77** waliopisha utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya BRT. Miradi hii itakapokamilika itapunguza msongamano wa magari, kupunguza muda wa kusafiri, kuboresha mandhari na kuongeza tija katika utoaji wa huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Jiji la Dar es Salaam.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** DART imeimarisha usimamizi na matengenezo ya miundombinu katika vituo vikuu vitano **(5)** vya Kimara, Ubungo, Morocco, Gerezani na Kivukoni, vituo vidogo ishirini na saba **(27)** na madaraja ya waenda kwa miguu matatu **(3).** Vilevile, Ofisi ya Rais -TAMISEMI kupitia DART kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Mamlaka ya Serikali Mtandao inaendelea na usanifu wa mfumo wa ukusanyaji nauli (*Automatic Fare Collection System - AFCS*) na ununuzi wa vifaa vya mfano yakiwemo mageti sita **(6)** na kadi janja *(smart cards)* kwa ajili ya ukusanyaji wa nauli na kudhibiti upotevu wa mapato.

**Tume ya Utumishi wa Walimu**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Tume ya Utumishi wa Walimu imepokea na kushughulikia rufaa **106** zinazohusu masuala ya utumishi wa walimu. Aidha, vikao vya Kamati **208** vya kisheria vimefanyika katika ngazi ya Wilaya na kuwezesha walimu **2,591** kuthibitishwa kazini, walimu **112** walibadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza, walimu **123,444** wamepandishwa vyeo na mashauri ya nidhamu **399** yalitolewa uamuzi. Mafanikio haya yamesaidia kuongeza ari ya utendaji kazi wa walimu ili kuinua kiwango cha taaluma katika Shule za Msingi na Sekondari.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Makatibu **139** wa Wilaya wamejengewa uwezo kuhusu masuala ya utumishi wa walimu, upandishwaji vyeo na usimamizi wa nidhamu. Mafunzo hayo yataongeza ufanisi katika kuimarisha usimamizi wa walimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vilevile, watumishi **80** wa Tume ya Utumishi wa Walimu wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa vihatarishi katika utendaji wa kila siku wa kazi za Tume. Mkakati huo utawezesha Tume kuchukua hatua za haraka za kuondoa vihatarishi hivyo ili kufikia malengo ya utekelezaji wa majukumu yake.

**Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo**

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo kimekamilisha ujenzi wa kumbi mbili za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **1,008** kwa kutumia mapato ya ndani ya Chuo. Aidha, viti **504** visivyohamishika vimefungwa katika darasa moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **504.** Ujenzi wa miundombinu hiyo umeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa wanachuo. Vilevile, hadi kufikia Februari 2020, Chuo cha Serikali za Mitaa kimevuka lengo kwa kudahili wanafunzi **7,484** kati ya lengo la kudahili wanafunzi **5,000** sawa na **asilimia 149.68.**

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimefanikiwa kuanzisha Shahada ya Kwanza ya Menejimenti ya Utawala katika Serikali za Mitaa ambayo imepokea wanafunzi **20** katika mwaka wa masomo wa 2019/20 ili kukidhi mahitaji wa wataalam wa Menejimenti na Utawala katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mkakati huo unalenga kukitangaza Chuo ndani na nje ya nchi ili watu wengi zaidi wavutiwe kusoma katika Chuo cha Serikali za Mitaa ambacho ni cha kipekee katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo kimefanikiwa kupeleka masomoni jumla ya watumishi ***55*** kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Kati ya hao, watumishi **14** wamekwenda kusoma Shahada ya Uzamivu; Watumishi ***tisa (9)*** Shahada ya Uzamili; Watumishi wanne ***(4)*** Shahada ya Kwanza na watumishi **28** wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi **724** kutoka katika Halmashauri **14** za Mikoa ya Mbeya, Morogoro, Iringa, Singida, Dar es Salaam na Dodoma wamepatiwa mafunzo kuhusu uandaaji wa mipango na bajeti, usimamizi wa mazingira, usimamizi wa fedha za Serikali za Mitaa na masuala ya utawala bora.

**Shirika la Elimu Kibaha**

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya kuanzishwa kwa Shirika la Elimu Kibaha ni kupambana na maadui watatu wa maendeleo ambao ni ***Ujinga, Umaskini*** na ***Maradhi***. Hivyo, Shirika linasimamia utoaji wa huduma za elimu kupitia Shule za Msingi na Sekondari na huduma za afya na maendeleo ya jamii kupitia Hospitali ya Rufaa Tumbi na Chuo cha Maendeleo ya Jamii .

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika la Elimu Kibaha limewezesha kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **2,796** na kutoa huduma za maktaba kwa wadau **16,050** wa ndani na nje. Shirika limefanikiwa kukarabati miundombinu ya Shule ya Sekondari Kibaha uliohusisha ujenzi wa uzio, ukarabati wa mabweni matatu yenye uwezo wa kulaza jumla ya wanafunzi **660**, ujenzi wa jengo la utawala, jengo la maktaba, jengo la maabara, jengo la kilimo, jiko na bwalo na madarasa mawili ya Kidato cha Kwanza uliogharimu **Shilingi bilioni 1.18.** Ukarabati uliofanyika umesaidia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** kitaaluma, Shule zinazomilikiwa na Shirika zimeendelea kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa. Mathalani, Shule ya Sekondari Kibaha imefanya vizuri katika Mtihani wa Taifa wa mwaka 2019 kwa kufaulisha **asilimia 100** ya wanafunzi **172** waliofanya mtihani wa Kidato cha Sita. Aidha, jumla ya wanafunzi **59** walifaulu Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Kidato cha Nne kwa mwaka 2019 sawa na takribani **asilimia 87** ya wanafunzi **68** waliofanya mtihani huo. Vilevile, wanafunzi **119** sawa na asilimia **99** wa Shule ya Msingi Tumbi wamefaulu Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba wa mwaka 2019 kati ya wanafunzi **120** waliofanya mtihani huo.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2019/20, Shirika limetoa elimu ya ujasiriamali kwa wanufaika **695** katika fani za ufugaji, kilimo, ufundi wa umeme wa majumbani, uungaji na uundaji vyuma, uashi na useremala, ufundi wa mitambo na magari, hoteli na ushonaji. Mafunzo hayo yametolewa kupitia Chuo cha Maendeleo ya Jamii kinachomilikiwa na Shirika. Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha vijana kupata elimu ya ujasiriamali ili waweze kutekeleza miradi itakayokuza kipato na ajira.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Shirika lilikuwa limetoa huduma za afya kwa wagonjwa **36,500** kupitia Hospitali ya Rufaa ya Tumbi. Kati ya hao, wagonjwa **18,592** walitibiwa na kuondoka na wagonjwa **17,908** walilazwa na kutibiwa. Aidha, Hospitali imehudumia majeruhi **1,336** kutokana na ajali wakiwemo wanawake **364** na wanaume **972**.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2020, Shirika limefanikiwa kufunga mtambo mpya wa *X-Ray* wenye thamani ya **Shilingi milioni 428** kwa ufadhili wa nchi ya Korea Kusini. Aidha, mashine mbili za kutolea dawa ya usingizi zimesimikwa ili kuboresha huduma za upasuaji na matibabu ya dharura. Vilevile, Shirika limekarabati jengo la watoto na wodi Daraja la I na II kwa gharama ya **Shilingi milioni 42.56.**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha upatikanaji wa dawa, Shirika limeanzisha duka la dawa la Hospitali kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa. Kwa sasa hali ya upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa Hospitalini hapo ni **asilimia 90.**

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

# HOTUBA YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

151. *Mheshimiwa Spika,* Shirika limeimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato ya Shirika ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato. Matumizi ya mifumo hiyo yamechangia kuimarisha makusanyo kutoka **Shilingi milioni 263.04** kwa mwezi hadi **Shilingi milioni 285.89** kwa mwezi sawa na **Shilingi bilioni 3.43** kwa mwaka.

152. *Mheshimiwa Spika,* mapato yanayokusanywa yamewezesha Shirika kuimarisha uwekezaji ambapo wafanyabiashara **1,673** wamepata vibanda vya biashara na wanaliingizia Shirika mapato. Wafanyabiashara hao wanajumuisha wapangaji wa Ofisi na maeneo ya wazi **121,** wapangaji wa maduka **205**, wapangaji wa mbao katika soko dogo **231**, wafanyabiashara katika soko la wazi **575** na eneo la shimoni ndani ya soko wafanyabiashara wadogo **541.** Aidha, Shirika limefanya mapitio ya Mpango wa Biashara ili kupanua fursa za uwekezaji ndani na nje ya Jiji la Dar es Salaam.

153. *Mheshimiwa Spika,* Shirika limefanikiwa kuimarisha hali ya usafi na mazingira ndani na nje ya soko kwa kutekeleza mikakati ya uondoshaji wa taka. Aidha, ukarabati mdogo wa soko umefanyika kwa gharama ya **Shilingi milioni 64.5** hasa sehemu ya shimoni kwa kufunga mifumo ya hewa (viyoyozi) kwa kuzingatia idadi kubwa ya watu wanaotumia soko hilo. Mikakati hiyo imesaidia kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa watumiaji.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

154. *Mheshimiwa Spika,* hadi Februari 2020, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imefanikiwa kukusanya marejesho ya mikopo kiasi cha **Shilingi milioni 227.58** kutoka kwenye Halmashauri zilizokopeshwa mikopo kwa ajili ya uwekezaji. Aidha, michango ya akiba kiasi cha **Shilingi milioni 97.26** imekusanywa kutoka kwenye Halmashauri ili kujenga uwezo wa Bodi kutoa mikopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

155. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imefanikiwa kutoa mkopo wa **Shilingi milioni 550.00** kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la biashara ambalo litakuwa na ukumbi wa mikutano na biashara nyingine na **Shilingi milioni 520.0** zimekopeshwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa ajili ya kuendeleza uwanja wa michezo wa Halmashauri.

156. *Mheshimiwa Spika,* utoaji wa mikopo umefanyika sambamba na utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wataalam wa Halmashauri **22** za Mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam na Pwani kuhusu uandaaji wa maandiko ya miradi ya maendeleo na kuimarisha usimamizi wa miradi iliyopatiwa mikopo ili kudhibiti viashiria vinavyoweza kukwamisha malengo ya miradi. Lengo la Bodi ni kujenga uwezo wa Halmashauri ili ziweze kuandaa maandiko ya miradi yatakayokidhi vigezo vya kupata mkopo.

## D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

157. *Mheshimiwa Spika,* Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kuzindua Bunge mwaka 2015 na maelekezo ya viongozi wengine wa Kitaifa, Sera, Miongozo ya Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi.

**Ofisi ya Rais-TAMISEMI**

158. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma *(D by D);*
   ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi, Lishe na Ustawi wa Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ikijumuisha utekelezaji wa mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Ada;
   iv) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   v) Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI;
   vi) Kuendeleza rasilimaliwatu katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kuwaongezea ujuzi kwa lengo la kuongeza ufanisi;
   vii) Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya Biashara na Uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;
   viii) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   ix) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI ikiwa ni pamoja na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   x) Kuratibu shughuli za utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI;
   xi) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya barabara, afya, elimu inayotekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   xii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya, na Halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri 30 ambazo zimeelekezwa na Serikali kuhamia katika maeneo yao ya utawala; na
   xiii) Kusimamia matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

**Tawala za Mikoa**

159. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Tawala za Mikoa zitatekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;
   ii) Kuratibu utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan katika usimamizi wa afya ya msingi, elimu ya msingi na sekondari, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, lishe na ustawi wa jamii;
   iii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa majengo ya Ofisi na nyumba za makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya , Makatibu Tawala Wasaidizi, Maafisa Tarafa na watumishi waandamizi;
   iv) Kuratibu zoezi la Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 wa Rais, Wabunge na Madiwani uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2020;
   v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisekta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;
   vi) Kusimamia rasilimaliwatu na fedha katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   vii) Kuratibu mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   viii) Kuratibu utekelezaji wa masuala mtambuka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   ix) Kuratibu uanzishwaji wa viwanda kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara mijini na vijijini, uwekezaji wa viwanda vidogo, vya kati, na vikubwa kwa kutumia malighafi zilizopo;
   x) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   xi) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali za uchumi katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   xii) Kuendelea kusimamia na kuimarisha Utawala Bora katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   xiii) Kuratibu uanzishaji wa viwanda vya kuchakata/kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo;
   xiv) Kufanya mapitio ya mipango mikakati ya Tawala za Mikoa na kuratibu mapitio ya mipango mikakati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   xv) Kuratibu uendelezaji wa maeneo maalum ya shughuli za kiuchumi na uwekezaji;
   xvi) Kuratibu utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake (4%), Vijana (4%) na Watu Wenye Ulemavu (2%);
   xvii) Kuhamasisha na kusimamia kilimo cha mazao ya kipaumbele; na
   xviii) Kuandaa na kuboresha wasifu wa uwekezaji (*Investment Profile)* na Miongozo ya Uwekezaji *(Investment Guide).*

**Mamlaka za Serikali za Mitaa**

160. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-
   i) Kusimamia ulinzi na usalama;
   ii) Kushiriki katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2020;
   iii) Kuimarisha na kubuni mikakati ya kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani;
   iv) Ukamilishaji na kuanza ujenzi wa majengo ya Ofisi, nyumba za makazi ya viongozi na watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo Halmashauri 30 zilizohamia katika maeneo yao ya utawala;
   v) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya huduma za kijamii na kiuchumi katika sekta zote hususan kujenga na kuboresha Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya, Zahanati, maabara za masomo ya sayansi, nyumba za watumishi, matundu ya vyoo, na vyumba vya madarasa;
   vi) Kusimamia Mpango wa Utoaji wa Elimumsingi Bila Ada katika Shule za Msingi na Sekondari;
   vii) Kukamilisha ujenzi wa miradi viporo ya miundombinu mbalimbali ya huduma za kijamii;
   viii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji kwa kuhakikisha mikutano ya kisheria inafanyika na taarifa za mikutano hiyo zinawekwa katika maeneo ya wazi na katika tovuti za kila Halmashauri hasa taarifa za mapato na matumizi.
   ix) Kubuni na kutekeleza miradi ya kimkakati itakayosaidia kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri;
   x) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuimarisha utendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   xi) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na maeneo ya wafanyabiashara wadogo (Machinga);
   xii) Kusimamia na kuratibu shughuli za uendelezaji Miji na Vijiji; na
   xiii) Kusimamia utunzaji wa mazingira na shughuli mtambuka.

## E. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OR-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

**Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)**

161. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA kupitia Mfuko wa Barabara umepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-
   i) Matengenezo ya barabara za Wilaya zilizopo vijijini na mijini zenye urefu wa kilometa 23,175.11. Kati ya hizo, kilomita 14,104.86 ni matengenezo ya kawaida, kilometa 6,094.52 ni matengenezo ya maeneo korofi na kilometa 2,975.73 ni matengenezo ya muda maalum.
   ii) Ujenzi na ukarabati wa madaraja 80, makalvati 2,052 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 79.9. Ujenzi wa barabara urefu wa kilometa 35.3 kwa kiwango cha lami na ukarabati urefu wa kilometa 321 kwa kiwango cha changarawe.

Katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya Shilingi bilioni 275.03 zimetengwa kupitia Mfuko wa Barabara kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo pamoja na kazi za ufuatiliaji na utawala.

**Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu Katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**

162. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam umetengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 186.8** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-
   i) Kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 47.59 kwa kiwango cha lami kwa mikataba na Makandarasi inayoendelea;
   ii) Kuanza ujenzi wa barabara ya Nzasa-Kilungule-Buza (kilomita 7.6),Ulongoni-Bangulo-Kinyerezi (kilomita 7.5) na Magomeni Mapipa- Urafiki (kilomita 7.31);
   iii) Kuanza ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 11.7 kwa kiwango cha lami katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni;
   iv) Kuendelea na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 26;
   v) Kukamilisha ujenzi wa masoko sita (6) ya Kilakala, Kigilagila, Bomubom, Minazi Mirefu, Mbagala na Bwawani;
   vi) Kuandaa Mpango wa Uendelezaji Ukanda wa Mabasi Yaendayo Haraka (Intergrated Transport and Land Use Planning along BRT Corridor);
   vii) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani (Local Government Revenue Collection Information System) uliounganishwa na mfumo wa kijiografia wenye taarifa muhimu za vyanzo vya mapato; na
   viii) Ununuzi wa vifaa vya kufanyia usafi wa miundombinu ya barabara na mifereji ya maji ya mvua.

**Mradi wa Kuboresha Barabara Katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (Agri-Connect Programme)**

163. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, TARURA imetengewa **Shilingi bilioni 35.5** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuboresha Barabara katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo utakaohusisha ujenzi wa barabara katika baadhi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Maeneo ambayo barabara hizo zitajengwa yatakuwa ni yale yenye miradi mingine ya uendelezaji wa kilimo inayofadhiliwa na Jumuiya ya Nchi za Ulaya na kuratibiwa na Wizara ya Kilimo. Lengo la mradi huu ni kuboresha miundombinu ya barabara katika maeneo yanayozalisha mboga mboga, chai na kahawa ili kuimarisha mnyonyoro wa thamani wa mazao na upatikanaji wa masoko.

**Mradi wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini *(Roads to Inclusion and Socio-Economic Opportunities - RISE)***

164. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaanza utekelezaji wa Mradi mpya wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii. Mradi utatekelezwa katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara ambapo kazi za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zitafanyika katika Mkoa wa Iringa na kazi ya matengenezo ya maeneo korofi na matengenezo ya kawaida yatafanyika kwenye Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro, Rukwa, Katavi, Songwe, Tanga, Pwani, Dodoma, Mtwara, Ruvuma na Lindi. Mradi huu utagharimu jumla ya **Shilingi bilioni 817.25** sawa na **Dola za Marekani millioni 350)** kwa kipindi cha miaka sita (6) kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2025/26 ambazo Serikali inatarajia kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu una vipengele vinne ambavyo ni ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini, uimarishaji wa Taasisi, usimamizi wa rasilimaliwatu na ufuatiliaji wa miradi na ushirikishwaji wa jamii. Lengo la mradi huu ni kuboresha ujenzi na upitikaji wa barabara ili kusaidia kuinua kipato cha watu wanaoishi vijijini katika maeneo yaliyoteuliwa na kujenga uwezo wa usimamizi endelevu wa barabara za vijijini. Katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi bilioni 28.0** zimetengwa ili kuanza utekelezaji wa mradi.

165. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na ukuaji wa miji nchini unaoenda sambamba na uhitaji wa miundombinu ya msingi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mwaka wa fedha 2020/21 itaanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi mpya ujulikanao kama *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness Project* (TACTIC). Mradi huu utahusisha Halmashauri **45** za Majiji, Manispaa na Miji. Lengo la mradi huu ni kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ya uwekezaji katika maeneo ya mijini. Mradi huu ni muendelezo wa Mradi wa Miji ya Kimkakati (TSCP) na Mradi wa Kuimarisha Miundombinu katika Halmashauri za Miji (ULGSP) uliogharamiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia.

**Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Katika Jiji la Dar es Salaam (DART)**

166. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam utatekeleza kazi zifuatazo:-
   i) Kusimamia utoaji wa huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) katika Jiji la Dar es Salaam;
   ii) Kuendelea na utekelezaji wa mpango kazi juu ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa miundombinu ya barabara Awamu ya Tatu;
   iii) Kuanza taratibu za kuwapata Wazabuni wa kutoa huduma za kusafirisha abiria, Mkusanyaji wa Nauli na Meneja wa Mfuko wa Fedha kwa Awamu ya Pili na ya Tatu ya mradi;
   iv) Kuimarisha makusanyo ya mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;
   v) Kufanya mapitio ya michoro kwa ajili ya usimikaji wa mtandao wa mawasiliano wa Wakala (DART - net);
   vi) Kuhuisha Kanuni na Sheria Ndogo ili ziendane na mahitaji ya uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka; na
   vii) Usimamizi, uendeshaji na ufuatiliaji wa mashauri mahakamani na usimamizi wa mikataba ya Wakala.

**Tume ya Utumishi wa Walimu**

167. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kusimamia maadili na kutoa uamuzi wa mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko ya walimu katika Shule za Msingi na Sekondari;
   ii) Kusimamia upangaji na msawazo wa Walimu kwa Shule za Msingi na Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
   iii) Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu Jijini Dodoma;
   iv) Kuratibu upandishwaji wa madaraja kwa walimu;
   v) Kuimarisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusimamia masuala ya walimu nchini;
   vi) Kuelimisha wadau kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu;
   vii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wa Tume Makao Makuu na kwenye Wilaya pamoja na kuendeleza rasilimaliwatu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi; na
   viii) Kufanya mapitio na kuandaa Mpango Mkakati wa Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2024/25.

**Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo**

168. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kudahili wanafunzi 7,000 wakiwemo wanafunzi 5,800 Kampasi ya Hombolo na wanafunzi 1,200 katika Kampasi iliyoko Dodoma Mjini;
   ii) Kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 katika Kampasi ya Hombolo;
   iii) Kukamilisha ujenzi wa daharia (hostel) ya wanafunzi wa kike yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 kwa kuweka samani;
   iv) Ujenzi wa darasa na Ofisi Awamu ya Kwanza katika Kampasi ya Dodoma Mjini; na
   v) Ujenzi wa jengo la utawala Awamu ya Kwanza katika Kampasi ya Hombolo.

**Shirika la Elimu Kibaha**

169. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kuendelea kutoa huduma za afya, kinga na tiba katika Hospitali ya Tumbi;
   ii) Kuendelea kutoa elimu ya uuguzi na utabibu kwa wanafunzi 430 katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;
   iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi 1,758 wa Sekondari na wanafunzi 926 wa Shule ya Msingi;
   iv) Kuendelea kutoa huduma za maendeleo ya jamii ili kupunguza umaskini kwa kutoa mafunzo ya ufundi, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha na shamba darasa la mifugo na mazao;
   v) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya Hospitali;
   vi) Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa jamii;
   vii) Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa Hospitali ya Tumbi;
   viii) Kujenga maabara ya Baiolojia, Maarifa ya Nyumbani (Home Economics) na mabweni katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha; na
   ix) Kukarabati madarasa ya Shule ya Msingi Tumbi.

**Shirika la Masoko ya Kariakoo**

170. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Masoko ya Kariakoo litatekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu katika maeneo mbalimbali ya Shirika ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara;
   ii) Kuendelea na ujenzi wa Soko la jumla katika eneo la Mbezi Beach (Makonde); na
   iii) Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ndani ya Shirika la Masoko ya Kariakoo.

**Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

171. *Mheshimiwa Spika;* katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-
   i) Kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo;
   ii) Kuendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu kuandaa maandiko ya miradi ya maendeleo itakayokidhi vigezo vya kukopesheka;
   iii) Kuimarisha ufuatiliaji wa urejeshwaji wa mikopo na uwasilishwaji wa michango kutoka Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi; na
   iv) Kubuni vyanzo vipya vya mapato.

# HOTUBA YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## F. MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### Sekta ya Afya

172. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika sekta ya afya:-

i) Ujenzi wa wodi tatu (3) katika kila Hospitali 67 za Halmashauri zinazoendelea kujengwa ambapo zimetengwa jumla ya Shilingi bilioni 32.50 kwa kazi hiyo. Kukamilika kwa ujenzi wa wodi hizo kutawezesha Hospitali hizo kuanza kutoa huduma kwa wagonjwa;

ii) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya 27 za Halmashauri ambapo zimetengwa jumla ya Shilingi bilioni 27.00. Hospitali hizo zinajengwa katika Halmashauri za Wilaya za Karatu, Chalinze, Kondoa, Kongwa, Mbogwe, Biharamulo, Nsimbo, Kigoma, Kakonko, Liwale, Serengeti, Sengerema, Mbeya, Kilombero, Kaliua, Babati, Mvomero, Newala, Madaba, Kwimba, Msalala, Ikungi, Handeni, Mkinga, Halmashauri ya Mji wa Tunduma na Halmashauri za Manispaa za Sumbawanga na Tabora;

iii) Ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati 3 katika kila Halmashauri ambapo zimetengwa jumla ya Shilingi bilioni 27.75, Kipaumbele kitakuwa ni kukamilisha maboma ya Zahanati zilizoanza kujengwa kwa nguvu za Wananchi;

iv) Ununuzi wa vifaa tiba katika Hospitali 67 za Halmashauri ili kuziwezesha kuanza kutoa huduma. Katika mwaka wa fedha 2020/21, zimetengwa jumla ya Shilingi bilioni 32.50 kwa kazi hiyo;

***Mchanganuo wa miundombinu ya vituo vya kutolea huduma za afya na upatikanaji wa vifaa tiba umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 10.***

v) Mpango wa Uimarishaji wa Huduma za Afya ya Msingi kwa Matokeo umetengewa **Shilingi bilioni 128.91** kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya afya, ununuzi wa vifaa tiba, ajira za watumishi wa afya kwa mkataba, kujenga uwezo wa watumishi wa sekta ya afya na usimamizi wa mradi.

### Sekta ya Elimu

173. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo katika sekta ya elimu:-

i) Ugharamiaji wa Elimu msingi Bila Ada ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 298.13** kwa Shule za Msingi na Sekondari. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 137.63** zitatumika kwa Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 160.49** zitatumika kwa Shule za Sekondari. Bajeti hiyo ni sawa na ongezeko la **Shilingi bilioni 9.6** ikilinganishwa na Bajeti ya **Shilingi bilioni 288.48** iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Ongezeko la Bajeti limetokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika Shule za Msingi na Sekondari ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.11);***

ii) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa katika Shule za Msingi kwenye Halmashauri **184** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 26.10** zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.12).*** Miradi itakayokamilishwa ni ile iliyoanza kutekelezwa kwa nguvu za wananchi ili ianze kutoa huduma;

iii) Ukamilishaji wa ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi **1,411** katika Shule za Sekondari kwenye Halmashauri **184** ambapo zimetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 42.33** ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 13).*** Lengo ni kuwezesha ukamilishaji wa maabara hizo ili zianze kutumika kwa ajili ya masomo ya sayansi katika Shule za Sekondari; na

iv) Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu umetengewa **Shilingi bilioni 73.6** kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari kwenye Halmashauri 184 nchini (**Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 14**). Aidha, Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (LANES) imetengewa **Shilingi bilioni 9.34** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **150** kwa ajili ya elimu ya awali, ujenzi wa mabweni **10** katika Shule zenye watoto wenye mahitaji maalum, kujenga uwezo wa Walimu kufundisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, ununuzi wa vifaa vya watoto wenye mahitaji maalum na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA.

### Sekta ya Miundombinu

174. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambao utahusisha utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

i) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita **23,531,** madaraja **80,** makalvati **2,052** na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita **79.9** ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 275.03** kupitia Mfuko wa Barabara;

ii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP) ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 186.8** kwa ajili ya ujenzi wa kilomita **70** za barabara kwa kiwango cha lami;

iii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Barabara Katika Maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo *(Agri-Connect Programme)* ambao umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 35.5;**

iv) Kuanza utekelezaji wa Mradi mpya wa Barabara wa Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini *(Roads to Inclusion and Socio-Economic Opportunities - RISE)* ambao umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 28.0.** Mradi utatekelezwa katika Mikoa 13 ya Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro, Rukwa, Katavi, Songwe, Tanga, Pwani, Dodoma, Mtwara, Ruvuma na Lindi.

v) Kuanza maandalizi ya mradi mpya wa *Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness Project* (TACTIC) ambao utahusisha ujenzi wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji.

### Maeneo ya Utawala

175. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeweka kipaumbele na kutenga **Shilingi bilioni 49.29** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya utawala ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tarafa na nyumba za viongozi katika Mikoa, Wilaya na Tarafa ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 15).***

***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imetenga fedha za kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri na nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara kama ifuatavyo:- Ujenzi wa majengo ya utawala ya Ofisi za Halmashauri **100** ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 80.42** kwa ajili ya kutekeleza ujenzi huo. Aidha, ujenzi wa nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara umepangwa kufanyika katika Halmashauri **9** ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 1.35** zimetengwa ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.16).***

### Ununuzi wa Magari

176. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya magari **54** yatanunuliwa katika Mikoa na Halmashauri. Kati ya magari hayo, magari **16** yatanunuliwa kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambapo zimetengwa **Shilingi bilioni 4.48** na magari **38** yatanunuliwa kwa ajili ya Halmashauri **38** zenye makusanyo madogo ya mapato ya ndani ambapo zimetengwa jumla ya **Shilingi bilioni 8.36** ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.17).***

### Miradi ya Kimkakati

177. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambapo Halmashauri **16** zimetengewa jumla **Shilingi bilioni 50.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.18).*** Miradi hiyo ina lengo la kuongeza wigo wa mapato ya Halmashauri ili kuziwezesha kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa ufanisi na kupunguza utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu.

### Kiinua Mgongo cha Madiwani

178. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 61.76** kwa ajili ya kulipa kiinua mgongo cha Madiwani watakapomaliza muda wao wa uongozi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

### Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

179. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itasimamia utoaji wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 64.46** zimetengwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 25.78** zitatumika kwa ajili ya vikundi vya Wanawake, **Shilingi bilioni 25.78** zitatumika kwa ajili ya vikundi vya Vijana na **Shilingi bilioni 12.89** zitatumika kutoa mikopo kwa vikundi vya Watu Wenye Ulemavu ***(Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 19).***

### Programu ya Maboresho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa *(Regional and Local Government Strengthening Programme-RLGSP)*

180. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaanza utekelezaji wa programu mpya ya Maboresho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo itatekelezwa kwa muda wa miaka 10 kwa kipindi cha miaka mitano mitano kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2029/30. Malengo ya programu hii ni kuimarisha ugatuaji wa majukumu na mahusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kuimarisha utoaji wa huduma kwa kuboresha usimamizi wa rasilimali watu na fedha, kuimarisha ushiriki wa jamii katika kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo, kukuza uchumi katika ngazi ya jamii *(Local Economic Development)* na kujenga uwezo wa usimamizi na ufuatiliaji na tathmini.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Programu hii imeandaliwa kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Awamu ya Kwanza na Pili pamoja na maboresho mengine yanayoendelea ndani ya Serikali. Programu hii itasaidia kuimarisha utawala bora, usimamizi wa rasilimali katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii na ushiriki wa jamii katika kujiletea maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2020/21, programu imetengewa **Shilingi bilioni 1.5.**

### Tume ya Utumishi wa Walimu

182. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Utumishi wa Walimu imetengewa **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Tume katika Jiji la Dodoma.

## G. SHUKRANI

183. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, naomba kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, Mwenyekiti wa Kamati na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Maoni na ushauri wa Kamati yamesaidia kuleta mageuzi makubwa yaliyotokea katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa programu, miradi na shughuli mbalimbali za Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), *Global Partnership for Education,* Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) na Nchi zote zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wadau wa Maendeleo katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuboresha utoaji huduma na kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru Wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sehemu kubwa ya mafanikio ambayo Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepata katika uboreshaji huduma za afya, elimu na sekta nyingine za kiuchumi yametokana na ushirikiano wa wananchi na Wadau mbalimbali.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Kipekee nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb) kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph M. Nyamhanga, Naibu Makatibu Wakuu Dkt. Dorothy O. Gwajima na Bw. Gerald G. Mweli pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bibi Winifrida G. Rutaindurwa. Aidha, ninawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais -TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika (Mb) na Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri, Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais. Aidha, ninawashukuru sana Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Dkt. Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

189. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kisarawe kwa ushirikiano wanaonipa wakati wote ninapotekeleza majukumu haya ya Kitaifa. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuboresha utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii. Aidha, naishukuru familia yangu kwa uvumilivu muda wote nilipokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu haya ya Kitaifa.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

### Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

190. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 185 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Nane na Sitini, Milioni Mia Sita Themanini na Tatu, Elfu Arobaini na Tisa, Mia Nne Ishirini na Sita (Shilingi 860,683,049,426.00).** Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa mwaka wa fedha 2020/21**

| OFISI/TAASISI | MAKADIRIO |
|---|---|
| Ofisi ya Rais - TAMISEMI | 11,520,000.00 |
| Taasisi | 45,500,839,514.00 |
| Mikoa | 209,698,912.00 |
| Halmashauri | 814,960,990,076.00 |
| **JUMLA KUU** | **860,683,049,426.00** |

191. ***Mheshimiwa Spika,*** sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi Trilioni Saba Bilioni Kumi na Tisa Milioni Mia Nane Laki Tatu Hamsini na Tatu Elfu (Shilingi 7,019,800,353,000.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 02 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 185.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya fedha zinazoombwa, **Shilingi 4,729,880,457,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida yanayojumuisha Mishahara **Shilingi 3,878,738,058,000.00** na **Shilingi 851,142,399,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,289,919,896,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo kati ya hizo **Shilingi 1,296,949,390,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 992,970,506,000.00** ni fedha za nje ***(Mchanganuo wa fedha zinazoombwa katika mwaka wa fedha 2020/21 umeoneshwa katika Jedwali Na. 2).***

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Makisio katika Mafungu 28 ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 |
|---|---|
| Matumizi ya Kawaida Ofisi ya Rais -TAMISEMI | |
| **Mishahara** | |
| Mishahara Makao Makuu | 11,298,245,000 |
| Mishahara ya Taasisi | 42,148,645,000 |
| **Jumla Mishahara Ofisi ya Rais - TAMISEMI** | **53,446,890,000** |
| | |
| **Matumizi Mengineyo** | |
| Makao Makuu | 70,634,361,155 |
| Taasisi | 1,318,869,845 |
| Jumla ya Matumizi Mengineyo | 71,953,231,000 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **125,400,121,000** |
| | |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)** | |
| Mishahara | 8,165,271,000 |
| Matumizi Mengineyo | 6,108,202,000 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida TSC** | **14,273,473,000** |
| | |
| **MIKOA NA HALMASHAURI** | |
| **MIKOA:** | |
| Mishahara | 76,896,293,000 |
| Matumizi Mengineyo | 58,998,656,000 |
| **Jumla ya Matumizi ya Kawaida** | **135,894,949,000** |
| | |
| **HALMASHAURI** | |
| Mishahara | 3,740,229,604,000 |
| Matumizi Mengineyo (SK) | 232,212,477,000 |
| Matumizi Mengineyo (MSM) | 481,869,833,000 |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **4,454,311,914,000** |
| | |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| **OFISI YA RAIS -TAMISEMI** | |
| Fedha za Ndani | 276,534,159,000 |
| Fedha za Nje | 301,513,025,000 |
| **Jumla Maendeleo** | **578,047,184,000** |
| | |
| **TUME YA UTUMISHI WA WALIMU** | |
| Fedha za Ndani | 500,000,000 |
| **Jumla** | **500,000,000** |
| | |
| **MIKOA** | |
| Fedha za Ndani | 57,724,000,000 |
| Fedha za Nje | 28,268,688,000 |
| **Jumla Maendeleo** | **85,992,688,000** |
| | |
| **HALMASHAURI** | |
| Fedha za Ndani (SK) | 629,100,064,000 |
| Fedha za Ndani (MSM) | 333,091,167,000 |
| Fedha za Nje | 663,188,793,000 |
| **Jumla Maendeleo Halmashauri** | **1,625,380,024,000** |
| **JUMLA KUU** | **7,019,800,353,000** |

***SK** - Serikali Kuu na **MSM** - Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa*

193. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi, Mikoa na Halmashauri ambayo ni sehemu ya hotuba hii.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz

195. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

HABARI MICHEZO

# AC MILAN, MIAMI ZAMWANIA SILVA




**MIAMI,** Marekani

KLABU ya David Beckham, Inter Miami ya nchini Marekani, inashindana na AC Milan kuwania saini ya nyota wa Manchester City, David Silva, kwa mujibu wa gazeti la Corriere dello Sport.

Ripoti za nchini Italia zinadai kwamba, Milan tayari imeingia kwenye mazungumzo ya kumsajili Mhispania huyo wakati mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 amefurahia misimu 10 akiwa nchini England, lakini anatarajiwa kuondoka kwenye uwaja wa Etihad, na Milan wamewasiliana na wawakilishi wa mchezaji huyo kukubaliana ada yake.

Hata hivyo, Beckham ambaye anaimiliki klabu ya Inter Miami amekuwa akimfuatilia Silva kwa kumsajili.

Klabu nyingine kwenye Ligi hiyo ya Marekani, MLS, New York City FC pia inawania kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispanial.

Klabu hiyo ikiwa pia inamilikiwa na Manchester City, uhusiano wake unaweza kufanikisha usajili wa mchezaji huyo.

Mwaka 2018 Silva aliweka wazi mipango ya kuondoka City wakati alipoiambia BBC Sport: "Inatagemea na hali jinsi itakavyokuwa."

# Kroos hataki wachezaji wakatwe mishahara

**MADRID,** Hispania

TONI Kroos angepeda kupokea mshahara wake kamili, ambao utamuwezesha kufanya mambo ya 'msingi' na kusaidia sehemu inayohitaji fedha, kuliko kuona wachezaji wakipunguziwa mishahara wakati huu wa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Klabu ya soka zinakabiliwa na wakati mgumu wa kifedha kutokana na mlipuko wa corona, zikipoteza fedha nyingi kutoka na mashindano kusimamishwa.

Akizungumza na televisheni ya SWR, nyota huyo wa Real Madrid alisema kukatwa mishahara ni kama kutoa mchango sehemu isiyo sahihi.

Anaamini kupunguza mishahara kunainufaisha zaidi klabu ambazo tayari zinawalimiki matajiri, wakati fedha hizo zingeweza kutumika sehemu nyingine.

"Wakati mfanyakazi akiwa anaumwa au kwenda likizo bado anaendelea kulipwa mshahara, kwa sababau kukosekana kwake ni kwa muda tu bado ni muajiliwa," alisema.

"Hivyo naamini suala la wachezaji kukatwa mishahara yao sio jambo zuri, kwani haliwasaidii wachezaji bali linazinufaisha klabu."







# Haaland amsifia Solskjaer

**MANCHESTER,** England

ERLING Braut Haaland amedai Ole Gunnar Solskjaer amemsaidia kuwa na uwezo mkubwa mbele ya goli na kujikuta akiwa mmoja wa wamaliziaji bora Ulaya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Norway amekuwa gumzo baada ya kufunga mabao 40 msimu huu akiwa na Red Bull Salzburg na baadae Borussia Dortmund akiwa amejiunga na miamba hao wa soka la Ujerumani, Bundesliga, wakati wa dirisha la Januari mwaka huu.

Haaland alikuwa akihusishwa mno na uhamisho wa kwenda Manchester United mwanzoni mwa mwaka kabla ya tangazo la kushitua kwamba klabu ya Ujerumani imepata saini yake - huku nyota huyo mwenye umri wa miaka 19 akikataa kujiunga na Solskjaer, ambaye alimnoa wakati akiwa kwenye klabu yake ya utotoni ya Molde.

Lakini licha ya kukataa nafasi ya kujiunga na tena na kocha huyo wa United, Haaland amekubali kwamba alikuwa mtu muhimu sana kwenye maendeleo yake ya kisoka - na mchezaji huyo wa zamani alimfundisha jinsi ya kutulia akiwa eneo la penalti.

Akizungumza na Eurosport, alikumbua mchezo wa Molde dhidi ya wapinzani wao wa soka la Norway, Brann, ambao walikuwa na safu ya ulinzi subufu, ambako aliweza kufunga mabao manne ndani ya dakika 20 za kwanza za mchezo.

"Kabla ya mchezo ule, Solskjaer na mimi tulifanya mazoezi ya umaliziaji eneo la hatari," alisema. "Sio pasi tu. Nakumbuka alinifundisha njia rahisi zaidi na sheria zake.

"Alinifundisha kabla ya mchezo na alinifundisha kuwa mtulivu, na kunitaka kuwa makini na nilifuata maelekezo yakee."

## HABARI MICHEZO

# Berbatov amtaka Kane aondoke Spurs

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Dimitar Berbatov, anaamini Harry Kane kufikiria kuondoka Tottenham na kutua pale Old Trafford ni jambo linalowezekana.

Berbatov aliondoka Tottenham na kwenda United kwa ada ya pauni milioni 30.7 mwaka 2008 na akashinda mataji mawili ya Kombe la Ligi Kuu England chini ya utawala wa kocha, Sir Alex Ferguson.

Anafikiria kama Kane kuondoka Tottenham ili kushinda mataji, United ndio sehemu yenye nafasi ya kutimiza ndoto zake.

Berbatov amesema: "Naona hali inafanana na ile niliyopitia mimi na kile kinachotokea kwa Kane.

"Nahisi kwamba ni muda ambao unafanana na mimi wakati wangu wa uchezaji, unatakiwa kufikiria kama upo sehemu sahihi na fikiria kuhusu mambo mengine."

Kane anabakiwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi Ulaya kwa sasa, licha ya kuumia misuli, ambayo imeuweka nje ya dimba tangu Januari kabla ya misimu yote ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 hivi karibu alizungumzia majaliwa yake pale Tottenham na kuonyesha namna gani anavyotaka kushinda mataji.





# RONALDO KURUDI REAL MADRID

**TURIN,** Italia

JUVENTUS ipo tayari kumwachia mchezaji wake nyota, Cristiano Ronaldo, kurudi katika Klabu yake ya zamani ya Real Madrid kwa bei ndogo, kwa mujibu wa gazeti la Corriere dello Sport.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Italia, Juventus, klabu hiyo inaweza kukubali ofa ya kiasi cha pauni milioni 50 kwa raia huyo wa Ureno, baada ya miamba hao wa soka la Hispania kuonyesha kumwania tena.

Mlipuko wa ugonjwa wa corona umesimamisha matukio ya michezo duniani pamoja na soka, na inatarajiwa kuzigharimu klabu fedha nyingi kwa miezi inayokuja.

Viwanja vyote vya michezo vimefungwa duniani kote na Juventus wanaweza kulazmika kuuza baadhi ya bidhaa zake muhimu.

Ronaldo ndiye mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, huku akiwa na mkataba unaomuingizia pauni milioni 27.5 kwa msimu, na unamalizika Juni 2022.

Hata hivyo, wachezaji wa Juventus wamekubali kupungua kwa mishahara yao, ambapo klabu itaweza kupata pauni milioni 80 kwa miezi minne ijayo.

Ronaldo peke yake atapoteza kiasi cha pauni milioni 10 kwa miezi inayokuja. Kwa sasa, hata klabu zenye utajiri mkubwa kama Juventus haiwezi kuhimili madeni ya wachezaji wake bila ya kuhuisha mikataba yao na kuweka mfumo mpya wa malipo kwa siku za usoni.

Wiki iliyopita, mwenyekiti wa Juventus, Andrea Agnelli, alikuwa anajiamini kwamba watafikia makubaliano ya mkataba mpya na Ronaldo utakaomweka hapo hadi mwaka 2024.

Hata hivyo, ripoti ya hivi karibuni inabainisha kwamba, sasa Juventus imefungua mlango kwa Ronaldo kama anataka kurudi Real Madrid.

# *Ronaldinho atolewa jela kwa dhamana*

**ASUNCION,** Paraguay

MCHEZAJI wa zamani wa Barcelona, Ronaldinho, ametolewa gerezani nchini Paraguay baada ya siku 32 kwa kosa la kughushi hati ya kusafiria.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 40 atakwekwa kizuizini nyumbani katika hoteli moja ya mji mkuu wa Paraguay wa Asuncion baada ya kuripotiwa kulipa dhamana ya pauni milioni 1.3.

Wote yeye na kaka yake, Roberto walihukumiwa kwa kuingia nchini humo kwa hati ya kusafiria ya kughushi mwezi uliopita na alihukumiwa kufungwa jela miezi sita.

Lakini Jaji, Gustavo Amarilla amewaruhusu wote kubakia hotelini kwa muda, huku kesi hiyo bado ikiwa imeamuliwa na wakili wa mchezaji huyo anajaribu kukata rufaa maamuzi ya kumfunga jela.

Ilishauriwa kwamba, alitakiwa kutofungwa jela kutokana na umaarufu wake kama mchezaji bora wa zamani, huku wakisema kwamba, kumuweka kizuizini ni kutokumtendea haki.



# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:



## KUPOTEA KWA CHETI



**MUSSA HARID MLWILO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2299-0065 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KITWIRU SEKONDARI mwaka 2013.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MBE/RUJ/RB/212991/2020.

## KUPOTEA KWA CHETI



**Alex I. Ngowi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S/0125/0023 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1996 katika shule ya sekondari Lyamungo .

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Control Number: 991081206014**

## OMBI LA URAIA



**BARBRA DAVID NAIGAGA**

**Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MGANDA. Nchi atokayo UGANDA. Shughuli zake ni MWALIMU. Anwani ya Mwajiri/biashara. Yupo hapa nchini tangu 2008. Pamoja na kuishi DSM pia amewahi kuishi DSM. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. AC: 27/340/2616"B".**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

KAHAMA OIL MILLS LTD ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA TRUCK YENYE NAMBA ZA USAJILI T 278 ADE. YENYE CHASSIS NO 4305408 NA ENGINE NO 03382.

KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/ / TR /RB/ 130/2020.

156934

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI**
**KMAHAKAMA YA MWANZO..DODOMA MJINI**
**WILAYA YA DODOMA**
**MADAI NAMBARI 38/2020**
**MDAI……KARAN DEWAN**
**MDAIWA…… RAHILU HAJI (MAMA CHIKU)**
**KWA ENOCK LUCAS LUKUMBO**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai ya TSH.3,000,000 Hivyo unahitajika/mnahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya jumatatu tarehe 20/04/2020 saa 02:00 asubuhi kwa kujibu madai hayo kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiitetea katika shauri hilo.

Na kama hakuhudhiria/hamkuhudhuria siku ilitajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha umepokea/mmepokea kuitwa kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08/04/2020.

## KUPOTEA KWA CHETI



**JONATHAN MBUNDA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MAKOKA SEKONDARI mwaka 2013.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/MSI/RB/292634/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**Neema Stephano Kidemi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0646-0027 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika shuke ya Sekondari Nkoaranga na cheti cha Chuo kilichotolewa na Chuo cha Bishop Durning Teachers College chenye namba E610/0012 mwaka 2019.

Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa :
**DAR/KIJ/RB/298745/2020**

## OMBI LA URAIA



**CAROLINE MUTHONI NJERU**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo KENYA. Shughuli zake ni MWALIMU. Anwani ya Mwajiri/biashara. Yupo hapa nchini tangu 2008. Pamoja na kuishi DSM pia amewahi kuishi DSM. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. AC: 27/340/2616"C".

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND APPEAL 74/2019**
**TERESPHORY MUGANYIZI ANTHONY……………………APPLICANT**
**VERSUS**
**MERCHARDES OSWALD KALEMELA & ANOTHER………………RESPONDENT**

**TO: RHINO AUCTION MART**
**P.O. Box**
**DAR ES SALAAM.**

WHEREAS: The above named applicant has instituted APPEAL against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by Advocate or agent duly authorized on 24th day APRIL, 2020 at 9.00 am Before Hon. P. MANYANDA JUDGE (Chamber no: 2).

Taken notice that, in default of your appearance on that day the APPEAL will be heard and determined in your absence.

Given under my hand and the seal of this Court, this 17th day of MARCH, 2020.

115693702

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**

**KUPOTEA KWA HATI YA UMILIKI ARDHI**

HATI NAMBARI: 62335
MMILIKI: SELEMANI UMANDE OMARI, WA S.L.P 13997
ARDHI: KIWANJA NA. 64 KITALU NA. 6 MBWENI, KINONDONI

MUOMBAJI: GEKC ATTORNEYS
WA S.L.P-
KINONDONI
DAR ES SALAAM

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya Kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda mwezi mmoja tokea tarehe ya Taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekena, irudishwe kwa,
Msajili wa Hati,
S.L.P 1191,
DAR ES SALAAM

Assistant Register of Titles
DAR ES SALAAM
06—Dec-2019

15693302


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# Mwamnyeto Coastal Union waanza kuagana

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuwapo kwa tetesi za kuwindwa na vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga, Uongozi wa Coastal Union umesema umeanza mchakato wa kusaka mrithi wa beki wao tegemeo, Bakari Mwamnyeto, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kamati ya usajili ya Coastal Union, Hemed Ally 'Aurora', alisema wameanza kujiandaa kisaikolojia kutafuta beki mpya endapo Mwamnyeto ataondoka klabuni hapo baada ya msimu huu kumalizika.

Aurora alisema endapo ataondoka beki huyo, hawatatereka kutokana kujiweka katika nafasi nzuri ya kusajili mchezaji mwingine ambaye ataisaidia Coastal Union kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu Bara na mashindano mengine watakayoshiriki.

"Mwamnyeto ni mchezaji mzuri na tuna imani msimu ujao hatutakuwa naye kutokana na tayari baadhi ya klabu hapa nchini na za nje ya nchi kutaka huduma ya beki huyo, endapo makubalino yakiwa mazuri na Mwamnyeto atafanikiwa kuondoka, tutasajili mbadala wake kutoka kwenye timu ya vijana au nje ya kikosi chetu," alisema Aurora.

Alisema mbali na pengo hilo wanalolitarajia, tayari walishaanza mchakato wa kukiimarisha kikosi chao na sasa wanasubiri rasmi dirisha la usajili kufunguliwa.

Alisema pia Coastal Union itahakikisha inambakisha Kocha wake Mkuu, Juma Mgunda kwa kumpa mkataba mpya wa kuendelea kuinoa timu hiyo.

# Simbu aendelea kujifua Arusha

**Na Shufaa Lyimo**

MWANARIADHA maarufu nchini, Alphonce Simbu, amesema anaendelea kufanya mazoezi chini ya kocha wake raia wa Uingereza ili kulinda kiwango chake wakati huu michezo mbalimbali ikiwa imesimama.

Akizungumza na gazeti hili jana, Simbu alisema kuahirishwa kwa Michezo ya Olimpiki kumemwathiri kisaikolojia kwa kueleza alishakuwa tayari kwenda kushindana kuwania medali.

"Kuahirishwa kwa Olimpiki kumeniathiri sana, nilikuwa nimeshatua nguvu na akili za kwenda kushindana," alisema Simbu.

Mwanariadha huyo aliongeza kwa sasa anaendelea kujiimarisha huku akisubiri uamuzi mwingine mpya kuhusiana na kurejea kwa mashindano mbalimbali duniani.

"Nimeamua kufanya mazoezi mbali na makazi ya watu ili kuepuka msongamano kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona mpaka ratiba mpya itakapopangwa," Simbu alisema.

Aliwataka Watanzania kuendelea kufanya maombi ili janga hilo limalizike na kuwambusha wachezaji wenzake kutojisahau kwa kufanya mazoezi.

# TSHISHIMBI AENDELEA KUIVURUGA SIMBA SC

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya kukataa kufanya mazungumzo ya kumsajili kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi, uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba umemtaja nyota huyo kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kuwa ni kiungo bora kwa sasa hapa nchini.

**Mkataba wa Tshishimbi na Yanga unaelekea ukingoni lakini bado hajakubali kusaini mkataba mpya ambao amepewa na klabu hiyo baada ya kutanguliwa na mazungumzo.**

Hata hivyo taarifa nyingine zinasema kiungo huyo anatembea na mkataba wa Simba na kinachosubiriwa ni kumaliza mkataba wake na Yanga ili atambulishwe rasmi ametua Msimbazi.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema Tshishimbi ana kiwango cha juu na anapokuwa uwanjani anaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Manara alimtaja Tshishimbi kuwa mmoja wa nyota waliojituma na kucheza kwa juhudi katika mchezo wa watani wa jadi uliochezwa Machi 8, mwaka huu ambao Yanga walipata ushindi wa bao 1-0.

"Hakuna ubishi, Tshishimbi ni kiungo bora kwa sasa hapa nchini au katika Ligi Kuu, lakini siwezi kumzungumzia sana kwa sababu ni mchezaji wa Yanga, suala kama anatembea na mkataba wa Simba si kweli," Manara alisema.

Aliongeza alimtumia salamu za heri katika siku yake ya kuzaliwa kwa sababu ni rafiki yake kama ilivyokuwa kwa Mrisho Ngasa na wachezaji wengine maarufu wa hapa nchini.

Kiongozi huyo pia alisema klabu yao imewapiga marufuku wachezaji wao kuzungumza na vyombo vya habari bila ya kupata ruhusa.



Uwanja wa kisasa wa mpira wa miguu unaojengwa na Kampuni ya Juvenile Sports Academy, katika eneo la Shule ya Sekondari ya Nyangao, iliyopo Lindi kwa ajili ya mikoa ya Kanda ya Kusini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kituo cha kisasa chajengwa Kusini

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

ILI kuhakikisha Kanda ya Kusini inafanya vema, Kampuni ya Juvenile Sport Academy, imeanza ujenzi wa kituo cha kisasa cha michezo katika Kanda ya Kusini ili kukuza vipaji mbalimbali vikiwamo vya mchezo wa soka na riadha hapa nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Ally Kamtande, alisema kituo hicho kinajengwa katika Shule ya Sekondari Nyangao iliyopo mkoani hapa.

Kamtande alisema kwa sasa tayari wameshaanza kuboresha eneo la uwanja wa mpira wa miguu kwa kuweka nyasi bandia na malengo yao ikifika Januari mwakani, vijana waanze kuutumia uwanja huo.

Alisema lengo la ujenzi wa kituo hiko ni kuunga mkono juhudi za Serikali ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli, katika kukuza vipaji vya wachezaji chipukizi kwa sababu inafahamu michezo ni ajira.

"Uamuzi wa kujenga kituo hicho katika Shule ya Sekondari Nyangao ulichukuliwa kwa sababu hapa kuna miundombinu rafiki ya kimichezo, hivyo tunawaomba wazazi kutuunga mkono kwa kuwaleta wanafunzi mara kituo hicho kitapofunguliwa," alisema Kamtande.

Kiongozi huyo alisema kituo hicho kitakuwa na makocha wa kisasa wa michezo yote na kimejengwa katika mazingira bora yatakayowawezesha vijana kujifunza kwa usahihi na kufurahia masomo yao.


"Ukanda huu ulikuwa hauna kituo kama hiki hivyo kukamilika kwake kutakuwa mkombozi, ni wajibu wetu wadau wa michezo kuwekeza katika miundombinu ili kuinua vipaji vya watoto wetu kama ambavyo Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ilivyosisitiza," Mkurugenzi huyo alisema.

Kukamilika kwa kituo hicho, kutatoa fursa kwa klabu za Ligi Kuu Bara na kuweka kambi wakati wa maandalizi ya msimu mpya kutokana na huduma zote muhimu zinazotakiwa zitapatikana ikiwamo chumba cha mazoezi ya viungo.

Naye Makamu wa Kwanza wa Rais wa TFF, Athumani Nyamlani alisema wadau wa michezo nchini wanakumbushwa kushirikiana na taasisi nyingine katika kubuni miradi ya aina hiyo yenye lengo la kukuza vipaji.

Nyamlani alisema kwa sasa Tanzania ina mahitaji makubwa katika fani ya michezo yakiwamo ya madaktari wa tiba, makocha, waamuzi, wakufunzi, wataalam wa lishe na na vituo zaidi vya michezo.

Michezo
Alhamisi Aprili 9, 2020
Nipashe




Wakala amtaka Ozil kukomaa UKURASA 30

# KADUGUDA AFUNGUKA MABILIONI YA MO

**●●● Aeleza fedha si tatizo kwa mwekezaji huyo, asisitiza mabadiliko yanahitaji muda, uvumilivu...**

**Na Somoe Ng'itu**

MAFANIKIO! Klabu ya Simba yenye makazi yake Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam, inawaomba wadau wote wa soka nchini kuhakikisha wanashirikiana kufanikisha mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji ya klabu hiyo na kuweka historia hapa nchini, imefahamika.

**Akizungumza jijini jana, Kaimu Mwenyekiti wa Simba, Mwina Kaduguda, alisema kuna changamoto mbalimbali za kiutawala zinazokwamisha kukamilika kwa mchakato huo na hali hiyo inasababishwa na kufuata taratibu za nchi katika kukamilisha mabadiliko hayo.**

Kaduguda alisema ili kuhamia katika mfumo huo mpya ambao utaifanya Simba ijiendeshe kisasa, klabu inatakiwa kukamilisha taratibu za mabadiliko hayo kwa wanachama kuridhia vipengele vilivyopendekezwa kwenye katiba ya klabu hiyo.

Kiongozi huyo alisema Simba na wadau wengine wanatakiwa kukamilisha mfumo huo mapema na kamwe kiasi cha fedha cha Sh. bilioni 20 zinazotakiwa kutolewa na mwekezaji, Mohammed Dewji (MO), sio tatizo kwa mfanyabiashara huyo.

"Narudia tena, bilioni 20 sio tatizo kwa Mohammed, isipokuwa tatizo liko kwenye mabadiliko, kutoka katika mfumo wa akina Kaduguda, Kassim Dewji, Hassan Dalali, na kuweka mfumo ambao utatengeneza utaratibu wa kiutawala ili watakapokuja wengine wataufuata na mtu akijaribu kuja na jipya, ataulizwa hiki umekitoa wapi," Kaduguda alisema.

Alisema Simba ndio klabu pekee Afrika Mashariki na Kati ambayo imethubutu kufanya mabadiliko na timu nyingine zinasubiri kuiga endapo vinara hao wa Ligi Kuu Bara watapata mafanikio kwa sababu wengi hupenda kuiga mambo mazuri.

Katibu Mkuu huyo wa zamani wa Chama cha Soka Tanzania (FAT sasa TFF), alisema matarajio ya Simba ni kufika katika hadhi ambayo TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemkorasia ya Congo -( DRC) au Ismailia ya Misri na mafanikio haya yatapelekea klabu nyingine kubadilisha mifumo yao ya uendeshaji.

"Tunataka kuondoka huku kwenye kuendesha mpira kimazoea, Simba inapofanikiwa basi ujue na Yanga pia itafanikiwa, hakuna klabu au mtu anayeweza kuiga kitu kizuri au kisichokuwa na mafanikio, haiwezekani," Kaduguda alisema.

Alisema pia wanachama wa Simba watakiwa kutokuwa na hofu za wajumbe waliowachagua wanaunda Bodi ya Wakurugenzi imara ambayo ina malengo ya kuona klabu hiyo inatimiza ndoto zake za kuchukua ubingwa wa Afrika badala ya kufikiria kuifunga Yanga pekee.

"Kwanza kupatikana mimi, Mo amepata mtu sahihi, mimi ninaweza kuwa similiki hata baiskeli, lakini kichwani nina madini ya kutosha, tunaweza kusema Mohammed au Simba ilichelewa kunipata," Kaduguda aliongeza.

Kaduguda alisema pia kwa mujibu wa katiba ya klabu hiyo, ataendelea kukaimu nafasi hiyo mpaka mwaka 2022 baada ya mkutano mkuu uliofanyika Desemba 8, 2019 kuridhia mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo ilimteua kuchukua nafasi iliyoachwa na aliyekuwa Mwenyekiti, Swedi Mkwabi.

Naye Ofisa Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliliambia gazeti hili mchakaro wa kubadili mfumo unahitaji muda na haufanyiki haraka kutokana na umuhimu wake katika kufikia malengo.

Aliongeza wakati mfumo bado ukiwa haujakamilika, baadhi ya shughuli za maendeleo kufikia huko zimeshafanyika ikiwamo ujenzi wa viwanja viwili ambavyo zinatumiwa na timu za klabu hiyo.

**KI-CORONA...**



Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Haji Manara, akisalimiana kwa miguu na Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd, eneo la Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Yanga yamsafiria Kisinda

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanafanikiwa kunasa saini ya winga wa As Vita, Tuisila Kisinda, uongozi wa Yanga unatarajia kutuma mwakilishi kwenda Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ili kukamilisha mchakato wa usajili.

Taarifa za uhakika kutoka ndani ya Yanga zinasema tayari wameshajiandaa kumtuma kiongozi mmoja kwenda DRC kumsajili Kisinda kama ilivyopendekezwa na Kocha Mkuu, Luc Eymael.

"Kiongozi mmoja wa GSM anatarajia kusafiri kuelekea Congo, tunasubiri hii corona iishe, kwani tunahitaji kwenda kumalizana na Kisinda, nyota huyo ni mapendekezo ya kocha mwenyewe na pia tutasajili wachezaji wengine wanne wa kimataifa," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza nafasi alizopendekeza kocha huyo ya mshambuliaji, winga, kiungo na beki na tayari mdhamini wao anasimamia masuala ya usajili na kuendelea vizuri na mazungumzo na baadhi ya wachezaji wa ndani.

"Wachezaji hao wengine, tutawataja muda ukifika, kwa sababu sasa sio busara kutaja majina yao kutokana na mambo bado yako mwanzoni, " aliongeza kiongozi huyo.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela aliliambia gazeti hili mchakato wa usajili unaendelea 'kimya kimya' na watahakikisha wanawanasa wachezaji waliopendekezwa na benchi la ufundi.

Bado Yanga haijakata tamaa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa sababu inaamini kwenye soka lolote linaweza kutokea katika mechi 10 zilizosalia za watani zao, Simba.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >